# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

## KIMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA

## KIMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA

### KIMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED

### KUPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU

### UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI

Sura Ya Tano: Al - Maidah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu

### UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhudi ya miaka mingi sana ya watu waliojitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Kama lilivyo jina la Tafsiri yenyewe ndivyo ilivyo Tafsiri yenyewe ambayo mwanachuoni huyu mahiri kabisa aliyeifafanua ni mtu aliyebobea katika fani zote ambazo mfasiri (Mfafanuzi) anatakiwa awe nazo.

Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya ameonesha cheche zake katika vitabu vingi alivyoviandika katika maudhui mbali mbalimbali na hivyo kujipatia wasomaji wengi sana.

Msomi huyu, mwenye fikra huru na anayetetea kile anachokiamini, ni mtu mwenye mawazo mapana na kuyaangalia mambo kwa undani sana, kipaumbele chake ni katika maslahi ya umma huu na amejaribu sana kwenda na wakati.

Sifa kubwa pekee ya mwanachuoni huyu ni kuwa yeye hakujihusisha sana na kung'ang'ania madhehebu fulani tu, labda hii yatokana na wadhifa wake wa ukadhi aliokuwa nao katika nchi ya Lebanon ambayo ina madhehebu mengi, ambapo sula la madhehebu ni nyeti nchini humo, hata hivyo yeye aliweza kuamua matatizo ya watu kwenye ofisi yake kulingana na madhehebu yao pale walipomwendea, hiyo ilimsaidia sana hata kuweza kutoa kitabu kitwacho 'Al-Fiqh a'laa madhaahabil-khamsah' (Fikhi ya madhehebu matano) yaani ya Hanafi, Maaliki, Shafi, Hambali na Shia (ambacho twataraji kitatoka hivi karibuni Inshaallah).

Jambo lililotupa msukumo wa kukifasiri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ni zile faida nyingi atakazozipata msomaji na kujua mambo mengi na ya ajabu yaliyo mapya kwake ambayo si rahisi kuyapata kwa wafasiri wengine.

Msomaji atapata faida katika fani za Sayansi, Siasa, Historia, Mashairi, visa vizuri, na Saikolojia miongoni mwa mengine; ndiyo maana msomaji atashangaa kidogo anapoisoma Tafsiri hii atakapoona mwandishi amewataja na kuwanukuu watu kama kina Mfalme Edward, wanasyansi kama kina Enstein, Charlie Champlin (Mchekeshaji maarufu), na wengineo,vile vile

kutaja nchi mbalimbali zikiwemo za Afrika; kama vile Afrika ya kusini, Zimbabwe nk, hali inayoifanya tafsiri hii kuwa ni ya kipekee kabisa.

Mtindo alioutumia mwandishi ni sahali uliokusudiwa watu wa tabaka mbalimbali, wanavyuoni na watu wa kawaida.

Nia yetu ni kukigawanya kitabu hiki bure lakini tumelazimika kukiuza kwa bei nafuu ili kurudisha gharama za uchapishaji.

**Mwisho**: Shukrani kubwa iwaendee bila ya kuwataja watu waliojitolea usiku na mchana, jopo la wafasiri, wahariri, wachapaji, waliotupa moyo na kutoa maoni yao na walioisimamia ili kuhakikisha kwamba kitabu kimemfikia msomaji.

## MAKOSA YA CHAPA

Sikumbuki kama nimewahi kusoma kitabu kilichotoka kupigwa chapa, cha zamani au cha sasa, bila ya kukuta makosa ya chapa, Nafikiri sitasoma kitabu kisichokuwa hivyo. Nimejaribu sana kuliepuka hilo katika tungo zangu, lakini sikufanikiwa.

Nilikuwa sifikirii kama ninaweza kuona makosa haya katika maandishi ya msahafu mtukufu, kama yale yaliyo katika baadhi ya chapa; kwa mfano neno yabswutu kwa swad, badala ya yabsutu kwa sin, na katika chapa ya Tafsir Arrazi ya Misr ya mwaka 1935, Sura ya (2:146), Imeandikwa La Ya'alamuun, (hawajui) badala ya Ya'alamuun (wanajua). Mfano wa makosa haya hausameheki.

Katika Tafsir Al-Manar, chapa ya Pili, sura (5:212), imeandikwa "Fawqahum ila yawmil qiyama" badala ya "Fawqahum yawamal qiyama" Hatuwezi kusema kosa hili ni kubwa zaidi kuliko lile.

Lakini mkosaji atatuletea udhuru kwa msemo mashuhuri huko kwetu jabal amail 'Makosa ya chapa.'

Katika Tafsiri Majmau chapa ya Urfan, Sura (46:15), imeandikwa: " Hatta idha balagha arbai' na sanah badala ya: Hattaidha balagha ashuddahu arbai ' na sanah"

Kusema hivi sio kama ninajitetea kutokana na makosa ya chapa atakayoyakuta msomaji katika kitabu hiki, ijapokuwa naomba msamaha kama litatokea hili, lakini makusudio yangu hasa ni kumwambia yule atakayefungua macho yake kwenye makosa ya matamko na kuufungia macho uzuri wa maana.

Vilevile ninamwambia yule ambaye siku moja aliniambia: "Vitabu vyako vimejaa makosa ya chapa, kama kwamba hakuna kitu chochote katika vitabu hivyo isipokuwa makosa ya chapa tu. Wote hao ninawaambia: Mungu awasamehe na aniongoze mimi na nyinyi.

Vyovyote iwavyo, mimi ninaomba msamaha kutokana na makosa ya kifikra na ya chapa. Anasema Amirul Muminiin (a.s): **"Watu wote ni wapungufu wenye kuchanganyikiwa, isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu."**

Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye mwenye jukumu la kunikubaliayale niliyoyapatia na kunisamehe niliyakosea, kwa jaha ya Mtume na kizazi chake, ziwashukie rehema na amani (Amin).

**MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYAH**

1

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِّلَّذِينَ آمَنُوا الْيَهُودَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا وَلَتَجِدَنَّ أَقْرَبَهُم مَّوَدَّةً لِّلَّذِينَ
آمَنُوا الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصَارَىٰ ذَٰلِكَ بِأَنَّ مِنْهُمْ قِسِّيسِينَ وَرُهْبَانًا وَأَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ﴾

82. Hakika utawakuta walio shadidi kuliko watu wote katika uadui kwa walio amini ni Mayahudi na washirikina. Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanao sema: Sisi ni Manasara. Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi.

﴿وَإِذَا سَمِعُوا مَا أُنزِلَ إِلَى الرَّسُولِ تَرَىٰ أَعْيُنَهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ مِمَّا عَرَفُوا مِنَ الْحَقِّ يَقُولُونَ
رَبَّنَا آمَنَّا فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ﴾

83. Na wanaposikia yaliyoteremshwa kwa Mtume, utaona macho yao yanamiminika machozi kwa sababu ya haki waliyoitambua, wanasema: Mola wetu tumeamini tuandike pamoja na wanaoshuhudia

﴿وَمَا لَنَا لَا نُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا جَاءَنَا مِنَ الْحَقِّ وَنَطْمَعُ أَن يُدْخِلَنَا رَبُّنَا مَعَ الْقَوْمِ الصَّالِحِينَ﴾

84. Na kwa nini tusimwamini Mwenyezi Mungu na haki iliyotujia, na hali tunatumai Mola atuingize peponi pamoja na watu wema?

﴿فَأَثَابَهُمُ اللَّهُ بِمَا قَالُوا جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَذَٰلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ﴾

85. Basi Mwenyezi Mungu atawalipa, kwa yale waliyosema, Bustani zipitazo chini yake mito, Humo watakaa milele, Na hayo ndiyo malipo ya wafanyao mema.

﴿وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ﴾

86. Na wale waliokufuru na kuzikanusha Aya zetu, hao ndio watu wa motoni

## UADUI WA MAYAHUDI NA URAFIKI WAWAKRISTO

**Aya 82 - 86**

### MAANA

Hakika utawakuta walio maadui zaidi kuliko watu wengine kwa walioamini ni mayahudi na washirikina.

Yaani mayahudi na washirikina ndio waliokuwa maadui zaidi kwa Waislamu. Mara nyingi watu wameitolea ushahidi Aya hii, kuwa dini ya kikristo iko karibu zaidi na Uislam kuliko dini ya kiyahudi. Hilo ni kosa ikiwa inakusudiwa dini ya kiyahudi na ya kikristo kabla ya kugeuzwa. Kwa sababu dini kwa Mwenyezi Mungu na Mitume wake ni moja tu kwa upande wa itikadi na msingi yake. Na kama ikikusudia baada ya kubadilishwa, basi zote mbili ni sawa (Ukristo na Uyahudi) hakuna yenye afadhali.

Usahihi ni kuwa uhasama wa mayahudi na washirikina katika Uislam unatokana na mgongano baina ya mwito wa kiislam na tabia iliyokuwa imeshika kasi katika Bara arabu mwanzo wa utume. Tabia hiyo ilikua ni mashindano ya kupora mali na watumwa. Vilevile riba, ghushi na mengineyo ya kutumia nguvu na utapeli. Tabia hii iliambukiza

wafanyibiashara wa kigeni, kama walivyoambukizwa viongozi wa kiyahudi waliokuwa wakimiliki viwanda na biashara ya ndani.

Ukaja mwito wa Muhammad **(s.a.w.w)** unaohimiza uadilifu na kukataa dhuluma na unyonyaji wa aina zote, na kuzuia unyonyaji wa mayahudi na washirikina. Kutokana na hali hiyo ndipo pande zote mbili zikakutana na kukubaliana kwa pamoja kujiepusha na dini na itikadi na kuungana mkono kupigana na Muhammad **(s.a.w.w)**, adui wa wote wawili.

Kwa ufafanuzi zaidi ni kuwa uadui wa mayahudi na washirikina kwa waislam, ulikuwa ni kwa msukumo wa kidunia na wala sio wa kidini, lakini mayahudi walijificha nyuma ya pazia la dini kwa kujionyesha na unafiki; sawa na wafanyavyo leo watu wanaotafuta chumo la haramu. Zaidi ya hayo ni kuwa mayahudi na washirikina wanashirikiana katika ubaguzi. Lakini washirikina pamoja na ujahili wao walikuwa na moyo usiokuwa mgumu, wakarimu na wenye fikra huru zaidi ya mayahudi. Ndio maana wengi wao wakamwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na ni mayahudi wachache tu ndio waliomwamini Muhammad.

## NI NANI WALIO KARIBU NAWAISLAMU KIMAPENZI

Na utawakuta walio karibu zaidi kwa mapenzi na waumini ni wale waliosema sisi ni wanaswara.

Baadhi wanaichukulia Aya hii na iliyo baada yake ni chombo cha kukoroga mambo, kwamba Uislamu unaelemea mojawapo ya majeshi mawili hivi sasa. Jambo hili ndilo lililotufanya tufafanue Aya hizi nne kwa namna ambayo haitaacha nafasi kwa wale wanaobadilisha mambo.

Hakika mwenye kuziangalia vizuri Aya hizi, hawezi kuwa na hata chembe ya shaka kuwa zinakamilishana na kwamba haifai kabisa kuifasiri moja pekee yake bila ya kuichanganya na wenzake.

Nazo ziko wazi kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakuwafanya bora manaswara, kwa ujumla, kuliko makundi mengine katika kuwa karibu kiurafiki, si kwa umbali wala karibu.

Isipokuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) alikusudia kikundi maalum kutoka manaswara (wakristo) kwa dalili ya kuwa yeye hakuishia hapo tu bali aliendelea kusema: "Hayo ni kwa sababu wako miongoni mwao makasisi na watawa, na kwamba wao hawafanyi kiburi." Tena akaendelea kusema: Na wanaposikia yaliyoteremshwa kwa mtume, utaona macho yao yanamiminika machozi kwa sababu ya haki waliyoitambua; wanasema: "Mola wetu! Tumeamini basi tuandikie pamoja na wanaoshuhudia"

Maana yake ni kuwa miongoni mwa manaswara (wakristo) wako walioujua Uislamu,wakaukubali kwa kutii, kukinai na kwa imani.

Historia inathibitisha hivyo; kama ambavyo inathibitisha chuki ya manaswara kwa Uislam na Waislam. Kwa mfano: Fedheha ya Wataliano huko Tripoli ya Magharibi, na Wafaransa katika Algeria, Tunisia, Morocco na Syria, Vile vile fedheha ya Waingereza katika Misr, Iraq, Sudan n.k.

Na leo hii[1] Marekani wanaaungana na mayahudi katika kulingamiza taifa la Palestina. Wanawapa silaha za kisasa maharamia hawa, kisha wanafanya uchokozi na kudai kuwa wao ndio waliochokozwa na kuungwa mkono na

1 Huo ni mwaka 1967

Marekani katika Baraza la Usalama na Umoja wa mataifa. Hapo Marekani husema: Huu ndio ukweli uadilifu na demokrasia.

Je, baada ya hayo na mengi yasiyokuwa haya, itasemwa kuwa wakristo wote wako karibu kwa urafiki na waislam? Haya hayasemwi ila na mjinga au mwenye kutaka kuwapoteza watu. Kisha mpotezaji huyu atasema nini kuhusu kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"Na kwa nini tusimwamini Mwenyezi Mungu na haki iliyotujia, na hali tunatumai Mola atuingize pamoja na watu wema?."

Haki iliyowajia na kuiamini, ni ile waliyobashiriwa na Isa:

﴿وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِن بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدُ﴾

"Na kutoa Bishara ya Mjumbe atakayekuja baada yangu aitwaye Ahmad" (61:6)

Hayo, bila shaka, yanatiliwa mkazo na kukanushwa na kauli yake Mwenyezi Mungu aliyoifuatilia bila ya upambanuzi wowote isemayo:

Basi Mwenyezi Mungu atawalipa, kwa yale waliyosema, Bustani zipitazo chini yake mito, humo watakaa milele na hayo ndiyo malipo ya wafanyao mema.

Ushahidi wa wema na kulipwa pepo kwa kundi hili la wakristo ni dalili ya mkato ya kusilimu, na kwamba ndilo pekee lililokusudiwa baada ya kusifiwa wema na thawabu.

Ama wakristo ambao wameikana haki baada ya kuijua au wakaipinga bila ya kuangalia dalili zake na ubadhirifu wake, hawa wamekemewa na Mwenyezi Mungu na kuwapa kiaga kwa kusema:

Na wale waliokufuru na kuzikadhibisha Aya zetu hao ndio watu wa Motoni.

**Unaweza kuuliza**: kuwa kauli ya waliokufuru na kuzikadhibisha Aya zetu, inamhusu kila mwenye kukufuru na kukadhibisha. Sasa je, kuna wajihi gani wa kuhusisha wakristo?

**Jibu**: Mfumo wa maneno unafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) baada ya kuahidi pepo wenye kuamini katika wakristo, amewaahidi moto wenye kung'ang'ania ukafiri miongoni mwao. Ameleta neno la jumla, ili kujumuisha kemeo kwa kila mwenye kuihalifu haki na kuipinga, jambo ambao halipingani na yale tuliyoyasema.

Kwa ufupi ni kuwa Aya hii iko wazi kuwa makusduio ni kundi mahsusi katika wakristo - wale waliojua haki na kuiamini. Na kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) atawaingiza peponi kwa sababu ya imani yao na amali yao njema.

Tukikadiria kuwa kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na utawakuta walio karibu kwa mapenzi na waumin ni wale waliosema sisi ni manaswara," inawakusanya wakristo wote, basi itawajibika tuiache dhahiri ya Aya na tuihusishe na wale walioamini katika wao kwa sababu mbili:

**Kwanza**: kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja katika Aya kadhaa kuwa manswara wamemfanyia Mungu washirika, wakaficha jina la Muhammad **(s.a.w.w)** na wakawafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu. Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) akakataza kuwafanya mayahudi na manswara kuwa marafiki. Na akasema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ﴾

"Enyi Mlioamini msiwafanye marafiki mayahudi na manswara" (5:51)

Tukiunganisha Aya hii, na zilizo mfano wa Aya hii, juu ya kauli yake Mwenyezi Mungu na utawakuta walio karibu zaidi kwa mapenzi na waumin ni wale waliosema sisi ni manswara," maana yanakuwa:

﴿مِّنْهُمْ أُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ سَاءَ مَا يَعْمَلُونَ﴾

"Miongoni mwao wako watu washikao njia ya wastani, na wengi wao wanayoyafanya ni mambo mbaya" (5: 66)

**Pili**: ni kuwa wafasiri wanasema, Aya hii tunayoizungumzia ilishuka kwa sababu ya Najashi, mfalme wa Uhabeshi[1] aliyekuwa mnaswara (Mkiristo). Kwani Mtume **(s.a.w.w)** alipoona adhabu inayowapata sahaba zake kutoka kwa washirikina, mwanzo mwanzo wa mwito wa Uislam, aliwaamuru kuhamia Uhabeshi na kuwaambia: "Huko kuna mfalme ambaye hadhulumiwi mbele yake yeyote." Wakaenda huko, miongoni mwao akiwemo Jafar bin Abu Talib. Wakapata amani kwa Najashi na ujirani mwema. Hilo lilikuwa mnamo mwaka wa tano wa kutangazwa Utume.

Zimekuja Hadith Mutawatir kuwa Najashi na Baraza lake, la Mambo ya dini na mambo ya kidunia, walisilimu mikononi mwa Jafar bin Abu Talib baada ya kuwasomea Aya za Qur'an Tukufu na kutaja mazuri ya Uislam. Na kwamba walibubujikwa na machozi waliposikia Aya za Mwenyezi Mungu.

Baada ya hayo tunasema kwamba yule anayetolea ushahidi kauli ya Mwenyezi Mungu (Na utawakuta walio karibu zaidi kwa mapenzi na waumin ni wale waliosema sisi ni manswara) kwamba ukristo na wakristo kwa ujumla wote wako karibu zaidi na Uislamu na waislamu kuliko wengine, na kunyamazia Aya zinazokamilisha Aya hii, anayefanya hivyo huyo hakijui Kitabu cha Mwenyezi Mungu au ni mwenye kujionyesha tu kwa kutaka kuongeza chumvi kwa kuutumia Uislamu na Qur'an au anaweza kuwa ni mhaini anayezitia sumu fikra dhaifu katika Uislamu ili zikubali madai ya maadui wa dini, wanaowasaidia Israil na kuwapongeza kwa uchokozi wao kwa Waarabu na Waislam.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُحَرِّمُوا طَيِّبَاتِ مَا أَحَلَّ ا للَّـهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوا إِنَّ اللَّـهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ﴾

87. Enyi mlioamini! Msiharamishe vizuri alivyowahalalishia Mwenyezi Mungu. Wala msipetuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaopetuka mipaka.

﴿وَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّـهُ حَلَالًا طَيِّبًا وَاتَّقُوا اللَّـهَ الَّذِي أَنتُم بِهِ مُؤْمِنُونَ﴾

88. Na kuleni katika vile alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu vilivyo halali na vizuri, na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye nyinyi mnamwamini.

## MSIHARAMISHE VIZURI

**Aya 87 - 88**

### MAANA

Enyi mlioamini! Msiharamishe vizuri alivyowahalalishia Mwenyezi Mungu.

1 Sasa ni Ethiopia

Wamesema kuwa Aya hii imeshuka kwa Masahaba waliokuwa na hofu sana na Mwenyezi Mungu wakajiharamishia wanawake, vyakula vizuri na mavazi. Wakawa wanaswali usiku na kufunga mchana. Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akawaita na kuwasomea Aya hii, akasema: Ama mimi ninaswali usiku na ninalala, ninafunga na ninafungua na ninawaendea wanawake. Basi atakayejiepusha na mwenendo wangu si katika mimi."

Na kauli yake Mwenyezi Mungu; Wala msipetuke mipaka. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wapetukao mipaka, inafahamisha kuwa kuharamisha halali ni sawa na kuhalalisha haramu, yote mawili ni dhulma na ukiukaji mipaka.

Na kuleni katika vile alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu vilivyo halali na vizuri. Imetangulia tafsir yake katika Juz.2 (2:168)

﴿لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَٰكِن يُؤَاخِذُكُم بِمَا عَقَّدتُّمُ الْأَيْمَانَ ۖ فَكَفَّارَتُهُ إِطْعَامُ عَشَرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعِمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ ۖ فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ ۚ ذَٰلِكَ كَفَّارَةُ أَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ ۚ وَاحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

89. Mwenyezi Mungu hawachukuli kwa viapo vyenu vya upuuzi; lakini anawachukulia kwa mlivyoapa kwa nia. Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa wastani wa mnavyowalisha watu wenu, au kuwavisha au kumwacha huru mtumwa. Na asiyeweza kupata (hayo), basi afunge siku tatu. Hayo ndiyo kafara ya viapo vyenu. Na vichungeni viapo vyenu. Namna hii Mwenyezi Mungu anawabainisha Aya zake ili mpate kushukuru.

## VIAPO VYA UPUUZI

**Aya 89**

### MAANA

Mwenyezi Mungu Hawachukuli kwa viapo vyenu vya upuzi.

Viapo vya upuzi ni kuachia ulimi bila ya kukusudia; kama vile kusema: Hapana wallahi, kumjibu aliyeuliza Je umemwona fulani, au kusema: Sivyo wallah, kumjibu aliyesema: Hutaki hii na Viapo hivi havitiliwi manani wala havina kafara kama mtu akihalifu lile aliloliapia.

Na aliyesema hawezi kuhisabiwa kuwa mwongo, na mtu yeyote hawezi kumwambia umemwapia Mwenyezi Mungu uwongo.

Kwa maneno mengine ni kwamba viapo hivyo havina athari yoyote ya kiapo. Hata hivyo iliyo bora ni kuacha ikiwa mtu hajaghafilika.

Lakini anawachukulia kwa mlivyoapa kwa nia.

Yaani kiapo cha sharia ambacho ni wajibu kukitekeleza na kutiliwa manani, ni kile anachoapa mtu aliyebaleghe mwenye akili timamu, kwa kukusudia, kutaka na kuwa na hiyari.

Wameafikiana kuwa kiapo kinakamilika ikiwa ni kwa kuapa kwa jina la Allah au kwa mojawapo ya majina yake mema, kama vile Khaliq, Razak (Muumbaji na Mruzuku)

Shia na Hanafi wanasema: "Kiapo hakiwi kwa jina la Msahafu na Mtume au Al-Ka'aba, kutokana na Hadith isemayo: **Ambaye ataapa, basi na ape kwa jina la Allah au aache."**

Shafi, Malik au Hambal wanasema: "Kinakuwa kwa jina la Msahafu. Hambali amekua peke yake katika kusema kuwa kinakuwa kwa Mtume vilevile.

Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa wastani wa mnavyowalisha watu wenu, au kuwavisha au kumwacha huru mtumwa.

Akiapa na akavunja kiapo, yaani akifanya lile alililoliapia kuliacha au kuacha lile aliloapia kulifanya, ni wajibu kwake atoe kafara akihiyarishwa baina ya mambo matatu.

**Kwanza**: kuwalisha masikini kumi mlo moja kila mmoja, kwa pamoja au mbali mbali kwa sharti ya kuwa ni mlo wa chakula ambacho aghalabu yeye hula na famlia yake. Inajuzu kumpa masikini kibaba cha chakula badala ya mlo. Makusudio ya masikini, ni yule ambaye ni halali kumpa Zaka, Kibaba ni zaidi kidogo ya 800 gm.

**Pili**: ni kuwavisha masikini kumi. Inatosha ile inayoitwa nguo ya kawaida. Kwa sababu sharia haikuhusisha. Kwa hiyo yakachukulia maana yaliyozoeleka bila ya kutofautisha mpya na ya zamani; mradi tu isiwe imechakaa au iliyochanika.

**Tatu**: ni kumwacha huru mtumwa; wala hakuna utumwa leo.

Na asiyeweza kupata (hayo), basi afunge siku tatu.

Yaani akishindwa kuyapata hayo matatu yaliyotangulia, atafunga siku tatu. Na akishindwa kufunga, basi ataomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu na kutaraji msamaha wake.

Hayo ndiyo kafara ya viapo vyenu.

Hayo ni ishara ya kulisha, kuvisha, kuacha huru mtumwa na kufunga baada ya kushindwa na mambo matatu.

Na vichungeni viapo vyenu. Kuvifanya ni vya kawaida. Kwani kiapo cha Mwenyezi Mungu kina heshima yake na utukufu wake. Mwenyezi Mungu anasema: "Wala msimfanye Mwenyezi Mungu ni pondokeo la viapo vyenu" Juz.2 (2:224)

Kuna Hadith isemayo: **"Hakika Nabii wa Mwenyezi Mungu, Musa aliwaamuru waongo wasiape kwa Mwenyezi Mungu. Na mimi ninawaamuru waongo na wa kweli wasimwapie Mwenyezi Mungu."**

Namna hii Mwenyezi Mungu anawabainishia Aya zake ili mpate kushukuru.

Amesema Razi: "Maana yako wazi." Hata hivyo Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaka kutukumbusha neema za kujua hukumu zake, ili tusizitoe mahali pengine.

2

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنصَابُ وَالْأَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

90. Enyi mlioamini! Hakika pombe na kamari na mizimu na mburuga ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni nayo, ili mpate kufaulu.

﴿إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَن يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَ ن ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ فَهَلْ أَنتُم مُّنتَهُونَ﴾

91. Hakika Shetani anataka kuwaingizia uadui na bughudha baina yenu kwa pombe na kamari na kuwazuia kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kuswali, basi je, mtakoma.

﴿وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَاحْذَرُوا فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُوا أَنَّمَا عَلَىٰ رَسُولِنَا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ﴾

92. Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na tahadharini na mkikengeuka basi jueni kuwa ni juu ya mtume wetu kufikisha (ujumbe) tu waziwazi.

## POMBE NA KAMARI

**Aya 90 - 92**

### MAANA

Enyi mlioamini! Hakika pombe na kamari na mizimu na mburuga ni uchafu katika kazi ya shetani.

Tumezungumzia kwa ufafanuzi kuhusu pombe na kamari katika kufasiri Aya Juz.2 (2:219). Na kuhusu mizimu na Mburuga katika Aya ya 3 ya Sura hii tuliyonayo.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amenasibisha kwa shetani kunywa pombe, kucheza kamari, kuabudu masanamu na kuagulia kwa mburuga. Kwa sababu Shetani ndiye anayapendekeza na kuwaghuri watu kwayo.

Basi jiepusheni nayo ili mpate kufaulu.

Dhamiri ya jiepusheni nayo inarudia uchafu. Hiyo ni amri ya kujiepusha; na amri inafahamisha wajibu, hasa wakati wa kubainisha sababu. Na ameibainisha hapo kuwa sababu ya kujiepusha ni kufaulu. Hata kama kusingekuwa na dalili ya kuharamishwa pombe zaidi ya kuwekwa sawa na kuabudu sanamu, ingelitosha. Sikwambii tena kama tukiunganisha na (2:219, 7:32), Hadith Mutawatir na Ijmai ya Waislamu tangu wakati wa Mtume **(s.a.w.w)** mpaka siku ya mwisho.

Hakika Shetani anataka kuwaingizia uadui na bughudha baina yenu kwa pombe na kamari na kuwazuia kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kuswali.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutilia mkazo uharamu wa pombe na kamari, na akakulinganisha na kuabudu masanamu na akakujaalia ni uchaTafsir fu unaotokana na adui wa mtu, na tena akabainisha kuwa njia ya kujiepusha ni kufaulu, baada ya yote haya. Anaonyesha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwamba kwenye mambo mawili hayo kuna uharibifu mara mbili:

**Kwanza**: wa kijamii - kutoelewana pamoja na kuleta chuki na undani baina ya watu.

**Pili**: ni wa kidini - kuzuia kumkumbuka Mwenyezi Mungu na ibada zake. Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) akataka watu wakome kunywa pombe na kucheza kamari kwa ibara fasaha kabisa Basi je mtakoma?

Uislamu unahimiza kwa mahimizo yote kuwa mtu aungane na Muumba wake na jamii yake, na kwamba mtu mbele ya Mungu na mbele ya watu, awe mwenye kuridhiwa na kuheshimiwa.

Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume kwa kuacha pombe na kamari na mengineyo yaliyoharamishwa.

Na tahadharini isije ikawapata adhabu ya Mwenyezi Mungu, kama mkihalifu amri yake na amri ya Mtume wake. Imam Aliy (a.s) anasema:

**"Mwenye kuinasihi nafsi yake zaidi ya watu (wote) ni yule anayemtii Mola wake zaidi yao. Na mwenye kuihadaa nafsi yake zaidi ya watu (wote) ni yule mwenye kuasi zaidi yao."**

Na mkikengeuka basi jueni kuwa ni juu ya Mtume wetu kufikisha tu (ujumbe) waziwazi.

Naye ametekeleza kikamilifu, akasimamisha hoja na kutoka katika jukumu la kufikisha. Atakayehalifu ni yeye peke yake na jukumu lake.

﴿لَيْسَ عَلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جُنَاحٌ فِيمَا طَعِمُوا إِذَا مَا اتَّقَوا وَّآمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ثُمَّ اتَّقَوا وَّآمَنُوا ثُمَّ اتَّقَوا وَّأَحْسَنُوا وَاللَّـهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ﴾

93. Si dhambi juu ya wale walioamini na wakatenda mema wa vile walivyovila maadamu wakiwa na takua na wakiamini na wakitenda mema, tena wakawa na takua na wakaamini, tena wakawa na takua na wakafanya mazuri, Na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao mazuri.

## WENYE TAKUA NA KUAMINI

**Aya 93**

### MAANA

Wafasiri wameafikiana kwamba iliposhuka Aya ya kuharamisha pombe, baadhi ya Masahaba walimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: Itakuwaje kwa ndugu zetu waliokufa wakiwa wanywaji?

Ndipo ikashuka Aya hii ambayo kwa ujumla inafahamisha kuwa mwenye kunywa pombe kabla ya kubainishwa hukumu yake, hapana vibaya juu yake ikiwa ni katika waumini wanaomcha Mungu. Kuanzia hapa ndipo mafakihi wakaafikiana kwamba kila kitu ni halali mpaka kikatazwe.

Baada ya kuafikiana wafasiri kuwa maana haya ndiyo makusudio katika Aya walihitalifiana katika sababu zinazowajibisha kukaririka takua mara tatu; ambapo mara ya kwanza kumetajwa, pamoja na Imani na amali njema, mara ya pili pamoja na Imani tu na mara ya tatu pamoja na uzuri.

Razi amenukuu, katika hilo, kauli tano. Mwenye Majmaul-bayan akasema: Makusudio ya takua ya kwanza ni kuacha kunywa pombe baada ya kuharamishwa; ya pili ni kudumu juu ya hilo na ya tatu ni kuacha maasi yote pamoja na kufanya mema.

Mmoja wa wafasiri wapya anasema: "Nafsi yangu bado haijatulia na chochote katika tafsir hii; wala Mwenyezi Mungu hajanifungulia chochote. Tunavyofikiria sisi - Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi - ni kwamba lengo

la kukaririka huku ni kubainisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwamba mwenye takua ya kweli ni yule anayemcha Mwenyezi Mungu katika hali zake zote, ujana, uzee na ukongwe, na katika dhiki na faraja. Na kwamba mwenye kufa juu ya hilo basi yuko katika amani na usalama.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَيَبْلُوَنَّكُمُ اللَّـهُ بِشَيْءٍ مِّنَ الصَّيْدِ تَنَالُهُ أَيْدِيكُمْ وَرِمَاحُكُمْ لِيَعْلَمَ اللَّـهُ مَن يَخَافُهُ بِالْغَيْبِ فَمَنِ اعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾

94. Enyi mlioamini! Hakika Mwenyezi Mungu atawajaribu kwa baadhi ya mawindo yatakayofikiwa na mikono yenu na mikuki yenu, ili Mwenyezi Mungu amjue ni nani anayemwogopa kwa ghaibu, Basi atakayeruka mipaka baada ya hayo, atapata adhabu iumizayo.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَأَنتُمْ حُرُمٌ وَمَن قَتَلَهُ مِنكُم مُّتَعَمِّدًا فَجَزَاءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعَمِ يَحْكُمُ بِهِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ هَدْيًا بَالِغَ الْكَعْبَةِ أَوْ كَفَّارَةٌ طَعَامُ مَسَاكِينَ أَوْ عَدْلُ ذَٰلِكَ صِيَامًا لِّيَذُوقَ وَبَالَ أَمْرِهِ عَفَا اللَّـهُ عَمَّا سَلَفَ وَمَنْ عَادَ فَيَنتَقِمُ اللَّـهُ مِنْهُ وَ اللَّـهُ عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ﴾

95. Enyi Mlioamini! Msiue windo na hali mko katika Ihram. Na miongoni mwenu atakayemuua kwa kusudi, basi malipo (yake) yatakuwa ni mfano wa aliyemuua katika wanyama wa kufugwa, kama watavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu, mnyama apelekwe Al-kaaba (kama sadaka); au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini; au badala ya hayo ni kufunga; ili aonje ubaya wa jambo lake. Mwenyezi Mungu amekwisha yasamehe yaliyopita; na atakayerudia, Mwenyezi Mungu atampa adhabu; na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye nguvu mwenye kuadhibu.

﴿أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهُ مَتَاعًا لَّكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ وَحُرِّمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ الْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرُمًا وَاتَّقُوا اللَّـهَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ﴾

96. Mmehalalishiwa kuvua baharini na chakula chake, kwa manufaa yenu na kwa wasafiri. Na mmeharamishiwa kuwinda bara maadamu mko katika Ihram, Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwake mtakusanywa.

## HAKUNA KUWINDA KATIKA HARAM WALA PAMOJA NA IHRAM

**Aya 94 - 96**

### MAANA

Enyi Mlioamini! Hakika Mwenyezi Mungu atawajaribu kwa baadhi ya mawindo yanayofikiwa na mikono yenu na mikuki yenu.

Makusudio ya baadhi ni mawindo ya bara tu. Kauli yake Mwenyezi Mungu yanayoafikiwa na mikono yenu na mikuki" ni fumbo la kuwinda, bila ya shaka. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameharamisha kuwinda bara katika Haram[1] na katika hali ya Ihram[2] jambo ambalo ni jepesi; sawa na alivyowaharimishia Wana wa Israil kuvua samaki siku ya Jumamosi (sabato).

1 Haram ni eneo la Al-Kaaba na pambizoni mwake.
2 Ihram ni hali maalum anayokuwa nayo Hujaji (mwenye kuhiji).

Ili Mwenyezi Mungu amjue ni nani anayemwogopa kwa ghaibu.

Yaani Mwenyezi Mungu amewajaribu kwa kuharamisha kuwinda katika hali hii ili ampambanue yule anayemwogopa katika siri kama yule anayemtii katika dhahiri na yule anayejionyesha kwa kumtii na kumwogopa mbele ya watu na kumwasi katika uficho.

Basi atakayeruka mipaka baada ya hayo, atapata adhabu iumizayo.

Yaani mwenye kuhalifu amri ya Mwenyezi Mungu kwa kuwinda baada ya ubainifu huu na hoja, basi atastahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu na mateso.

### MAANA YA KUJARIBU KWA MWENYEZI MUNGU

**Unaweza kuuliza**: kuwa kwa Mwenyezi Mungu halifichiki lolote lilo katika ardhi wala katika mbingu; sasa kuna wajihi gani wa kauli yake Mwenyezi Mungu: "Hakika Mwenyezi Mungu atawajaribu, na kauli yake: "Ili Mwenyezi Mungu amjue anayemwogopa"

**Jibu**: Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) hamjaribu mja wake ili ajue ambayo hakuwa akijua, hapana! Kwani yeye anamjua zaidi kuliko yeye mwenyewe. Isipokuwa anamtia mtihani kwa mambo mengi; kama haya yafuatayo:-

Kuyafasiri yale yalioko katika nafsi ya mja yajitokeze. Ambapo hekima imepitishwa kutowahisabu watu kwa yale anayoyajua kwao wala yale yanayokuwa katika nafsi zao katika silika. Isipokuwa atawahisabu na matukio ya matendo. Silika ya kinafsi peke yake haina haja ya kuhisabiwa wala kupewa adhabu, maadam iko ndani tu ya binadamu na athari yake haionekani kwa macho au kusikiwa kwa masikio.

Imam Ali (a.s) anasema: "Mwenyezi Mungu anasema: Jueni kuwa mali zenu na watoto wenu ni fitna. Maana yake ni kuwa anawajaribu kwa mali na watoto ili abainike mwenye kuichukia riziki yake na mwenye kuridhia ugawanyo wake, ingawaje Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni mjuzi zaidi kuliko nafsi zao, lakini ni kudhihirisha vitendo ambavyo vinastahiki thawabu na adhabu.

Kumpambanua mwovu na mwema na kuidhihirisha hakika yake mbele ya watu na kumchukulia vile anavyostahiki. Na hayo, mara nyingi sana, hutokea katika maisha ya watu.

Kwa mfano wewe unajua Zedi ni katika watu wa elimu na maarifa. Ikawa yeye yuko baina ya watu wasiojua ujuzi wake, nawe ukataka wajue mwamko wake na elimu yake. Kwa hiyo ukamuuliza mbele ya watu, ili aseme na ajulikane.

Au pengine unajua kwamba yeye ni duni mjinga, na watu wanamdhania kuwa ni mjuzi mwenye hekima. Kwa hiyo ukafanya hivyo hivyo udhihirishe ujinga wake na uduni wake.

Watu wengi wao wenyewe hawajijui na wanasema : lau tungelikuwa na hali fulani, basi tungefanya kadha wa kadha. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu huwapa uwezo na fursa ili awe na hoja juu yao na ijulikane hakika yao na hali yao. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَمِنْهُم مَّنْ عَاهَدَ اللَّـهَ لَئِنْ آتَانَا مِن فَضْلِهِ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٥﴾ فَلَمَّا
آتَاهُم مِّن فَضْلِهِ بَخِلُوا بِهِ وَتَوَلَّوا وَّهُم مُّعْرِضُونَ﴾

"Na miongoni mwao wako waliomwahidi Mwenyezi Mungu kuwa: Akitupa katika fadhila zake, kwa hakika tutatoa sadaka na kwa hakika tutakuwa katika wanaotenda mema. Alipowapa katika fadhila yake wakaifanyia ubakhili na wakageuka na huku wao wanapuuza" (9:75-76)

Wana wa Israil walimtaka Musa awafanyie siku ya kupumzika na kufanya ibada, Mwenyezi Mungu akawajaalia siku ya Jumamosi (sabato).

Wakaahidi kutofanya chochote siku hiyo; kama walivyotaka, lakini ikawa samaki wanawajia sana siku hii na inapokwisha Jumamosi na samaki nao hupotea. Wana wa Israil wakafanya hila ya kuwavua na wakavunja ahadi.

Kwa hiyo kwenye wajihi wa kwanza tulioueleza - kudhihiri vitendo vinavyostahiki thawabu na adhabu, ndiyo yamechukuliwa maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu "Hakika atawajaribu Mwenyezi Mungu, ili amjue Mwenyezi Mungu anayemwogopa. Na ili awajue Mwenyezi Mungu wale walioamini" na mfano wa Aya hii.

Enyi mlioamini! Msiue windo na hali mko katika Ihram.

Wameafikiana Mafakihi kwamba kuwinda ndani ya Haram haijuzu kwa aliye katika Ihram na asiye katika Ihram. Ama nje ya Haram inajuzu kuwinda kwa asiyekuwa katika Ihram. Lau atachinja aliye katika Ihram windo basi litakuwa ni mfu ulio haramu kuliwa na watu wote.

Imeelezwa katika Kitab Fiqhu Sunna cha Sayyid Sabiq kwamba mpaka wa Haram ya Makka kwa upande wa Kaskazini ni sehemu inayaoitwa Tani'm, kilomita 6 kutoka Makka. Upande wa kusini ni mahali panapoitwa Ardhah, kilomita 12. Upande wa Mashariki ni Ja'rana kilomita 15.

Na miongoni mwenu atakayemua kwa kusudi, basi malipo (yake) yatakuwa ni mfano wa aliyemuua katika wanyama wa kufugwa, kama watakavyo hukumu waadilifu wawili miongoni mwenu. Mnyama apelekwe Al-K'aaba (kama sadaka); au kutoa kafara kwa kuwalisha masikini au badala ya hayo ni kufunga.

Mwenye kuwa katika Ihram akiuwa, au akiwa hayuko katika Ihram, lakini ameuwa ndani ya haramu, basi ikiwa mnyama aliyemuuwa ana mfano katika aina tatu za wanyama wa kufugwa - Ngamia, Ngombe, Kondo au Mbuzi, basi atakuwa na hiyari ya kuchinja mfano wa mnyama aliyeuliwa na mtoe sadaka; au kutoa thamani ya mnyama anyefanana na aliyemuua. Anunue chakula na kukitoa sadaka kwa masikini kila masikini vibaba viwili, kilogram 1.6 takriba. Wengine wamesema kuwa atatoa kibaba kimoja, au afunge kwa kila vibaba viwili siku moja, au kwa kila kibaba kimoja kulingana na kauli nyingine.

Maana ya "Kama watakavyohukumu waadiifu wawili" ni kushuhudia watu wawili waadilifu, kuwa mnyama huyu wa kufuga ni sawa na mnyama aliyeuawa.

Maana ya "Mnyama apelekwe Al-Kaaba" ni kuchinjwa huyo mnyama jirani ya Al-Kaaba na kutolewa nyama yake kwa masikini.

Ikiwa hakupata mfano katika aina zile tatu za wanyama wa kufugwa, basi atatoa kima cha mnyama mwingine wa kufugwa na anunue chakula na kukitoa sadaka; au kufunga, kwa ufafanuzi uliotangulia.

Ili aonaje ubaya wa jambo lake.

Kuwinda katika Haram au katika hali ya Ihram ni kuvunja mwiko wa Mwenyezi Mungu, kwa hiyo ndio akaadhibiwa mwindaji kwa kafara hiyo iliyotajwa. Maana ya ubaya wa jambo lake, ni mwisho wa kitendo chake kibaya.

Mwenyezi Mungu amekwishayasamehe yaliyopita; ya kuwinda kabla ya kuharamishwa. Na atakayerudia kuwinda, Mwenyezi Mungu atampa adhabu kwa kung'ang'ania kwake dhambi.

Mmehalalishiwa kuvua baharini na chakula chake, kwa manufaa yenu na kwa wasafiri.

Dhamiri katika chakula chake inarudia bahari, kwa sababu mna vinavyoliwa visivyo vuliwa. Inawezekana kuwa dhamiri inarudia kinachovuliwa; na maana yawe Mwenyezi Mungu (s.w.t) amehalalisha kuvua na kula vilevile. Makusudio ya wasafiri ni wale wasiokuwa katika Ihram.

Na mmeharamishiwa kuwinda bara maadamu mko katika Ihram.

Yaani kuvua baharini ni halali kwa hali yoyote. Imam Jafar Assadiq (a.s) anasema: **Usihalalishe chochote katika mawindo - ya bara - ukiwa katika Ihram. Wala usipokuwa katika Ihram pia usimfahamishe aliye katika Ihram au asiye katika Ihram, akawinda na wala usimwonyeshe kwani katika hayo kuna fidia kwa mwenye kufanya makusudi.**

Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwake mtakusanywa.

Yaani jitahidi ni katika kumtii na kutafuta radhi zake, ili awalipe wema siku ya ufufuo.

3

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿جَعَلَ اللَّـهُ الْكَعْبَةَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ قِيَامًا لِّلنَّاسِ وَالشَّهْرَ الْحَرَامَ وَالْهَدْيَ وَالْقَلَائِدَ ذَٰلِكَ لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّـهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَنَّ اللَّـهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ﴾

97. Mwenyezi Mungu amefanya Al-Kaaba nyumba tukufu, kuwa ni kisimamo cha watu na miezi mitukufu na wanyama wa kuchinja na vigwe; hayo ni kwa sababu mjue kuwa Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

﴿اعْلَمُوا أَنَّ اللَّـهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ وَأَنَّ اللَّـهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

98. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu na kwamba Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira, Mwingi wa kurehemu.

﴿مَّا عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا الْبَلَاغُ وَاللَّـهُ يَعْلَمُ مَا تُبْدُونَ وَمَا تَكْتُمُونَ﴾

99. Haimlazimu Mtume ila kufikisha tu, na Mwenyezi Mungu anajua mnayo yadhihirisha na mnayoyaficha.

## NYUMBA TAKATIFU

**Aya 97-99**

### MAANA

Mwenyezi Mungu ameifanya Al-Kaaba, nyumba takatifu, kuwa ni kisimamo cha watu na miezi mitakatifu na wanyama wa kuchinja na vigwe.

Kisimamo cha watu; yaani mahali pa ibada na ibada za Hijja. Miezi mitakatifu ni ile minne Rajab, Dhul-qa'da, Dhul-Hijja na Muharram[1] Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameharamisha kupigana huko na katika miezi hiyo; ispokuwa kutetea nafsi au mali. Anasema:

﴿وَلَا تُقَاتِلُوهُمْ عِندَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ حَتَّىٰ يُقَاتِلُوكُمْ فِيهِ﴾

"Wala msipigane nao karibu na Msikiti Mtakatifu mpaka wakupigeni huko" (2:191) Na akasema tena:

﴿الشَّهْرُ الْحَرَامُ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ وَالْحُرُمَاتُ قِصَاصٌ فَمَنِ اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَاعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ﴾

"Mwezi mtakatifu kwa mwezi mtakatifu; na vitu vitakatifu vina kisasi. Basi wanaowachokoza, pia nanyi wachokozeni kwa kadiri walivyowachokoza" (2:194)

Mnyama wa kuchinja, ni wale wanaochinjwa Makka. Na kigwe ni ukambaa anaofungwa nao mnyama wa kuchinja kuwa ni alama ya kufahamisha kuwa ni wa Al-Kaaba ili asitaradhiwe na yeyote. Kwa hiyo kuunganisha vigwe kwa wanyama ni kuunganisha maalum katika ujumla.

Makusudio ya kutaja chinjo pamoja na Nyumba takatifu na miezi mitakatifu ni kwamba mnyama wa kuchinja inapasa awe salama yeye na anayemchunga, kwa sababu yeye anakusudia Haram tukufu.

---

1 Mfunguo kumi, Mfunguo pili, mfunguo tatu na mfunguo nne.

Bali ni kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewapa amani ndege na wanyama walio katika haramu yake; isipokuwa mwewe, kipanga, kunguru, panya, nge, mbwa anayeuma watu na kila tunayemuona anaudhi.

Hayo ni kwa sababu mjue kuwa Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo mbinguni na yaliyomo ardhini na kwamba Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kubainisha miko ya Al-Kaaba, miezi mitukufu na wanyama wa kuchinja, anaashiria kwamba hekima ya sharia hii ni kuwa watu wajue kwamba Mwenyezi Mungu anajua ufafanuzi wa mambo katika ardhi na katika mbingu; na ambayo yana masilahi kwa watu katika dini yao na dunia yao.

Kuna masilahi gani makubwa zaidi ya usalama wa maisha ya mtu na mali yake ijapokuwa ni kwa kipindi fulani. Tumeyaona mataifa makubwa yanayotwangana, wakati huu, yakiafikiana kuwa baadhi ya miji iwe ni maeneo maalumu ya amani, haijuzu kwa taifa linalopigana kuishirikisha katika vita wala kuweka vituo vya kijeshi katika ardhi hiyo au kupita wanajeshi wake.

Jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu na kwamba Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekutanisha adhabu na rehema na maghufira ili mja awe anahofia adhabu yake na kutaraji rehema yake. Kwa sababu mja, akiwa na hofu atajiepusha na maasi na akiwa na matarajio atajitahidi katika twaa.

Razi anasema: "Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja kuwa yeye ni mkali wa kuadhibu, kisha akafuatishia kwa wasifu wa rehema na maghufira. Na huu ni uzinduzi juu ya undani kuwa kupatikana kiumbe ni kwa ajili ya rehema. Na kwa dhahiri ni kuwa mwisho hauwi ila kwa rehema" Hiyo ni kweli kabisa.

Haimlazimu Mtume ila kufikisha tu.

Hatakiwi jingine zaidi ya hilo, ambapo hapana udhuru baada ya kufikisha kwa anayepuuza na kupetuka mpaka. Ama hisabu na adhabu hiyo ni juu ya Mwenyezi Mungu pekee Yake. Mwenyezi Mungu anasema:

"Hakika ni juu yako kufikisha tu, na ni juu yetu hisabu." (13:40)

Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyadhihirisha katika kauli na vitendo na mnayoyaficha. Haya ni makemeo kwa anayeinyamazia haki, na hasa yule anayeifanyia biashara kwa kujipanua na jina la dini na la nchi.

﴿قُل لَّا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيثِ فَاتَّقُوا اللَّـهَ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

100. Sema: Hawi sawa habithi na mwema, hata ukikupendeza wingi wa habith, Basi mcheni Mwenyezi Mungu enyi wenye akili ili mpate kufaulu.

## WINGI WA MWOVU

**Aya 100**

### MAANA

Aya hii inarudufu Aya ile isemayo:

﴿لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفَائِزُونَ﴾

"Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi, watu wa Peponi ndio wenye kufuzu" (59:20)

Wingi wa habithi ni anayoyamiliki miongoni mwa jaha na mali. Mwenye akili hawezi kumweka sawa habithi, na mwema hata kama ana mali nyingi na jaha kubwa. Kwa sababu jaha na mali hazimfanyi mwovu kuwa mwema; wala ufakiri na udhaifu haumfanyi mwema kuwa mwovu.

Mtu habith katika kipimo cha dini ni yule anayeasi hukumu za Mwenyezi Mungu katika kitabu chake na Sunna za Mtume wake. Na katika desturi ya watu ni yule wanayemhofia kwa shari yake na wasiyemwamini kwa jambo lolote na kutomsadiki katika kauli au vitendo vyake. Kimsingi ni kwamba mwenye sifa hizi, ni mbaya pia mbele ya Mwenyezi Mungu. Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema: **"Utukufu zaidi wa imani ni kuaminiwa na watu."** Ama mtu mwema ni yule aliye kinyume cha mtu habithi katika sifa zake zote.

### JE RIZIKI NI BAHATI AU MAJAALIWA?

**Unaweza kuuliza**: Ikiwa habithi anachukiwa na Mwenyezi Mungu na mwema anaridhiwa na Mwenyezi Mungu, kwa nini basi habithi anafaulu katika maisha haya na kuneemeshwa kwa jaha na utajiri, na mwema anaanguka na wala hapati matakwa yake?

**Jibu**: Maisha yana desturi na kanuni zinazokwenda nayo, na hazigeuki kwa hali yoyote ile. Kwa sababu hisia na uoni unakataa mkorogano katika ulimwengu. Desturi na kanuni hizi ni katika matengenezo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: Kwa sababu yeye ni muumbaji wa asili na vilivyomo katika asili.

Kimsingi ni kuwa desturi ya kawaida ya tabia inakataa kuwa mali, afya na ilimu, vishuke tu kutoka mbinguni. Isipokuwa vitu hivi na mfano wake vinakuja kwa njia zake na sababu zake za kimaumbile. Elimu inatokana na kujifundisha, afya inatokana na lishe na kinga, na mali inatokana na kazi. Kwa hiyo mwenye kujifunza hujua, mwenye kujiepusha na visababishi vya maradhi husalimika, mwenye kujinyonga atakufa tu; awe mwema au mwovu, mumin au kafiri.

Kwa hiyo wema au imani hauoteshi ngano wala hauponeshi ugonjwa wala haumfanyi asiyejua kuwa mjuzi, Yote haya na mfano wake yanakwenda kwa desturi ya tabia na desturi ya tabia inakwenda kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu, hilo halina shaka.

Kwa sababu yeye ndiye aliyejaalia kujifundisha ndio sababu ya elimu na kujikinga ndio sababu ya afya na kupanda kuwa ndio sababu ya kuvuna. Yeye ni Muumba wa kila kitu na kwake yeye ni mwishilio wa kila jambo.

Ndiyo! kuchuma mali kuna njia nyingi, na milango mingi, nyingine Mwenyezi Mungu amezihalalisha na nyingine akaziharamisha. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amehalalisha biashara, kilimo na viwanda; na akaharamisha riba, utapeli, rushwa, kupora na ulanguzi.

Mwenye kuchuma mali kwa njia ya halali hunasibishwa chumo lake kwake, kwa sababu yeye amejitahidi na kufanya bidii kuitafuta, na vilevile hunasabishwa kwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu yeye ndiye aliyepitisha sababu hizi na kuzihalalisha kwa kila azitakaye, awe mwema au mwovu.

Ama mwenye kuchuma mali kwa njia za haramu; kama vile riba na unyang'anyi; chumo lake litanasibishwa kwake na kwa hali aliyoitumia,

wala halinasibishwi kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu ameharamisha njia hizi kwa mwema na mwovu.

**Utasema**: Haya yote ni kweli, lakini hayajibu swali wala hayatatui mushkeli. Tumewahi kumuona mwema na mwovu wote wakifuata njia za sharia za riziki, na kuzitafuta riziki kwa njia zile alizozihalalisha Mwenyezi Mungu na kuziharamisha, lakini pamoja na hayo, riziki inakuwa zaidi kwa mwovu aliye habith na kuwa dhiki kwa mwema, pengine huyu mwema ametoa juhudi maradufu ya yule mwovu, bali mara nyingine riziki humjia mwovu bila ya kutazamia wala maandalizi au juhudi, na inazuilika kumwendea mwema anapoitazamia na kuifanyia maandalizi na juhudi?

**Jibu**: Baadhi ya watu wanakimbilia kulifasiri hilo kwa kusema ni sadfa au bahati. Hakuna kinachofahamika kutokana na maelezo hayo zaidi ya kushindwa kwao kutoa tafsiri sahihi. Vinginevyo wasingelikimbilia kwenye maelezo ya kubahatisha tu.

Kwa hiyo sisi tunapinga Sadfa na bahati na tunaamini kwa imani ya mkato kwamba kuna chaguo la juu linajiingiza kwa sababu tusizozijua. kwa vile elimu katika masuala hayo na mfano wake, bado ni changa. Na kushindwa kwa elimu hakumaanishi kuwa kitu hakiko. Imani yetu hii inatiliwa mkazo na kauli zake Mwenyezi Mungu zifuatazo:

﴿وَاللَّـهُ فَضَّلَ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ فِي الرِّزْقِ﴾

"Na Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kuliko wengine katika riziki" (16:71)

﴿اللَّـهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ﴾

"Mwenyezi Mungu hukunjua riziki kwa amtakaye na huidhikisha (13:26) Aya hii imekuja kwa herufi zake katika 17:30, 28:82, 29:62, 30:37, 34: 36, 34: 39, 39:52, 42:12.

Kwa hiyo basi aliyesema au anayesema: Mwenyezi Mungu amemtajirisha fulani kwa kuwa yeye ni mwema basi atakuwa anazungumza mantiki ya Firaun na kupima kwa kipimo cha Shetani. Hekima yake Mwenyezi Mungu Mtukufu imetaka kumlipa mwema malipo mazuri na kumwadhibu mwovu katika akhera inayobakia sio katika hii dunia inayokwisha. Hii ni Nyumba ya matendo na ile ni Nyumba ya Hisabu. Zaidi ya haya ni kuwa wingi wa mali wa mwovu huenda ukawa ni balaa kwake na sababu ya kuadhibiwa kwake. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ذَرْهُمْ يَأْكُلُوا وَيَتَمَتَّعُوا وَيُلْهِهِمُ الْأَمَلُ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ﴾

"Waache wale na wafurahi na iwazuge tamaa, watakuja jua." (15:3)

﴿يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ وَالنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ﴾

"Hujistarehesha na hula kama walivyo wanyama, na moto ndio makazi yao." (47:12)

Kwa ufupi ni kwamba riziki inategemea mambo mawili. Kuhangaika na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Asiyehangaika ataishi omba omba; na mwenye kuhangaika Mwenyezi Mungu humruzuku kutokana na bidii yake, akitaka humpa nyingi na akitaka humpa chache.

Uhakika huu umo katika maumbile ya binadamu na anaufanya bila ya kujitambua. Mfanya biashara humwomba Mwenyezi Mungu (s.w.t) amruzuku kupata soko zuri la bidhaa zake na watu wazikubali. Mkulima

anamwomba Mungu aiteremshie mimea yake mvua; wala hamuombi kumwoteshea mimea bila ya mvua.

Mimi hapa namwomba Mwenyezi Mungu ampe tawfiq mwanangu katika masomo yake na kufaulu mtihani; wala si mwombi akipe mawazo chuo kikuu kimpatie shahada bila ya kusoma na kufanya mtihani. Iko methali isemayo: Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

Pengine inawezekana mahangaiko yasiambulie kitu, lakini pamoja na hayo inatakikana kupanga mipango na kuongeza juhudi. Kwa sababu kuongeza juhudi, kutumia mipango, na kuvumilia tabu ni sababu ya matakwa ya kufaulu kutoka kwake Mwenyezi Mungu Mtukufu.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَسْأَلُوا عَنْ أَشْيَاءَ إِن تُبْدَ لَكُمْ تَسُؤْكُمْ وَإِن تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنَزَّلُ
الْقُرْآنُ تُبْدَ لَكُمْ عَفَا اللَّـهُ عَنْهَا وَاللَّـهُ غَفُورٌ حَلِيمٌ﴾

101. Enyi Mlioamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatawachukiza. Na mnapoyauliza inapoteremshwa Qur'an mtabainishiwa. Mwenyezi Mungu ameyasamehe hayo. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira Mpole.

﴿قَدْ سَأَلَهَا قَوْمٌ مِّن قَبْلِكُمْ ثُمَّ أَصْبَحُوا بِهَا كَافِرِينَ﴾

102. Waliyauliza watu waliokuwa kabla yenu kisha wakawa makafiri kwayo.

## MSIULIZEULIZE MAMBO

**Aya 101-102**

### MAANA

Enyi Mlioamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatawachukiza.

Kauli yake Mwenyezi Mungu 'Msiulize' inaishiria kuwa baadhi ya Masahaba walikuwa waking'ang'ania kuuliza mambo yasiyokuwa na dharura yoyote kuyajua na huenda jibu lake likawaudhi waulizaji. Kuna riwaya isemayo kuwa mtu mmoja alimuuliza Mtume **(s.a.w.w)**: "Ni nani baba yangu?" Mtume akamwambia, "baba yako ni Fulani" Mwingine akauliza "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Baba yangu yuko wapi? Mtume akajibu: "Yuko motoni," ndipo ikashuka Aya hiyo.

Riwaya nyingine inasema kuwa Mtume alisema: "Mwenyezi Mungu amewafaradhishia kuhiji, basi hijini." Wakauliza: "Kila mwaka ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Mtume akanyamaza. Wakarudia kuuliza, akasema La; lau ningelisema naam, ingelikuwa wajib." Ndipo ikashuku Aya hii. Riwaya hii ndiyo yenye nguvu kuliko ile ya kwanza.

Na mnapoyauliza inapoteremshwa Qur'an mtabainishiwa.

Yaani msijikalifishe kuuliza mambo ila baada ya kuteremshwa Qur'an. Mtakapoanza kuuliza Mtume **(s.a.w.w)** atawadhirishia mliyokuwa mkiyauliza.

Kwa hali hii, inatubainikia kuwa riwaya ya Hija ndiyo yenye nguvu katika sababu ya kushuka Aya, kuliko riwaya ya kuuliza mababa na wahenga wa Masahaba. Kwa sababu Qur'an inaanza kuleta itikadi na sharia na wala sio kuanzia kwa mababa na mababu wa Masahaba. Katika Hadith imeelezwa: **"Hakika Mwenyezi Mungu ameweka mipaka msiikiuke;**

**amewafaradhishia faradhi msizipoteze; ameharamishia vitu msivifanye; na ameacha vitu vingine si kwa kusahau, lakini ni kwa kuwahurumia, basi vikubalini wala msivifanyie utafiti".**

Mwenyezi Mungu amesamehe hayo

Yaani maswali yenu yaliyotangulia, kwa hiyo msiyarudie. Imesemekana kuwa maana yake ni amezuia kutaja vitu mlivyoviulizia, basi nanyi jizuieni wala msijikalifu kuviulizia. Tafsir zote mbili zina uwezekano hazikataliwi na dhahiri ya tamko.

Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira, Mpole.

Humsamehe mkosaji akikosea tena.

Waliyauliza watu waliokuwa kabla yenu kisha wakawa makafiri kwayo.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwakataza kuuliza mambo wasiyokuwa na haja nayo, anawapigia mfano wa watu waliokuwa kabla yao, waliuliza wakang'ang'ania kuuliza. Walipobainishiwa na Mwenyezi Mungu walichukia wakaasi na wakastahiki adhabu. Lau wangeliacha kuuliza ingelikuwa bora kwao.

Wafasiri wamerefusha maneno katika kubainisha makusudio ya watu waliouliza, kisha wakawa makafiri kwa sababu ya kuuliza, lakini Aya haikubainisha. Pamoja na hivyo, tunaweza kusema kuwa watu waliouliza wakawa makafiri kwa sababu ya kuuliza ni wana wa Israil, kwa sababu ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu akiwasimulia:

﴿فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَىٰ أَكْبَرَ مِن ذَٰلِكَ فَقَالُوا أَرِنَا اللَّـهَ جَهْرَةً ﴾

"Hakika walimtaka Musa makubwa kuliko hayo, Walisema: Tuonyeshe Mwenyezi Mungu waziwazi" (4:153)

﴿مَا جَعَلَ اللَّـهُ مِن بَحِيرَةٍ وَلَا سَائِبَةٍ وَلَا وَصِيلَةٍ وَلَا حَامٍ وَلَـٰكِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّـهِ الْكَذِبَ وَأَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ﴾

103. Mwenyezi Mungu hakujaalia Bahira wala Saiba wala Waswila wala Hami; Lakini waliokufuru wanamzulia Mwenyezi Mungu uwongo na wengi wao hawafahamu.

﴿وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنزَلَ اللَّـهُ وَإِلَى الرَّسُولِ قَالُوا حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا أَوَلَوْ كَانَ آبَاؤُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ﴾

104. Wakiambiwa njooni katika yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na kwa Mtume, husema: Yanatutosha yale tuliyowakuta nayo babu zetu. Je hata kama baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka?

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا عَلَيْكُمْ أَنفُسَكُمْ لَا يَضُرُّكُم مَّن ضَلَّ إِذَا اهْتَدَيْتُمْ إِلَى اللَّـهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

105. Enyi mlioamini! Jiangalie nafsi zenu. Hawawadhuru waliopotea ikiwa mmeongoka. Marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu. Atawaambia yale mliyokuwa mkiyatenda.

## HAKUNA BAHIRAWALA SAIBA

**Aya 103-105**

## MAANA

Mwenyezi Mungu hakujaalia Bahira wala Saiba wala Waswila wala Hami.

Bahira, ni ngamia aliyetobolewa masikio, watu wa wakati wa Jahilia walikuwa wakifanya hivyo, ikiwa ngamia atazaa mimba kumi ; na inasemekana ni mimba tano. Wanamwacha bila ya kutumiwa na mtu yoyote. Saiba ni ngamia waliyemwekea nadhiri kwa waungu, na wana mwacha akijilisha mwenyewe popote bila ya kufungwa wala kuwa na mchungaji sawa na Bahira.

Wasila ni mbuzi anayezaa mtoto wa kiume na wa kike pamoja. Desturi yao ilikuwa kama akizaa mume wanamfanya ni wa waungu na akizaa mke ni wao. Iwapo atazaa mume na mke pamoja, hawamchinji mume wakisema kuwa ameunganishwa na dada yake. Hami ni dume aliyezalisha mimba kumi, wanamwacha hazuiliwi na maji wala malisho, wakisema ameuhami mgongo wake.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anabainisha kwamba yote hayo hayamo katika dini, na kwamba dume, jike na mbuzi, vyovyote wanavyofanyiwa, wanabakia na uhalali wake kama walivyokuwa mwanzo na wala hawaharamishwi na porojo hizo.

Lakini waliokufuru wanamzulia Mwenyezi Mungu uwongo na wengi wao hawafahamu.

Watu wa kijahilia walikuwa wakikubali kuweko kwa muumba kwa dalili kwamba wao wamenasibishia uharamu wa Hami, Saiba, Bahira na Waswila, lakini pamoja na hayo Mwenyezi Mungu amewanasibishia ukafiri.

Kwa sababu wao wamemnasibishia uharamu kwa uwongo na uzushi. Kwa hiyo, basi kila anayemnasibishia Mwenyezi Mungu na yasiyokuwa na dalili ya Kitab wala Hadith ya Mtume wake basi huyo ni kafir kwa sharti ya kutegemea kumnasibishia Mungu, huku akijua kutokuwepo dalili.

Hii, kwa lugha ya watu wa sharia, huitwa Bid'a (uzushi). Kuna Hadithi isemayo: "Kila bid'a ni upotevu na kila upotevu ni motoni".

Ilivyo ni kuwa kufaradhia huko kuko mbali na hali halisi ilivyo, Ni nani anayemnasibishia hukumu Mwenyezi Mungu huku akijua kuwa hakuna dalili. Pengine anaweza akadhani ni dalili, lakini kumbe sio dalili.

Wakiambiwa njooni katika yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na kwa Mtume, husema: "Yanatutosha yale tuliyowakuta nayo babu zetu. Je hata kama babu zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka?

Razi anasema: "Maana yanajulikana, nayo ni jibu la kuwapinga watu wa Taqlid (kufuata)". Tumezungumzia kuhusu Taqlid katika Juz.2 (2:170)

Enyi mlioamini! Jiangalieni nafsi zenu, Hawawadhuru waliopotea ikiwa mmeongoka, Marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu.

Razi ametaja njia nane za kufasiri Aya hii. Mmoja wa wafasiri wapya ameandika kurasa 33. Lililowafanya wawili hawa na wengineo kurefusha mambo hivi ni kuwa kuamrisha mema ni wajibu na dhahiri ya Aya inafahamisha kutokuwa wajib na kwamba ni juu ya mtu kujishughulikia mwenyewe. Ama wengine wana majukumu yao juu ya nafsi zao wala si wajibu kwa yoyote kuiongoza au kuikanya nafsi ya mwingine.

Ilivyo tafsir ya Aya hii ni kwamba, ni juu ya mtu kuamrisha mema. Kuamrisha kwake kukinufaisha basi hayo ndiyo yanayotakikana.

Vinginevyo basi atakuwa ametekeleza lile aliloamrishwa wala hautamdhuru upotevu wa aliyepotea.

Mwenye jukumu baada ya kuamrisha ni yule aliyepotea na wala sio mwamrishaji. Tafsir hii imetilia mkazo wajibu wa kuamrisha mema na sio kupinga.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا شَهَادَةُ بَيْنِكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ حِينَ الْ وَصِيَّةِ اثْنَانِ ذَوَا عَدْلٍ
مِّنكُمْ أَوْ آخَرَانِ مِنْ غَيْرِكُمْ إِنْ أَنتُمْ ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَأَصَابَتْكُم مُّصِيبَةُ الْمَوْتِ تَحْبِسُونَهُمَا مِن
بَعْدِ الصَّلَاةِ فَيُقْسِمَانِ بِاللَّـهِ إِنِ ارْتَبْتُمْ لَا نَشْتَرِي بِهِ ثَمَنًا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ وَلَا نَكْتُمُ شَهَادَةَ اللَّـهِ
إِنَّا إِذًا لَّمِنَ الْآثِمِينَ﴾

106. Enyi mlioamini! yanapo mfikia mauti mmoja wenu, wakati wa kuusia ushahidi kati yenu ni wa waadilifu wawili miongoni mwenu. Au Wengine wawili wasio kuwa katika nyinyi mnapokuwa safarini na msiba wa mauti ukawafikia. Mtawazuia wawili hao baada ya swala, na waape kwa Mwenyezi Mungu mkiwa na shaka: "Hatupokei thamani yoyote kwa haya hata kama ni jamaa wala hatufichi ushahidi wa Mwenyezi Mungu, hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi."

﴿فَإِنْ عُثِرَ عَلَىٰ أَنَّهُمَا اسْتَحَقَّا إِثْمًا فَآخَرَانِ يَقُومَانِ مَقَامَهُمَا مِنَ الَّذِينَ اسْتَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْأَوْلَيَانِ
فَيُقْسِمَانِ بِاللَّـهِ لَشَهَادَتُنَا أَحَقُّ مِن شَهَادَتِهِمَا وَمَا اعْتَدَيْنَا إِنَّا إِذًا لَّمِنَ الظَّالِمِينَ﴾

107. Ikigundulika kuwa wawili hao wamestahiki dhambi, basi wengine wawili watasimama mahali pao katika wale ambao wamestahiki (kudai). Washike nafasi ya wa mwanzo waape kwa Mwenyezi Mungu: "Ushahidi wetu ni haki zaidi kuliko wa wale; na sisi hatukupita kiasi; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa madhalimu.

﴿ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَن يَأْتُوا بِالشَّهَادَةِ عَلَىٰ وَجْهِهَا أَوْ يَخَافُوا أَن تُرَدَّ أَيْمَانٌ بَعْدَ أَيْمَانِهِمْ وَاتَّقُوا اللَّـهَ
وَاسْمَعُوا وَاللَّـهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ﴾

108. Hiyo inaelekea zaidi ya kwamba watatoa ushahidi ulio sawa au wataogopa visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao. Na mcheni Mwenyezi Mungu na msikie, Na hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi mafasiki.

## KUTHIBITISHAWASIA

**Aya 106-108**

### MAANA

Aya hizi tatu ni katika Aya za hukumu, na zinaingia katika mlango wa wasia na ushahidi. Ndani yake mna hukumu zifuatazo:

1. Enyi mlioamini! yanapomfikia mauti mmoja wenu, wakati wa kuusia ushahidi kati yenu ni wa waadilifu wawili miongoni mwenu.

Mwenyezi Mungu anakusudia kuwa atakayehisi kuwa ajali yake imekurubia na akataka kuusia anayoyataka, awalete waadilifu wawili katika Waislamu na awashuhudishe juu ya wasia wake.

Ilivyo ni kuwa wasia ni sunna na wala si wajibu ila kwa ambaye ana haki za watu au za Mwenyezi Mungu na zikamdhihirikia dalili za mauti na akahofia kupotea baada yake.

2. Au Wengine wawili wasiokuwa katika nyinyi mnapokuwa safarini na msiba wa mauti ukawafikia. Mtawazuia wawili hao baada ya Swala, na waape kwa Mwenyezi Mungu mkiwa na shaka: Hatupokei thamani yoyote kwa haya hata kama ni jamaa wala hatufichi ushahidi wa Mwenyezi Mungu, hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi.

Shia na Hambal wamesema kuwa Mwislamu akiusia safarini na asipate Mwislamu, basi anaweza kuwashuhudiza watu wawili katika Ahlul-Kitab (watu wa kitab) kuwa waape baada ya Swala mbele ya watu kuwa wao hawakuhini watu kuficha wala hawakupokea chochote kwa ushahidi au kiapo. Hapo ushahidi wao utakubaliwa kama utakavyokubaliwa wa Waislamu wote, Na itapasa juu ya hao mashahidi kuapa ikiwa kuna shaka katika ukweli wao. Ama mwaminifu hana kiapo, kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu: "Mkiwa na shaka."

Hivi ndivyo walivyofutu Shia Imamiya na Hanbal kwa kutegemea Aya hii. Ama Abu Hanifu, Malik na Shafi, wamesema kuwa haukubaliwi ushahidi wa asiyekuwa Mwislamu kwa hali yoyote ile, na wameifanyia taawili Aya kwa maana nyingine. Ameongezea Malik na Shafi kuwa haukubaliwi ushahidi wa asiyekuwa Mwislamu kwa hali yoyote hata kama ni kwa wao kwa wao, Hayo yamo katika Kitab Al-Mughni.

3. Ikigundulika kuwa wawili hao wamestahiki dhambi, basi wengine wawili watasimama mahali pao katika wale ambao wamestahiki (kudai). Washike nafasi ya wa mwanzo waape kwa Mwenyezi Mungu: Ushahidi wetu ni haki zaidi kuliko wa wale; na sisi hatukupita kiasi; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa madhalimu."

Imeelezwa katika sahih za Shia na Sunni kwamba: Aya hii ilishuka kwa sababu ya watu watatu waliosafiri kibiashara, mmoja wao akiwa Mwislamu na wawili Wakristo. Njiani yule Mwislamu akaugua na akahisi kuwa ajali yake imekurubia, akaandika wasia wake, akitaja vitu vyote alivyo navyo na akauficha katika baadhi ya mizigo yake bila ya kuwafahamisha wale wenzake; kisha akawausia kuwa mizigo yake waifikishe kwa watu wake.

Alipokufa, wale wawili walichukua kitu kutoka katika bidhaa zile za maiti na wakapeleka zilizobaki kwa watu wake. Walipogundua watu wa marehemu wasia wake, waliona kuwa kuna kitu fulani kilichotajwa hakimo. Hivyo wakawauliza wale wawili, wakakanusha na wakasema wakiapa: "Alichotupa ndicho tulichowapa".

Watu wa marehemu wakakiona kile kitu kwa mtu mwengine. Walipomuuliza umekipata wapi, akajibu kutoka kwa fulani na fulani (wale watuhumiwa wawili). Kesi ikapelekwa kwa Mtume **(s.a.w.w.)**. Inasemekana kuwa wale wawili walipoonyeshwa, walisema tulikinunua kwake (yule marehemu), Ndipo ikashuka Aya hii.

Maana yake yakiwa kama alama za kuleta shaka zikidhihiri kwa watuhumiwa basi wajibu wakati huo ni kusimama watu wawili katika warithi wa marehemu na waape kwa Mwenyezi Mungu kwamba wao ni wa kweli kuliko watuhumiwa na waseme katika kiapo chao: "Sisi hatukupita kiasi; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa madhalimu" Baada ya kiapo watahukumiwa watuhumiwa.

**Unaweza kuuliza**: Maneno ya wafasiri yamekuwa marefu na kugongana kuhusu kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Katika wale ambao wamestahiki."

Mpaka ikanukuliwa kutoka kwa mmoja wa wakale akisema: "Hii ndiyo jumla yenye mushkeli zaidi kwa muundo katika kitab cha Mwenyezi Mungu."Sasa je tafsir sahihi ni ipi?

**Jibu**: Lililowatia wafasiri kwenye shaka ni kuwa dhamir ya wanaostahiki inawarudia nani? Tujuwavyo sisi ni kuwa inawarudia warithi wa marehemu kwa sababu madeni na mambo mengine, yaliyokuwa yakimstahiki marehemu yanawastahiki warithi baada ya kufa kwake.

Kwa hiyo maana yatakuwa: Wataapa wawili katika wale ambao ni wajibu juu yao yale yaliyo wajibu kwa wanayemrithi. Mfumo wa Aya unalitilia mkazo hili.

Kwa sababu wengine wawili watakaosimama mahali pa watuhumiwa katika kuapa, hapana budi wawe ni katika warithi wa marehemu kwa maafikiano ya wafasiri, na haiwezekani kwa hali yoyote kuwa ni wengineo. Kwa hiyo inakuwa dhamiri ya wanaostahiki inawarudia wao hasa.

Hiyo inaelekea zaidi ya kwamba watatoa ushahidi ulio sawa au wataogopa visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao.

Hiyo ni ishara ya hukumu iliyotangulia na kuelekea zaidi ni ubainifu wa sababu ya hukumu. Yaani makusudio ya sharia tuliyoiweka ni kutogeuza mashahidi ushahidi wao wakaapa uwongo au kujizuia kuapa kwa kuhofiwa kupingwa viapo vyao na viapo vya warithi.

**Unaweza kuuliza kuwa**: Mwenyezi Mungu (s.w.t) alipobainisha hukumu aliweka wawili wawili, akasema: Ushahidi wao wawili, watasimama wawili. Lakini aliposihiria sababu ya hukumu amebainisha kwa wengi akasema: Ya kwamba watatoa ushahidi. Je kuna wajihi gani?

**Jibu**: mashahidi ni wane: wawili wanashuhudia mwanzo, na wawili watasimama mahali pao ikiwa litadhihiri kosa kwa ushahidi wa kwanza. Zaidi ya haya ni kwamba sababu katika hukumu ni kuenea kwenye maudhui yaliyo tajwa na mengineyo.

﴿يَوْمَ يَجْمَعُ اللَّـهُ الرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَا أُجِبْتُمْ قَالُوا لَا عِلْمَ لَنَا إِنَّكَ أَنتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ﴾

109. Siku ambayo Mwenyezi Mungu atawakusanya Mitume awaambie mlijibiwa nini? Watasema: Hatujui, hakika wewe ndiwe mjuzi sana wa ghaibu.

﴿إِذْ قَالَ اللَّـهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ اذْكُرْ نِعْمَتِي عَلَيْكَ وَعَلَىٰ وَالِدَتِكَ إِذْ أَيَّدتُّكَ بِرُوحِ الْقُ دُسِ تُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا وَإِذْ عَلَّمْتُكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرَاةَ وَالْإِنجِيلَ وَإِ ذْ تَخْلُقُ مِنَ الطِّينِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ بِإِذْنِي فَتَنفُخُ فِيهَا فَتَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِي وَتُبْرِئُ الْأَ كْمَهَ وَالْأَبْرَصَ بِإِذْنِي وَإِذْ تُخْرِجُ الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِي وَإِذْ كَفَفْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَنكَ إِذْ جِئْتَهُم بِالْبَيِّ نَاتِ فَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ إِنْ هَـٰذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ﴾

110. Atakaposema Mwenyezi Mungu: Ewe Isa mwana wa Maryam! Kumbuka neema yangu juu yako na juu ya mama yako. Nilipokutia nguvu kwa roho mtakatifu, ukazungumza na watu utotoni na katika utu uzima. Na nilivyokufundisha kitab na hekima na Tawrat na Injil. Na ulipotengeneza kwa udongo kama umbo la ndege kwa idhini yangu, kisha ukapuliza likawa

ndege kwa idhini yangu, na ulipowaponyesha vipofu na wenye mbalaga kwa idhini yangu na ulipowatoa wafu kwa idhini yangu, na nilipokukinga na wana wa Israil ulipowafikia na hoja zilizowazi; wakasema wale waliokufuru miongoni mwao. Haya si chochote ila ni uchawi tu.

﴿وَإِذْ أَوْحَيْتُ إِلَى الْحَوَارِيِّينَ أَنْ آمِنُوا بِي وَبِرَسُولِي قَالُوا آمَنَّا وَاشْهَدْ بِأَنَّنَا مُسْلِمُونَ﴾

111. Na nilipowafahamisha wanafunzi kwamba Niaminini mimi na Mtume wangu, wakasema Tumeamini na ushuhudie kuwa sisi ni wanyenyekevu.

## MITUME NA SIKU YA KUKUSANYWA

**Aya ya 109-111**

### MAANA

Siku ambayo Mwenyezi Mungu atawakusanya Mitume awaambie mlijibiwa nini?.

Razi anasema: "Desturi ya Mwenyezi Mungu inayopita katika Kitab chake kitukufu ni kwamba yeye akitaja aina yoyote ya hukumu, huifuatishia ama kwa mambo ya Mwenyezi Mungu, au kufafanua hali za Mitume au hali ya Kiyama, ili kutilia mkazo yaliyotangulia. Na alipotaja hapo hukumu miongoni mwa hukumu za sharia, amefuatisha kwanza kutaja hali za Kiyama kisha hali ya Isa"

Hadhara aliyoyataja Mwenyezi Mungu (s.w.t) hapa ni hadhara ya kutisha, atakayofufulia viumbe kwa ajili ya hisabu na hukumu, kabla ya kutoka hukumu ya msamaha.

Mwenyezi Mungu Mtukufu atawakusanya Mitume wake aliowatawanya katika nchi zake majimbo yake na mabara yake. Ilivyo ni kwamba majimbo yake na mabara yake Mwenyezi Mungu Mtukufu sio kama haya majimbo yetu na mabara yetu. Ni umma jinsi na kaumu.

Kisha atauliza kila umma na kila watu kupitia Mtume wao: "Wamekwambia nini hawa?" Anakusudia kwa swali hili kutoa hoja kwa waja wake, na kuwaandaa kwa hukumu yake. Mitume watajibu mbele ya hadhara hii: Hatujui, hakika wewe ndiwe mjuzi wa ghaibu, Na ajuaye ghaibu haifichiki juu yake dhahiri.

**Unaweza kuuliza kuwa**: Mitume wanawajua waliowapinga na kuwapiga vita katika uhai wao; sasa je, kuna wajihi gani wa kusema kwao hatujui?

**Jibu**: Makusudio ya kusema kwao huku sio kukanusha kujua kabisa, bali makusudio ni kwamba elimu yao si chochote kwa upande wa elimu yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu wao wanajua yale yaliyodhihirishwa na umma wao naye anayajua waliyoya dhihirisha na kuyaficha.

Atakaposema Mwenyezi Mungu: "Ewe Isa mwana wa Maryam! Kumbuka neema yangu juu yako na juu ya mama yako.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwauliza Mitume wake kwa neno fupi (Mlijibiwa nini), amemhusisha Isa (a.s) miongoni mwao kwa maneno marefu akitaja neema yake juu yake na juu ya mama yake.

Nilipokutia nguvu kwa roho mtakatifu (ambaye ni Jibril) ukazungumza na watu utotoni ili kumwepusha mama yako na kila dhana na katika utu uzima yaani maneno ya utotoni yalikuwa kama maneno ya utu uzimani.

Na nilivyokufundisha kitabu

Inasemekana makusudio ya kitab ni kuandika kwa sababu neno Kitabu limechukuliwa kutoka katika neno Kitaba (kuandika) na hekima sharia na Tawrat na Injili.

Na ulipotengeneza kwa udongo kama umbo la ndege kwa idhini yangu kisha ukapuliza likawa ndege kwa idhini yangu, na ulipowaponyesha vipofu na wenye mbalanga kwa idhini yangu na ulipowatoa wafu kwa idhini yangu.

Umepita mfano wa tafsiri yake katika Juz.3 (3:49) Mwenyezi Mugu amelikariri neno kwa idhini yangu mara nne kwa kutilia mkazo, kwamba kuumba, kufufua na kuponyesha kunatokana na uwezo wa Mwenyezi Mungu, na hakutokani na yeye Isa. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amedhihirisha vitendo hivi mikononi mwa Isa ili iwe ni dalili ya ukweli wake na utume wake.

## ISA NA UTUME WA UTOTO

Inaweza ikadhaniwa au kugeuzwa kwamba Isa ni ni mtume mtoto mdogo kwa sababu yeye alizungumza utotoni, huu ni ujinga au kutia sifa. Kwa sababu yeye alisema utotoni kwa ajli ya kumuondolea tuhuma mama yake tu, kutokana na kauli ya wakosaji, si kwa kuwa ni mtume. Ikiwa Mwenyezi Mungu amewaondolea taklifu watoto wadogo je anaweza kuwakalifu na mambo mazito; kama alivyoyataja katika kauli yake:

﴿إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا﴾

"Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito" (73:5)

Na ni nani atakayemsikia na kumtii na yeye yuko susuni? Je inaweza kuwa hoja ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake kwa mtoto anayenyonya? Ni mafunzo gani atakayoyafikisha kwa watu akiwa ananyonya matiti ya mama yake?

Injili zinazotiliwa maanani na wakristo zinaeleza kuwa Isa alitumwa akiwa katika rika la miaka thelathini (30). Imeelezwa katika Injili, Luka, ninanukuu: "Na Yesu mwenyewe, alipoanza kufundisha, alikua amepata umri wake kama miaka thelathini." Luka 3:23.

La kushangaza zaidi ni kuwa Injili za wakristo zinasema kuwa mwito wa Isa ulianza akiwa na miaka thelathini, kisha mwingine mtia chumvi anasema kuwa Isa ni mtume mtoto, kinyume na Muhammad aliyetumwa akiwa na miaka arubaini[1], akitoa dalili ya uzushi wake huu kwamba Isa alizungumza akiwa utotoni kwa ushahidi wa Qur'an, na kujitia kutojua kuwa Isa alizungumza utotoni ili kumtakasa mama yake, mkweli mtakatifu na wala sio kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa waja wake akiwa ananyonya.

Na nilipokukinga na wana wa Israili ulipowajia na hoja zilizo wazi; wakasema wale waliokufuru miongoni mwao: Haya si chochote ila ni uchawi tu.

Yamekuja maelezo katika Nahjul-balagha: "Isa alikuwa akifanya mto wa kulalia ni jiwe , akivaa magwanda, akila chakula kisicho na ladha, taa yake

1 Mtia chumvi huyu alitaka kumboresha Isa kuliko Muhammad kwa siri, lakini waliomshuhudia Muhammad wanajua ni nani. Angalia tafsiri ya Aya 113 Sura hii.

usiku ilikuwa ni mwezi, kimbilio lake wakati wa kusi ni Mashariki na Magharibi (hakuwa na kimbilio), matunda na manukato yake ni mimea inayoliwa na wanyama, hakuwa na mke wa kumtia msukosuko wala mtoto wa kumhuzunisha wala mali ya kumsumbua wala tamaa ya kumdhalilisha, kipando chake (usafiri) ni miguu yake na mtumishi wake ni mikono yake" Pamoja na hayo yote hakusalimika na mayahudi. Walijaribu kumuua wakamwita muongo na mchawi, mama yake wakamwita malaya, si kwa lolote ila ni kwa kuwa ametamka haki akiwalingania kwenye hiyo haki na kuwaamrisha. Haya hayahusiki na mayahudi tu kwani watu wengi humfanyia uadui anayewaongoza kwenye haki.

Na nilipowapa wahyi wanafunzi kwamba, niaminini mimi na mtume wangu, wakasema: "Tumeamini na ushuhudie kuwa sisi ni Waislamu." Neno wahyi linatumika kwa maana nyingi, ikiwemo ilham (ufahamisho): kama katika kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿وَأَوْحَىٰ رَبُّكَ إِلَى النَّحْلِ أَنِ اتَّخِذِي مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا﴾

"Na Mola wako akampa whyi Nyuki kwamba jitengenezee nyumba katika mlima" (16:68)

﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ أُمِّ مُوسَىٰ أَنْ أَرْضِعِيهِ فَإِذَا خِفْتِ عَلَيْهِ فَأَلْقِيهِ فِي الْيَمِّ﴾

"Na tulimpompa wahyi mama yake Musa ya kwamba mnyonyeshe na utakapomhofia basi mtie mtoni.." (28:7)

Maana ya wahyi kwenye Aya zote hizo ni ufahamisho na ndiyo maana yaliyotumika hapa.

**Unaweza kuuliza**: kwa nini Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemkumbusha Isa neema kinyume na mitume wengine pamoja na kwamba fadhila zake na neema zake hazina idadi.

**Jibu**: Mwenyezi Mungu amejumlisha msemo pamoja na Mitume na akafafanua pamoja na Isa kwa sababu wafuasi wake walizama sana kwa Isa. Ama wafuasi wengine hawakuwahi kudai uungu kwa mitume wao, ndipo ukaja ufafanuzi kwa kuweka hoja.

﴿إِذْ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيعُ رَبُّكَ أَن يُنَزِّلَ عَلَيْ نَا مَائِدَةً مِّنَ السَّمَاءِ قَالَ اتَّقُوا اللَّـهَ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ﴾

112. Waliposema Wanafunzi: "Ewe Isa bin Mariyam, Je Mola wako anaweza kuteremshia chakula kutoka mbinguni; akasema: Mcheni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni waumini.

﴿قَالُوا نُرِيدُ أَن نَّأْكُلَ مِنْهَا وَتَطْمَئِنَّ قُلُوبُنَا وَنَعْلَمَ أَن قَدْ صَدَقْتَنَا وَنَكُو نَ عَلَيْهَا مِنَ الشَّاهِدِينَ﴾

113. Wakasema: Tunataka kula katika hicho na ili zitulie nyoyo zetu na tujue ya kuwa umetuambia kweli na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia.

﴿قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّـهُمَّ رَبَّنَا أَنزِلْ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِّنَ السَّمَاءِ تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِّأَوَّ لِنَا وَآخِرِنَا وَآيَةً مِّنكَ وَارْزُقْنَا وَأَنتَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ﴾

114. Akasema Isa bin Maryam: Ewe Mwenyezi Mungu Mola wetu! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe sikukuu kwa ajili ya wa

mwanzo wetu na wa mwisho wetu na kiwe ishara itokayo kwako na uturuzuku kwani wewe ni mbora wa wanaoruzuku."

﴿قَالَ اللَّـهُ إِنِّي مُنَزِّلُهَا عَلَيْكُمْ فَمَن يَكْفُرْ بَعْدُ مِنكُمْ فَإِنِّي أُعَذِّبُهُ عَذَابًا لَّا أُعَذِّبُهُ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ﴾

115. Mwenyezi Mungu akasema: Hakika mimi nitakuteremshia lakini atakayekufuru baada ya hapo basi nitamwadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu yeyote katika walimwengu.

## CHAKULA KUTOKA MBINGUNI

**Aya 112-115**

### MAANA

Maneno yamekuwa mengi kuhusu chakula na waliokitaka kuwa je, walikuwa waumini au watiaji shaka? Na kwamba je, kilishuka chakula au hakikushuka kwa sababu wanafunzi waligeuza maombi yao baada ya kutishiwa na Mwenyezi Mungu aliposema: "Lakini atakayekufuru baada ya hapo basi nitamwadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu yeyote katika ulimwengu."

Kama tukikadiria kuwa kilikuja je kilikuwa ni cha aina gani na rangi gani? Kisha je, waligeuzwa manyani au nguruwe baadaye kwa sababu waliiba? Sisi tutaelekea kwenye mazungumzo yetu na tunayofahamishwa na matamko ya Aya na yanayoambatana nayo.

Waliposema Wanafunzi: Ewe Isa bin Mariyam, Je Mola wako anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni; akasema Mcheni Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi ni waumini.

Aya hii inaashiria kuwa wanafunzi hawakuwa wakimwamini Isa walipomtaka chakula kwa sababu wao hawahitajii chakula ndipo waamini, linalotilia nguvu hilo ni kusema kwao: Je anaweza Mola wako." Huku ni kutambulisha kutia shaka katika uweza wa Mwenyezi Mungu, Hata hivyo Aya iliyotangulia imeshuhudia kuamini kwao. "wakasema tumeamimi" Zaidi ya hayo neno wanafunzi lenyewe linafahamisha kumwamini Isa na sasa je kuna wajihi gani wa kuchanganya Aya mbili hizi?

Wafasiri wengi wamejibu kuwa swali lao hili halipingi imani yao. Kwa sababu makusudio yake ni kuamini kwa njia za hisia na macho, baada ya kuamini kwa njia ya akili na dalili. Kwa maneno mengine ni kuitia nguvu imani na kuithibitisha; sawa na alivyosema Ibrahim (a.s):

"Lakini upate kutulia moyo wangu" Juz.3 (2:260)

Na wanafunzi wamelifafanua kusudio lao hili kwa kusema kwao katika Aya inayofuatia:

Na ili zitulie nyoyo zetu ikiwa ni jibu la walivyoambiwa na Isa "mcheni Mola wenu ikiwa nyinyi ni waumini." Ama kusema kwao, "Je aweza Mola wako" maana yake je,atakubali Mola wako tukimuuliza kututeremshia chakula kutoka mbinguni?

Wakasema: Tunataka kula katika hicho na ili zitulie nyoyo zetu na tujue ya kuwa umetuambia kweli na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia.

Wanataka wale ili waamini na wajue au wanataka wale ili waitie nguvu imani katika nyoyo zao na elimu katika akili zao; kama tulivyotangulia

kueleza, kisha wampe habari asiyehudhuria chakula katika watu wao aamini mpinzani na utulie moyo wa muumini hata kama hatakula.

### WANAFUNZI WA MUHAMMAD (S.A.W.W) NAWA ISA (AS)

Mtume Muhammad naye alikuwa na wanafunzi kama alivyokuwa nao Isa (a.s) na Mtume wowote katika Mitume. Lakini wanafunzi wa Muhammad hawakumwomba kuwashibisha kutokana na njaa kwa kutumia miujiza yake, kama walivyofanya wanafunzi wa Isa ambao walisema"Tunataka kula katika hicho", wala hawakutaka awasalimishe na hofu , kama walivyofanya sahaba wa Musa (a.s) bali walimwambia katika baadhi ya vita kupitia mdomoni mwa Mikidadi bin Al-Aswadi "Endelea ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa lile alilokutakia Mwenyezi Mungu na sisi tuko pamoja nawe wala hatutakwambia yale waliyosema wana wa Israil kwa Musa: Nenda wewe na Mola wako mpigane na sisi tuko hapa tumekaa. Lakini sisi tunakwambia: Nenda wewe na Mola wako mkapigane na sisi tuko pamoja nanyi.

Walikuwa wakifa mashahidi mbele yake na huku wakisema: "Tumefuzu, naapa kwa Mola wa Al-Kaaba." Masimulizi ya historia yao utafikiri ni vigano tu. Ammara bin Yazid alipigana siku ya Uhud mpaka majeraha yakamzidia. Alipoona sasa anakufa alijitupa miguuni mwa Mtume **(s.a.w.w)**, hakuinua kichwa chake hapo mpaka alipomaliza uhai wake kwa muishilio huu mwema.

Alipoanguka Sa'ad bin Rabi, siku ya Uhud, alimwambia mmoja wa wenzake: "Mwambie Mtume wa Mwenyezi Mungu, Saad Bin Rabi anasema umetupa kitu bora cha Mtume alichowapa umma wake na wafikishie salam zangu watu wako uwaambie mwana wa Rabi anawaambia hamtakuwa na udhuru wowote kwa Mwenyezi Mungu kama mkimwacha Mtume wetu hata kidogo."

Amra bin Jumuh alikuwa mlemavu na akataka kutoka pamoja na Mtume kwenda vita vya Uhud. Watoto wake walipojaribu kumzuia akaondoka kumshtakia Mtume **(s.a.w.w)**: "Mimi nataraji kuchechemea usiku kwenda peponi" Mtume **(s.a.w.w)** akamruhusu. Akauliwa yeye, watoto wake wane na shemeji yake. Baada ya vita mjane wake akaja, akachukua maiti ya mumewe, nduguye na wanawe wane kwenye ngamia na kwenda nao Madina.

Wanawake wakamkabili kumuuliza habari, akasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko salama, ama msiba mwingine zaidi ya Mtume ni mwepesi." Wakamuuliza: "Na hizi maiti ni za nani?" Akawajibu: "Wanangu, mume wangu na ndugu yangu. Mwenyezi Mungu amewakirimu kwa kufa mashahidi ninawachukua nikawazike"

Mifano hii tumeileta kutofautisha baina ya sahaba wa Muhammad na wa mitume wengineo. Wala hatutakuwa tumeongeza chumvi, kama tukisema kuwa hakuna mtume yeyote aliyekuwa na masahaba kama Mtume Muhammad **(s.a.w.w)**. Ama siri ya hilo inakuwa katika utu wake utukufu wake na risala yake.

Akasema Isa bin Maryam: Ewe Mwenyezi Mungu Mola wetu! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe ishara itokayo kwako na uturuzuku kwani wewe ni mbora wa wanaoruzuku.

Alipoona kuwa wao wanang'ang'ania, aliomba kwa unyenyekevu: Ewe Mola wetu! Kuondoa shub-ha na kumkadhibisha kila atakayedai kuwa Isa ana uwezo katika hilo. Makusudio ya ishara ni mujiza. Na sikukuu ni furaha.

Mwenyewzi Mungu akasema: Hakika mimi nitakuteremshia lakini atakayekufuru baada ya hapo basi nitamwadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu yeyote katika walimwengu.

Mwenyezi Mungu aliitikia maombi ya Isa ili sahaba zake wazidi kumwamini na kuamini utume wake na awe na hoja nao, kama watahalifu na watastahiki adhabu kali ambayo hajamwadhibu yeyote katika waliokanusha na waliokufuru. Kwa sababu wao ndio waliotoa maombi ya chakula na kukitaka; na mwenye kuitikiwa maombi yake amesimamiwa na hoja na hana udhuru wowote wakuhalifu.

5

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿وَإِذْ قَالَ اللَّـهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَـٰهَيْنِ مِن دُونِ اللَّـهِ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقٍّ إِن كُنتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ ﴾

116. Na pale Mwenyezi Mungu atakaposema: Ewe Issa bin Maryam! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Atasema: Wewe umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu, Ikiwa niliyasema basi bila shaka umekwisha yajua. Wewe unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, wala mimi siyajui yaliyo katika nafsi yako. Hakika wewe ndiye mjuzi zaidi wa yaliyofichikana.

﴿مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِهِ أَنِ اعْبُدُوا اللَّـهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ وَكُنتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَّا دُمْتُ فِيهِمْ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنتَ أَنتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ وَأَنتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴾

117. Sikuwaambia ila uliyoniamrisha, ya kwamba, Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao na uliponifisha ukawa wewe ndiye mwangalizi juu yao. Na wewe ni shahidi juu a kila kitu.

﴿إِن تُعَذِّبْهُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ وَإِن تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴾

118. Ukiwaadhibu basi hao ni waja wako, Na ukiwasamehe basi wewe ndiye mwenye nguvu mwenye hekima.

## ISSA NA WATU

**Aya 116-118**

### LUGHA

Neno nafsi linatumika kwa maana nyingi, mingoni mwazo ni:

• Uhai wa binadamu na wanyama. Maana haya ndiyo aliyoyakusudia Mwenyezi Mungu aliposema: "Kila nafsi itaonja mauti"

• Dhati ya kitu, mfano: ndicho nafsi yake.

• Ghaibu, mfano: Siijui nafsi ya fulani, yaani ghaibu yake. Haya ndiyo maana yaliyokusudiwa katika: Unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu na wala siyajui yaliyo katika nafsi yako.

### MAANA

Na pale Mwenyezi Mungu atakaposema: Ewe Isa bin Maryam! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu hamkusudii Isa hasa kwa swali hili, kwa sababu yeye anajua kuwa Issa hakuwaambia watu hivyo. Isipokuwa anakusudia kuweka hoja kwa yule anayedai madai haya ya kikafiri kwa Isa na mama yake.

Atasema: Wewe umetakasika! Na ushirika. Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu.

Kwa sababu yeye ni Mtume na Mtume ni maasum, mwenye kuhifadhiwa na makosa, na yeye ametumwa kupiga vita ushirikina na kuleta mwito wa Tawhid (umoja wa Mungu), vipi tena yeye mwenyewe adai uungu na awatake watu wamwabudu?

Ikiwa niliyasema basi bila shaka umekwishayajua.Wewe unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu wala mimi siyajui yaliyo katika nafsi yako. Hakika wewe ndiye mjuzi zaidi wa yaliyofichikana.

Anatoa ushuhuda wa usafi wake wa shirki yao kutokana na ilimu ya Mwenyezi Mungu. Huo ni ushahidi tosha.

Sikuwaambia ila uliyoniamrisha, ya kwamba, Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao na uliponifisha ukawa wewe ndiye mwangalizi juu yao.

Imelezwa katika matayo: "Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Iblisi, Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa." (Mathayo:4:1-2), "....Nenda zako shetani, kwa maana imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako, umuabudu yeye pekee" (Mathayo 4:10).

Je Mungu anafunga? Basi anamfungia nani? Je anakuwa na njaa na yeye ndiye mtoaji riziki? Vipi ajaribiwe na Iblis na hali yeye ni mjuzi wa ghaib? Vipi aweze kuchukuliwa kutoka mlima mmoja hadi mwingine na yeye ndiye aliyeiumba na kuumba ulimwengu wote.

Ukiwaadhibu basi hao ni waja wako, Na ukiwasamehe basi wewe ndiye mwenye nguvu mwenye hekima.

Baadhi ya malezo ya tafsir yanasema kuwa kauli ya Isa (a.s): "Ukiwaadhibu basi hao ni waja wako, ni kuwaaombea msamaha kwa adabu na matarajio, na neno: "Basi ni waja wako" Inadhamini hilo. lakni baadhi wamekataa isipokuwa huchukulia kusamehewa kwa kutubia; yaani wakitubia uwasamehe.

Tunawajibu wenye kusema hivi kwamba msamaha pamoja na toba hauhitaji uombezi; kwa sababu mwenyewe Mwenyezi Mungu amejiwekea kumsamehe anayetubia. Kisha kuna kizuizi gani kwa Issa kuwaombea watu wake maghufira na rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu? Nabii Ibrahim alikwishawaombea watu wake kwa kusema:

﴿فَمَن تَبِعَنِي فَإِنَّهُ مِنِّي وَمَنْ عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

"Basi aliyenifuata huyo ni wangu mimi na aliyeniasi hakika wewe ni mwingi wa maghufira mwenye kurehemu" (14:36).

Zaidi ya hayo ni kwamba kumsamehe mkosaji ni jambo zuri kwa hali yoyote, "Je, wao wanaigawa rehema ya Mola wako?" (43:32)

﴿قَالَ اللَّـهُ هَـٰذَا يَوْمُ يَنفَعُ الصَّادِقِينَ صِدْقُهُمْ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا رَّضِيَ اللَّـهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ﴾

119. Mwenyezi Mungu atasema: Hii ndiyo siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata bustani zipitazo mito chini yake, Humo watadumu milele. Awe radhi nao Mwenyezi Mungu na wao wawe radhi naye, Huko ndiko kufuzu kukubwa.

﴿لِلَّـهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا فِيهِنَّ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

120. Mwenyezi Mungu ndiye mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo, naye ni Muweza wa kila kitu.

## UKWELI WAWAKWELI

**Aya 119-120**

### MAANA

Mwenyezi Mungu atasema: Hii ndiyo siku ambayo wasemao kweli utawafa ukweli. Wao watapata bustani zipitazo mito chini yake. humo watadumu milele.

Baada ya kumzungumzia Nabii Isa kwamba yeye aliwaambia watu wake mwabuduni Mwenyezi Mungu, Baada ya haya amefuatishia kuwasifu wakweli kwa ujumla na kwamba mwenye kuwa mkweli katika maisha haya atanufaika nao katika maisha ya pili na atalipwa pepo.

Mfuatilio huu ni ushahidi kutoka kwa mwenyezi Mungu juu ya ukweli wa Issa katika kauli yake na vitendo vyake; na kwamba yeye alitekeleza ujumbe wa Mola wake kwa ukamiifu. Basi mwenye kukufuru na kufanya ushirkina ni jukumu lake peke yake.

Awe radhi nao Mwenyezi Mungu na wao wawe radhi naye. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

Radhi ya Mwenyezi Mungu kwa mja wake ni pepo na neema. Na radhi ya mja kwa Mola wake ni kufurahia yale aliyompa Mwenyezi Mungu. Razi anasema: "Katika radhi ya Mwenyezi Mungu kuna siri za ajabu ambazo kalamu zinashindwa kuzielezea, amezijaalia Mwenyezi Mungu kwa watu wake" Na hawezi kuwa yeyote ni katika watu wake ila kwa kulipa thamani, na thamani yenyewe ni kuwa nembo ya mnunuzi iwe ni "lailaha illa llah" (Hakuna Mungu ispokuwa Allah) katika kila kitu; yaani kutoikasirikia katika jambo lolote hata kama atakerezwa na msumeno; kama alivyosema bwana wa viumbe: "Ikiwa wewe hukunikasirikia basi sijali" na kama alivyosema mjukuu wake, Husein Shahid: "Radhi ya Mwenyezi Mungu ndiyo radhi yetu sisi Ahlu bait, tunavumilia mitihani yake na atulipe malipo ya wanaovumilia"

Mwenyezi Mungu ndiye mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo, naye ni Muweza wa kila kitu.

Ambaye ana uweza huu na ufalme huu humpa anayemridhia bila ya hisabu. Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye Kurehemu

### MWISHO WA SURA YA TANO: AL - MAIDAH

Sura Ya Sita: Al-An'am
Imeteremshwa Makka isipokuwa baadhi ya Aya.
Ina Aya 165.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu

﴿الْحَمْدُ لِلَّـهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ ۖ ثُمَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ﴾

1. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi na akafanya giza na mwangaza. Tena wale waliokufuru wanamlinganisha Mola wao (na wengine).

﴿هُوَ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن طِينٍ ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا ۖ وَأَجَلٌ مُّسَمًّى عِندَهُ ۖ ثُمَّ أَنتُمْ تَمْتَرُونَ﴾

2. Yeye ndiye aliyewaumba kwa udongo. Kisha akapitisha muda; na muda maalum uko kwake, Tena nyinyi mnatia shaka.

﴿وَهُوَ اللَّـهُ فِي السَّمَاوَاتِ وَفِي الْأَرْضِ ۖ يَعْلَمُ سِرَّكُمْ وَجَهْرَكُمْ وَيَعْلَمُ مَا تَكْسِبُونَ﴾

3. Na yeye ndiye Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini; anaijua siri yenu na dhahiri yenu na anayajua mnayoyachuma.

## KUUMBA MBINGU NAARDHI

**Aya 1 - 3**

### MAANA

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi na akafanya giza na mwangaza.

Aya zote hizi tatu ni Aya za kilimwengu zinazofahamisha umoja wake na ukuu wake Mwenyezi Mungu.

Aya ya kwanza inaashiria kuumbwa mbingu na ardhi na giza na mwangaza.

Aya Ya pili, inaashiria kuumbwa mtu na kufufuliwa kwake baada ya kufa.

Na ya tatu, kuenea ujuzi wake kwa kila kitu.

Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu," anakusudia kufundisha; yaani semeni sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu (Alhamdulillah).

Kumsifu Mwenyezi Mungu ni kuzuri katika hali zote; hata wakati wa madhara. Kwa sababu yeye ndiye afaaye kutukuzwa na kuadhimisha. Ukipatwa na msiba na ukasema Alhamdulillah basi hapo unazingatiwa kuwa mvumilivu (mwenye subira) juu ya shida, na imani yako ni yenye nguvu iliyokita ambayo haiyumbishwi na chochote.

Uzuri wa Alhamdulillah unatiliwa mkazo wakati wa furaha na kuondolewa balaa. Kwa sababu ni kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa aliyoneemesha.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amejitaja kuwa ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi na giza na mwangaza ili azizindue akili kwamba Yeye hana mshirika katika uumbaji na Uungu. Kwa hiyo anakuwa Yeye peke yake ndiye mwenye kustahiki kusifiwa na kufanyiwa ikhlasi katika kuabudiwa.

Tena wale waliokufuru wanamlinganisha Mola wao (na wengine). Ajabu ya maajabu ni kwamba ulimwengu huu pamoja na ardhi yake na mbingu yake, na ubainifu huu ulio wazi na dalili mkato, bado hazikuliondoa giza zito kwenye akili ya mshirikina na kwenye moyo wake mpofu wa haki, na akaleta picha kuwa kuna mwingine mwenye kulingana sawa na Mwenyezi Mungu katika kustahiki kusifiwa na kuabudiwa.

Yeye ndiye aliyewaumba kwa udongo.

Yaani ameumba asili yenu, Adam kutokana na mchanga na maji. Au ameumba mada ya kila mtu kwa udongo, kwa sababu mtu anatokana na nyama na damu; na hivyo viwili vimetokana na mmea na nyama ya mnyama aliyetokana na mmea; na mmea nao umetokana na udongo.

Kisha akapitisha muda; na muda maalum uko kwake.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemwekea kila mtu muda (ajali) mara mbili: Wa kwanza, unaisha kwa kufa kwake, hapo hujulikana ameishi muda gani. Pili, ni kurudishwa na kufufuliwa kwake baada ya kufa. Ujuzi wa muda huu uko kwa Mwenyezi Mungu peke yake wala haujui yeyote katika viumbe vyake; kama lilivyofahamisha neno 'uko kwake'

Tena nyinyi mnatia shaka.

Yaani, baada ya kuweko dalili za uweza wa Mwenyezi Mungu katika kuumba kukubwa, ambako ni ulimwengu, na katika kuumba kudogo ambako ni kuumba mtu na kufa kwake na kufufuliwa kwake. Baada ya haya yote mnatia shaka katika kuweko Mwenyezi Mungu, umoja wake na utukufu wake!

Tafsir bora ya jumla hii ni kauli ya Amirul-muminin Ali (a.s): **"Namwonea ajabu anayemtilia shaka Mwenyezi Mungu naye anaona kuumba kwa Mwenyezi Mungu; ninamwonea ajabu anayesahau mauti naye anayaona mauti; na ninamstaajabia anayepinga kufufuliwa kwa mwisho naye anaona kufufuliwa kwa kwanza."**

Na yeye ndiye Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini; anaijua siri yenu na dhahiri yenu na anayajua mnayoyachuma.

Katika Aya ya kwanza Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja kwamba yeye ni Muumbaji wa mbingu na ardhi. Natija ya hayo ni kuwa yeye yuko mbinguni na ardhini; na maana ya kuweko humo ni kuweko athari zake. Katika Aya ya pili ametaja kuwa yeye ndiye Muumba wa binadamu, na atakayemfisha na atakayemfufua. Linalolazimiana na hilo ni kwamba Yeye ni Mjuzi wa anayoyaficha binadamu na anayoyadhihirisha na anayoyachuma katika imani na ukafiri, ikhlasi na unafiki na vilevile vitendo vinavyomrudia yeye vya kheri au shari.

﴿وَمَا تَأْتِيهِم مِّنْ آيَةٍ مِّنْ آيَاتِ رَبِّهِمْ إِلَّا كَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ﴾

4. Na haiwafikii ishara yoyote katika ishara za Mola wao ila wanaipinga.

﴿فَقَدْ كَذَّبُوا بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ فَسَوْفَ يَأْتِيهِمْ أَنبَاءُ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ﴾

5. Wameikadhibisha haki ilipowafikia; kwa hiyo zitawafikia habari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

﴿أَلَمْ يَرَوْا كَمْ أَهْلَكْنَا مِن قَبْلِهِم مِّن قَرْنٍ مَّكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ مَا لَمْ نُمَكِّن لَّكُمْ وَأَرْسَلْنَا
السَّمَاءَ عَلَيْهِم مِّدْرَارًا وَجَعَلْنَا الْأَنْهَارَ تَجْرِي مِن تَحْتِهِمْ فَأَهْلَكْنَاهُم بِذُنُوبِهِمْ وَأَنشَأْنَا مِن بَعْدِهِمْ
قَرْنًا آخَرِينَ﴾

6. Je hawaoni vizazi vingapi tulivyoviangamiza kabla yao? Tuliwamakinisha katika nchi tusivyowamakinisha nyinyi, Tukawapelekea mvua nyingi, Na tukaifanya mito inapita chini yao. Kisha tukawaangamiza kwa dhambi zao. Na tukaanzisha baada yao karne nyingine.

## KUKANA HOJA ZA MWENYEZI MUNGU

**Aya 4-6**

### LUGHA

Imeelezwa katika Tafsiri Razi: Wamesema baadhi: Karne ni miaka sitini. Wengine wakasema ni sabini. Wengine wakasema ni thamanini. Lililo karibu zaidi na ufahamu ni kwamba si yenye kukadiriwa kwa muda fulani kwa zaidi au kupungua, bali makusudio ni watu wa kila zama. Wakimaliza muda mwingi husemwa: Imekwisha karne. Dalili ya hilo ni kauli yake Mtume mtukufu **(s.a.w.w)**: **"karne bora ni karne yangu"**

Misingi ya itikadi ni mitatu, Tawhid, Utume na Ufufuo. Aya tatu zilizotangulia zimeelezea Tawhid na dalili zake, na Aya hii inaelezea Utume na hali ya wanaoukanusha.

Na haiwafikii ishara yoyote katika ishara za Mola wao ila wanaipinga.

Makusudio ya ishara hapa ni hoja mkato ya kuweko Mwenyezi Mungu na umoja wake, ufufuo na Utume wa Muhammad. Maana ni kuwa makafiri wanakataa dalili ya haki na wanaipinga bila ya kuichunguza. Lau wangelikuwa ni watafutaji ukweli wangeliangalia dalili na kuzingatia maana yake. Ama kukataa na kuipinga kabla ya kuichunguza ni inadi na ujuba.

### HAKUNA UDIKTETA ARDHINI WALA MBINGUNI

Wametofautiana wafasiri katika kuainisha makusudio ya hoja waliyoipinga na kuidharau. Je, ni Qur'an au muujiza mwingineo katika miujiza ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**? Au ni miujiza ya Mitume wote? Nimegundua wakati nikifuatilia tofauti hizi kuwa Aya hii tunayoifasiri na mfano wake katika Qur'an zimekusanya maana ambayo wafasiri wamejihimu kuisherehesha (kuifafanua).

Aya imekusanya dalili kwamba Uislamu unasimamia uhuru wa akili na kutoa maoni na kwamba si haki kwa yeyote, vyovyote awavyo kumtaka mwingine akubali maneno yake hivi hivi tu kwa upofu na bila ya dalili. Hata Muumba wa ulimwengu, ambaye neno lake ni tukufu, hawalazimishi waja wake kumwamini yeye na vitabu vyake, bila ya dalili.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasimamisha hoja kwa kila anayoyasema na kuyatolea mwito na kumtaka kila mwenye akili kuichunguza na kuangalia vizuri maana yake. Mwenyezi Mungu katika hilo ametukuka kabisa - ni kama kila mjuzi anayechunga haki; hata kama ukiwa mbali mshabaha wa Muumba na kiumbe.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

﴿أَوَلَمْ يَتَفَكَّرُوا فِي أَنفُسِهِم مَّا خَلَقَ اللَّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ﴾

"Je, hawafikiri katika nafsi zao. Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ila kwa haki" (30:8)

Na akasema:

﴿أَفَلَمْ يَنظُرُوا إِلَى السَّمَاءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَاهَا وَزَيَّنَّاهَا وَمَا لَهَا مِن فُرُوجٍ﴾

"Je, hawaangalii mbingu zilizo juu yao, vipi tulivyozijenga na tukazipamba wala hazina nyufa" (50:6)

Na akasema tena:

﴿كَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ﴾

"Namna hii tunazipambanua ishara kwa watu wanaofikiri" (10:24)

Aya hizi na nyinginezo, zinafahamisha kwa dalili mkato kuwa yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu huleta dalili na hoja kwenye mwito wa haki na kutoa mwito wa kuzifikiria vizuri na kuzichunguza.

Akipinga yule asiyeamini ila yale anayoyataka yeye, basi yeye peke yake ndiye mwenye jukumu la kukanusha kwake na kupinga kwake.

Wameikadhibisha haki ilipowafikia; kwa hiyo zitawafikia habari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

Mtu anaweza kujitia kutoijua haki bila ya kuitilia umuhimu, na kutoiamini, lakini akawa haiungi mkono wala kuipiga vita; kama ilivyo kwa mtu asiyejali mambo. Au anaweza kuwa katika msimamo wa mwenye kuikadhibisha.

Huyu ni mwenye kiburi, ikiwa atakadhibisha na huku anajijua. Ama akiikadhibisha na kuidharau, basi huyo ni mwenye kuipiga vita. Wa kwanza kosa lake ni hafifu kuliko wa pili kwa sababu yeye anafanana na mtu asiyepiga kura.Wa pili naye dhambi yake ni hafifu kuliko watatu kwa sababu yeye ameitia kura yake kwa waongo. Ama wa tatu amekadhibisha na akadhihirisha harakati dhidi ya haki, naye ndiye aliyekusudiwa kukemewa na kupewa kiaga, na kwamba yeye atakutana na malipo ya inadi yake na istihzai yake.

Je hawaoni vizazi vingapi tulivyoviangamiza kabla yao? Tuliwamakinisha katika nchi tusivyowamakinisha nyinyi.

Waarabu wa kijahiliya walikuwa wakijua mengi kuhusu watu wa Ad, Thamud, Lut na wengineo, na katika misafara yao walikuwa wakiona athari zao wakizishuhudia na kuzizungumzia. Walikuwa wakijua kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwaangamiza kwa sababu wao walikadhibisha haki waliyokuja nayo Mitume yao kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Aya hii inawahusu wale waliomkadhibisha Muhammad **(s.a.w.w)** kuwa wazingatie kuangamia kwa vizazi vilivyo pita. Nao walikuwa na milki na nguvu wasizokuwa nazo hao wanaoambiwa - Waarabu wa kijahiliya, Tukawapelekea mvua nyingi.

Yaani mvua inayoleta mavuno na kuwamiminia riziki. Na tukaifanya mito inapita chini yao. Ni fumbo la rutuba na mavuno mengi. Kisha tukawaangamiza kwa dhambi zao Mali na nguvu hazikuwafaa kitu. Na tukaanzisha baada yao karne nyingine. Mwenye akili ni yule mwenye kupata funzo kutokana na wengine kabla ya mwengine kupata funzo kutoka kwake.

6

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَابًا فِي قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَـٰذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ﴾

7. Na lau tungelikuteremshia maandishi katika karatasi na wakayagusa kwa mikono yao, bila shaka wale waliokufuru wangelisema: Haya si chochote ila ni uchawi dhahiri.

﴿وَقَالُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ مَلَكٌ وَلَوْ أَنزَلْنَا مَلَكًا لَّقُضِيَ الْأَمْرُ ثُمَّ لَا يُنظَرُونَ﴾

8. Wanasema: Mbona hakuteremshiwa Malaika. Na kama tungeliteremsha Malaika, hakika amri ingekwishahukumiwa kisha wasingelipewa nafasi.

﴿وَلَوْ جَعَلْنَاهُ مَلَكًا لَّجَعَلْنَاهُ رَجُلًا وَلَلَبَسْنَا عَلَيْهِم مَّا يَلْبِسُونَ﴾

9. Na kama tungelimfanya Malaika, bila shaka tungelimfanya mtu. Na tungeliwavisha yale wanayoyavaa.

﴿وَلَقَدِ اسْتُهْزِئَ بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُم مَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ﴾

10. Na hakika walifanyiwa stihzai Mitume kabla yake, lakini yakawazunguka wale waliofanya mzaha miongoni mwao, yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

﴿قُلْ سِيرُوا فِي الْأَرْضِ ثُمَّ انظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ﴾

11. Sema: Tembeeni katika ardhi, kisha muone ulikuwaje mwisho wa wa wale waliokadhibisha?

## LAU TUNGELIKUTEREMSHIA KARATASI

**Aya 7 - 11**

### MAANA

Na lau tungelikuteremshia maandishi katika karatasi

Mtume **(s.a.w.w)** alikaa Makka miaka kumi na tatu tangu kuteremshiwa Wahyi mpaka alipohama kwenda Madina. Katika muda wote huu alikuwa akiwalingania watu hapo kwenye Tawhid na uadilifu, na kuwakataza ushirikina na ukandamizaji.

Mfumo wake katika kutoa mwito ulikuwa ni hekima na mawaidha mazuri. Wakamwitikia wachache wao na wengi wao hawakumwitikia.

Isitoshe hawakutosheka kutomwitikia, bali walimpiga vita na kumuudhi kwa mikono yao na mara nyingine kwa ndimi zao. Akawa anavumilia maudhi yao na akijitahidi ili waamini, lakini Mwenyezi Mungu (s.w.t) akamwambia:

﴿وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ﴾

"Na wengi katika watu hawatakuwa wenye kuamini hata ukijitahidi vipi" (12:103)

Na akasema: Na lau tungelikueremshia maandishi katika karatasi na wakayagusa kwa mikono yao, bila shaka wale waliokufuru wangelisema: Haya si chochote ila ni uchawi dhahiri."

Yaani lau tungelikuteremshia maandishi katika ukurasa mmoja, wakayaona na wakayagusa na kuyashuhudia na macho yao wangeliyatia ila na kusema ni uchawi.

Aina hii ya watu iko katika kila kizazi na kila mahali. Wakati wetu huu kuna kundi kubwa la watu wasiotosheka na upinzani wa kuhisiwa na kuguswa, mpaka wakaviita vitu kwa vinyume vyake; mbwa mwitu wakamwita punda na nyoka wakamwita njiwa wa amani.

Hii Amerika inapigana vita vya kuangamiza watu katika Vietnam na huku inasema sisi tunajenga na kutumikia uhai, Na hiyo Israil inachokoza, kisha inasema sisi ndio tuliochokozwa.

Wanasema: Mbona hakuteremshiwa Malaika.

Dhamir ya 'wanasema' inawarudia washirikina wa Kiquraish. Walimtaka Mtume **(s.a.w.w)** awateremshie Malaika ashuhudie anayoyalingania, na awe na msaada wa kutekeleza risala yake. Mfano wa Aya hii ni kama Aya ile isemayo:

﴿وَقَالُوا مَالِ هَـٰذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ الطَّعَ امَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ لَوْلَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مَلَكٌ فَيَكُونَ مَعَهُ نَذِيرًا﴾

"Na wakasema: Ana nini Mtume huyu anakula chakula na anakwenda sokoni. Mbona hakuteremshiwa Malaika awe muonyaji pamoja naye." (25:7)

Na kama tungeliteremsha Malaika, hakika amri ingekwishahukumiwa kisha wasingelipewa nafasi.

Yaani lau kama Mwenyezi Mungu angeliwateremshia Malaika wangelikufa mara moja bila kungojea. Sasa hapa utauliza, kuna uhusiano gani kufa kwao mara moja na kuteremshiwa Malaika?

Baadhi ya wafasiri wamejibu kuwa watu wakimwona Malaika roho zao zitatoweka kabisa kutokana na vitisho wanavyoviona, Lakin kauli hii si ya kutegemewa kabisa. Wengine wakasema: Imetangulia katika hekima ya Mwenyezi Mungu kumwangamiza kila anayehalifu Malaika.

Kauli hii nayo ndiyo haifai kabisa kuliko ile iliyotangulia; Kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) hawaangamizi wanaomhalifu katika maisha haya, wala Malaika hawana utukufu zaidi ya Mwenyezi Mungu ambaye umetukuka sana utukufu wake.

Jibu sahihi ni kuwa: uhusiano uliopo kwenye kufa na kuteremshwa Malaika ni siri ambayo Mwenyezi Mungu hakuidhihirisha kwa waja wake wala siri hii haiwezi kujulikana na akili. Kwa hiyo ni wajibu kunyamaza aliyoyanyamazia Mwenyezi Mungu.

Na kama tungelimfanya Malaika, bila shaka tungelimfanya mtu.

Lau Mwenyezi Mungu angelimtuma Malaika kwa watu, angekuwa na hali mbili tu: Ama abakie na Sura yake au awe katika Sura ya mtu.

Na kubakia katika Sura yake na wakati huo huo kuwa mjumbe kwa watu, ni jambo lisilowezekana. Kwa sababu tabia ya Malaika si kama tabia ya mtu. Na kufikisha ujumbe kunahitajia kutangamana na hao watu, nako hakupatikani ikiwa maumbile na tabia hazilingani. Zaidi ya haya ni kwamba Malaika hawakuumbwa kuishi katika sayari hii.

Na lau angelikuwa katika mfano wa binadamu wangelisema tunataka Mtume wa kimalaika. Kwa hiyo Malaika kwa Sura yake ya kimalaika

hawezi kufikisha ujumbe na kwa sura ya mtu hawezi kuaminiwa na washirikina wa Makka.

Kwa hiyo tatizo litabakia hivyo hivyo bila ya ufumbuzi. Kwa hakika ni kwamba Aya hii inaelezea wazi kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwajadili wakadhibishaji kwa mfumo wa mantiki ambao wenye akili wanautumia kuwanyamazisha wabishani wao.

Na tungeliwavisha yale wanayoyavaa.

Yaani lau Mwenyezi Mungu Mtukufu akiwajaalia Malaika katika Sura ya mtu, watu wangelidhani kwamba yeye ni mtu hasa.

Na hakika walifanyiwa stihzai Mitume kabla yake, lakini yakawazunguka wale waliofanya mzaha miongoni mwao, yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

Yaani tulia ewe Muhammad kutokana na dharau unazozipata kwa watu wako.! Kwani kudharauliwa Mitume sio jambo lililoanza sasa, bali lilikuwako tangu zamani. Na Mwenyezi Mungu aliwaangamiza waliowafanyia mizaha Mitume wao; na yatawapitia wanaokufanyia mzaha yale yaliyowapitia waliokuwa kabla yao. Hayo yalikuwa, kwani Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwaangamiza waliomdharau Muhammad **(s.a.w.w)**; alipomwambia:

﴿إِنَّا كَفَيْنَاكَ الْمُسْتَهْزِئِينَ﴾

"Hakika sisi tumekutoshea (dhidi ya) wanaofanya mzaha (15:95)

Sema: Tembeeni katika ardhi, kisha muone ulikuwaje mwisho wa wa wale waliokadhibisha?

Tafsir yake imekwishatangulia katika Juz 4 (3:137).

﴿قُل لِّمَن مَّا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ قُل لِّلَّـهِ كَتَبَ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ لَيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ﴾

12. Sema: Ni vya nani vilivyomo ardhini na mbinguni? Useme ni vya Mwenyezi Mungu, Amejilazimishia rehema, Hakika atawakusanya Siku ya Kiyama. Isiyo na shaka, Wale ambao wamezitia hasarani nafsi zao, basi wao hawaamini.

﴿وَلَهُ مَا سَكَنَ فِي اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ﴾

13. Ni vyake vilivyotulia katika usiku na mchana; naye ndiye asikiaye na ajuaye.

﴿قُلْ أَغَيْرَ اللَّـهِ أَتَّخِذُ وَلِيًّا فَاطِرِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ يُطْعِمُ وَلَا يُطْعَمُ قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَسْلَمَ وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ﴾

14. Sema: Je nimfanye mlinzi asiyekuwa Mwenyezi Mungu; naye ndiye anayelisha, wala halishwi. Sema: Hakika mimi nimeamrishwa niwe wa mwanzo katika wenye kusilimu, Na wala kabisa usiwe katika washirikina.

﴿قُلْ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ﴾

15. Sema: Hakika mimi ninaogopa adhabu ya siku kubwa ikiwa nitamwasi Mola wangu.

﴿مَّن يُصْرَفْ عَنْهُ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمَهُ وَذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْمُبِينُ﴾

16. Atakayeepushwa nayo siku hiyo, hakika (Mwenyezi Mungu) amemrehemu na huko ndiko kufuzu kuliko wazi.

## AMEJILAZIMISHIA REHEMA

**Aya 12 - 16**

### MAANA

Sema: Ni vya nani vilivyomo ardhini na mbinguni? Useme ni vya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume wake mtukufu kuwauliza Washirikina wa Kiarabu: Ni nani anayemiliki mbingu na ardhi? Kisha akamwamrisha kuwajibu kuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake, yeye ndiye Mfalme wa wafalme.

Inawezekana kuwa yeye ndiye muulizaji na mwenye kujibu. Kwa sababu mwulizaji na mwenye kuulizwa wanaafikiana na jawabu. Kwani Washirikina wa Kiarabu walikuwa wakiamini kuwa Mwenyezi Mungu ni Muumba wa ulimwengu na ndiye mwenye kumiliki:

﴿وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ ا للَّـهُ فَأَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ﴾

"Ukiwauliza ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na akalitiisha jua na mwezi? Bila shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Basi wapi wanakogeuzwa?" (29:61)

**Unaweza kuuliza**: maadamu mambo yako hivyo, basi kuna faida gani ya kuuliza?

**Jibu**: Makusudio ya swali na jibu lake ni kumvuta mbishani akiri uwezekano wa kufufuliwa, na kusimamisha hoja juu yake. Kwa sababu ikiwa yeye ndiye Muumbaji wa ulimwengu na ndiye mwenye kuumiliki, basi anaweza kuumaliza na kuurudisha tena.

Amejilazimishia rehema.

Ameirudia Mwenyezi Mungu (s.w.t) jumla hii katik Sura hii Aya 54.

Wafasiri wanasema Mwenyezi Mungu amejiwabishia rehema kwa wajibu wa fadhila na ukarimu. Na sisi tunaamini kuwa Mwenyezi Mungu ni mwenye fadhila na ukarimu; wakati huo huo tukiamini kuwa rehema yake ni natija ya kujitosheleza na kila kitu na kuwa kila kitu kinamhitajia yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa sababu kiumbe kwa tabia yake anahitajia usaidizi wa Muumbaji na rehema zake kwa uhitajio wa sababu kwenye ilichokisababisha.

Kwa hiyo basi, rehema ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake haiepukani na dhati yake Mwenyezi Mungu na ukamilifu wake. Hivyo basi maana ya Amejilazimishia rehema yanakuwa kwamba rehema yake inalazimiana na dhati yake takatifu; sawa na ulivyo uweza na ujuzi.

Hakika atawakusanya Siku ya Kiyama.

Mkusanyiko huu vilevile ni lazima; ndio maana Mwenyezi Mungu Mtukufu akausifu kwa kusema: Isiyo na shaka, kwa sababu Siku hiyo atalipizwa kisasi aliyedhulumiwa kwa aliyemdhulumu na atalipwa mwovu mfano wa uovu wake, na mwema atalipwa zaidi ya mfano.

Lau si Siku hii, haki ingelikwenda bure na mwenye nguvu ndio angelikuwa mwenye amri na wala sio Muumbaji wa ulimwengu.

Wale ambao wamezitia hasarani nafsi zao, basi wao hawaamini hawaamini.

Zamakhshari anasema: "Makafiri wamechagua hasara, kwa hiyo hawataamini." Zamakhshari ni katika Mu'tazila wasemao mtu ana hiyari, halazimishwi.

Razi naye akasema; "Mwenyezi Mungu ndiye aliyejaalia hasara yao kwa hiyo hawakuamini" Razi ni katika Ashaira wasemao mtu analazimishwa hana hiyari. Wengine wamesema hawakuamini Makafiri kwa ajili ya kufuata baba zao.

Tuonavyo sisi ni kuwa Aya inaashiria kwenye hakika ya mtu na kwamba mtu ni nafsi yake na mwili wake, na kila kimoja katika viwili hivyo kinamkamilishia mwenzake na kwamba mtu hatakuwa na maisha sahihi mpaka avitumikie vyote viwili.

Mwenye kufanya amali kwa ajili ya roho tu bila mwili, au kwa mwili tu bila ya roho, basi amepata hasara na mwenye kupata hasara hiyo hawi na amani yoyote.

Ni vyake vilivyotulia katika usiku na mchana; naye ndiye asikiaye na ajuaye.

Yaani yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye mwenye kumiliki kila kitu. **Unaweza kuuliza**: kuwa maana haya yashafahimishwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aya iliyotangulia: 'Sema ni vya nani vilivyomo ardhini na mbinguni? Useme ni vya Mwenyezi Mungu.' Kuna wajihi gani wa kukaririka huku?

**Wafasiri wamejibu kuwa**: Aya ya kwanza imeeleza viumbe kwa wakati na hii ni kwa mahali; navyo ni vyombo viwili vya kila kiumbe, iwe ni kwa kimaada au kimaana (kimwili au kiroho). Kwa hiyo ukapatikana ujumla na maana kwa Aya zote mbili; na akafuatishia Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa sifa mbili za usikizi na ujuzi ili kutilia mkazo mkusanyiko wa maana hii.

Mara nyingi tumeeleza kuwa kukaririka katika Qur'an ni jambo la kawaida, lakini wafasiri wamekuwa wakijaribu kuleta kitu tu, hata kama hakuna haja.

Sema: Je nimfanye mlinzi asiyekuwa Mwenyezi Mungu?

Vipi nimtake msaada mwingine, Naye ni Muumba wa mbingu na ardhi? naye analisha na wala halishwi. Mwingine hawezi kujizuia na madhara wala kujinufaisha.

Sema: Hakika mimi nimeamrishwa niwe wa mwanzo katika wenye kusilimu.

Kwa sababu Muhammad ni mlinganiaji wa kwanza kwenye Uislamu, basi anakuwa yeye ni Mwislamu wa kwanza katika umma wake. Vinginevyo atakuwa katika wale ambao wanaamrisha na wao hawafuati amri. Hiyo haiwezekani kabisa kwa yule aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu kwa risala yake.

Na wala kabisa usiwe katika washirikina.

Ni muhali kuwa miongoni mwao. Maneno haya yamesihi tu kwa vile ni maelekezo kutoka kwa aliye juu kwenda kwa aliye chini; kama tulivyosema mara nyingi.

Sema: Hakika mimi ninaogopa adhabu ya siku kubwa ikiwa nitamwasi Mola wangu.

Mtume kufanya maasia haiwezekani kutokana na cheo cha Isma. Lakini 'kukadiria muhali si muhali' Lengo lake hapa ni kuthibitisha au kutilia mkazo msingi wa usawa baina ya watu wote mbele ya Mwenyezi Mungu na kwamba yeye ameumba pepo kwa anayemtii, hata kama ni mtumwa wa Kihabeshi; na akaumba moto kwa anayemwasi, hata kama ni sharifu wa Kiquiraish.

Na kumcha Mwenyezi Mungu (s.w.t) kunakuja kwa kiasi cha kujua ukubwa wake:

﴿إِنَّمَا يَخْشَى اللَّـهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ﴾

"Kwa hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wenye elimu tu" (35:28) na hasa Mitume.

Atakayeepushwa nayo siku hiyo, hakika (Mwenyezi Mungu) amemrehemu na huko ndiko kufuzu kuliko wazi.

Kila mwenye kuhofia vituko vikubwa, huona uokovu kuwa ni rehema kubwa, na kufuzu ni jambo adhimu.

﴿وَإِن يَمْسَسْكَ اللَّـهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ وَإِن يَمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

17. Na kama Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hakuna wa kuyaondoa ila yeye, Na akikugusisha kheri, basi yeye ndiye mwenye uweza juu ya kila kitu.

﴿وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ﴾

18. Naye ndiye mwenye kuwatenza nguvu waja wake; naye ndiye mwenye hekima mwenye habari.

﴿قُلْ أَيُّ شَيْءٍ أَكْبَرُ شَهَادَةً قُلِ اللَّـهُ شَهِيدٌ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَـٰذَا الْقُرْآنُ لِأُنذِرَكُم بِهِ وَمَن بَلَغَ أَئِنَّكُمْ لَتَشْهَدُونَ أَنَّ مَعَ اللَّـهِ آلِهَةً أُخْرَىٰ قُل لَّا أَشْهَدُ قُلْ إِنَّمَا هُوَ إِلَـٰهٌ وَاحِدٌ وَإِنَّنِي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ﴾

19. Sema: Ni kitu gani kikubwa zaidi kwa kutoa ushahidi? Mwenyezi Mungu ndiye shahidi baina yangu na baina yenu. Na nimepewa wahyi Qur'an hii ili niwaonye kwayo na kila imfikiayo. Je, kweli nyinyi mnashuhudia kwamba wako waungu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Mimi sishuhudii. Sema: Yeye ni Mungu mmoja tu, na hakika mimi ni mbali na hayo mnayoyashirikisha.

## HAKUNA MWONDOAJI MADHARA ILA MWENYEZI MUNGU

**Aya 17 - 19**

### MAANA

Na kama Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hakuna wa kuyaondoa ila yeye.

Aya hii inafahamisha kuwa: madhara kama vile ufukara, maradhi n.k. ni kazi ya Mwenyezi Mungu sio ya mtu. Vilevile kuyaondoa na kuepukana nayo ni kazi yake. Kwa hiyo kuna haja gani ya kufanya juhudi na kufanya kazi?

**Jibu**: **Kwanza**, kufanya juhudi na kujitafutia riziki ni wajibu kiakili na kinakili (nukuu). Ama kiakili ni kwamba uhai haukamiliki ila kwa kazi. Na kinukuu zimepituka kiwango cha mutawatir. Miongoni mwazo ni:

"Tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila ya Mwenyezi Mungu" (62:10)

﴿هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ ذَلُولًا فَامْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا مِن رِّزْقِهِ وَإِلَيْهِ النُّشُورُ﴾

"Yeye ndiye aliyeidhalilisha ardhi kwa ajili yenu; basi tembeeni katika pande zake na mle katika rizki zake." (67:15).

Katika Hadith ni **"Safirini mtapata faida."** Nyingine ni: **"Fanyianeni dawa enyi waja wa Mwenyezi Mungu, kwani yule ambaye ameteremsha ugonjwa, ameuteremshia na dawa".**

Kwa hiyo basi atakayezembea akaacha kuhangaika na akapatwa na madhara, yeye mwenyewe ndiye atakayekuwa na jukumu. Mwenye kuhangaika bila ya kuzembea na akaguswa na madhara, basi jamii yake iliyo mbovu katika hali na hukumu zake ndiyo itakayokuwa na jukumu. Ikiwa jamii yake pia ni nzuri basi atakuwa amedhurika kwa kudura ya Mwenyezi Mungu na majaaliwa yake.

Pili, Hakika Mwenyezi Mungu hamtakii madhara mja wake yeyote. Vipi iwe hivyo, na hali yeye ndiye aliyesema: "Na mimi siwadhulumu waja." (50:29) Na ndiye mwenye kusema:

"Na Mwenyezi Mungu ni mpole kwa waja" (2:207)

Na katika Hadith imeelezwa: **"Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwahurumia zaidi waja wake kuliko mama anavyomhurumia mwanawe."**

Kwa hiyo basi makusudio ya madhara katika Aya hii ni yale anayolipwa mja kutokana na amali yake; au ni mtihani kwa ajili ya masilahi yake na mengineyo ambayo hayapingani na uadilifu wake Mwenyezi Mungu na rehema yake, Tumeyafafanua hayo tulipofasiri (5:100).

Na akikugusisha kheri, basi yeye ndiye mwenye uweza juu ya kila kitu.

Yaani hakuna wa kuzuia heri na fadhila zake. Arrazi anasema: "Mwenyezi Mungu katika kheri ametaja kuwa yeye ndiye mwenye uweza juu ya kila kitu na katika madhara ametaja kuwa hakuna wa kuyaondoa ila yeye, ametaja hivyo kwa kufahamisha kuwa matakwa ya Mwenyezi Mungu kufikisha kheri yanashinda yale matakwa yake ya kufikisha madhara".

Naye ndiye mwenye kuwatenza nguvu waja wake; naye ndiye mwenye hekima mwenye habari.

Kutenza nguvu ni ishara ya uweza wa Mwenyezi Mungu na kuwa na habari ni ujuzi wake. Amewatenza nguvu Mwenyezi Mungu waja wake kwa kuwafanya waweko bila ya kutaka kwao; na amewatenza nguvu vilevile kwa mauti.

Ibnul-Arabi katika Futuhatil-makkiyya anasema: "Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewatenza nguvu waja wake kwa sababu wao wamempinga na wakagombana naye katika kuhalifu hukumu zake na mwenye kugombana na Mwenyezi Mungu basi yeye ni mwenye kutenzwa nguvu na hapana budi kushindwa.'

Sema: Ni kitu gani kikubwa zaidi kwa kutoa ushahidi?

Yako maelezo katika baadhi ya Hadith kuwa Washirikina wa Makka walimwambia Mtume: Mayahudi na Wakristo hawashuhudii Utume wako

hebu tuonyeshe anayekushuhudia, Ndipo akateremsha Mwenyezi Mungu (s.w.t) Aya hii.

Yaani waulize Ewe Muhammad ni nani ambaye ushahidi wake uko juu ya ushahidi wote? Kisha akamwamrisha kuwajibu:

Sema: Mwenyezi Mungu ndiye shahidi baina yangu na baina yenu.

Hakuna jawabu halisi kama hili, nalo ni kuwa shahidi baina yetu ni Mwenyezi Mungu.

Na nimepewa wahyi Qur'an hii ili niwaonye kwayo na kila imfikiayo.

Qur'an ni ushahidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya Mtume Muhammad, ambayo imewashinda kuleta hata Sura moja mfano wake, wakajaribu wakashindwa. Kushindwa huku ni ushahidi mkubwa wa ukweli wa Mtume katika risala yake.

Kauli yake: 'Ili niwaonye kwayo na kila imfikiayo,' Maana yake ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemteremshia hii Qur'an ili imuonye kila itakayemfikia mpaka siku ya ufufuo. Sahaba mmoja alikuwa akisema: "Atakeyefikiwa na Qur'an ni kama kwamba amemwona Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**"

Vilevile Aya hii inafahamisha kuwa ambaye haukumfikia mwito wa Muhammad **(s.a.w.w)**, basi anasamehewa katika kuacha Uislamu. Hayo nimeyazungumza kwa ufafanuzi katika Juz. 4 (3:115).

Je, kweli nyinyi mnashuhudia kwamba wako waungu wengine pamoja na Mwenyezi Mungu?

Swali hapa ni la kukanusha na kuyaweka mbali hayo. Maana ni vipi mtamfanya Mwenyezi Mungu pamoja na waungu wengine baada ya kuwa wazi dalili za umoja wake Mwenyezi Mungu Mtukufu! Kisha Mwenyezi Mungu akamwamrisha Mtume wake kujibu kuwa yeye hashuhudii kama wanavyoshuhudia.

Sema: Mimi sishuhudii. Kisha akamwamrisha jambo jingine: Sema: Yeye ni Mungu mmoja tu, na hakika mimi ni mbali na hayo mnayoyashirikisha ya kuabudu masanamu na mengineyo.

7

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَعْرِفُونَهُ كَمَا يَعْرِفُونَ أَبْنَاءَهُمُ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ﴾

20. Wale tuliowapa Kitab wanamjua kama wanavyowajua wana wao, Wale ambao wamezitia hasarani nafsi zao hawaamini.

﴿وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّـهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ﴾

21. Na ni nani dhalimu zaidi kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo, Au azikadhibishaye ishara zake? Hakika madhalimu hawatafaulu.

﴿وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا أَيْنَ شُرَكَاؤُكُمُ الَّذِينَ كُنتُمْ تَزْعُمُونَ﴾

22. Na siku tutakapowakusanya wote, kisha tutawaaambia wale walioshirikisha: Wako wapi washirikishwa wenu mliokuwa mnadai?

﴿ثُمَّ لَمْ تَكُن فِتْنَتُهُمْ إِلَّا أَن قَالُوا وَاللَّـهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ﴾

23. Kisha hautakuwa udhuru wao ila kusema Wallahi, Mola wetu! Hatukuwa washirikina.

﴿انظُرْ كَيْفَ كَذَبُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَضَلَّ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ﴾

24. Angalia jinsi wanavyojisemea uwongo wenyewe, Na yamepotea waliyokuwa wakiyazua.

## WANAMFAHAMU KAMAWANAVYO WAFAHAMU WANAWAO

**Aya ya 20 - 24**

### MAANA

Wale tuliowapa Kitab wanamjua kama wanavyowajua wana wao. Waliopewa Kitab ni Mayahudi na Wakristo, Dhamiri ya wanamjua inamrudia Muhammad **(s.a.w.w)**. Aya hii inawakabili maulama wa watu wa Kitab kwamba wao wanamjua vizuri Mtume wa mwisho, kama wanavyowajua wana wao, lakini wao wanaficha yale wanayoyajua. Maana haya yamekaririka katika Aya kadhaa, zikiwemo hizi zifuatazo:

﴿الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِندَهُمْ فِي التَّوْرَاةِ وَالْإِنجِيلِ﴾

"Ambao wanamfuata Nabii asiyesoma wala kuandika ambaye wanamwona ameandikwa kwao katika Tawrat na Injil" (7:157)

﴿أَوَلَمْ يَكُن لَّهُمْ آيَةً أَن يَعْلَمَهُ عُلَمَاءُ بَنِي إِسْرَائِيلَ﴾

Je, haikuwa ishara kwao kwamba wanayajua haya maulama wa wana wa Israil? (26:197)

Yamekwishapita maelezo kwa ufafanuzi katika Juz. 2 (2:146) na Juz. 4 (4:164). Si lazima kwa watu wa Kitab, katika kuujua ukweli wa Muhammad **(s.a.w.w)**, wakute jina lake limeandikwa kwao katika Tawrat na Injil. Kila mwenye kuusoma Uislamu kwa somo sawa sawa na upekuzi, ataamini kwa imani isiyokuwa na tashwishi yoyote kwamba Uislamu ni haki na ukweli.

Na mawili hayo (haki na ukweli) ndiyo johari za Uislamu, nguzo yake na lengo lake kutokana na neno Lailaha illa Ilah (Hakuna Mungu isipokuwa Allah) ambalo linamaanisha usawa baina ya watu, kumpa mtu msimamo wa misingi ya kufanya amali na ikhlasi na wala sio kwa misingi ya mali, jaha na nasabu. Na vilevile mshikamano na majukumu ya kila kiongozi kwa wachini wake katika mwito wa amani na usalama, maendeleo na utulivu usiokuwa na mwisho.

Wale ambao wamezitia hasarani nafsi zao hawaamini.

Imepita, punde tu Tafsir yake katika Aya 12 ya Sura hii.

Na ni nani dhalimu zaidi kuliko yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo.

Makusudio ya dhulma hapa ni Ukafiri. Kwa sababu kila anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, basi yeye ni kafiri. Hakuna tofauti yoyote baina ya anayemshirikisha na yule mwenye kugeuza hukumu yoyote katika hukumu zake kwa makusudi na kujua; na yule mwenye kudai unaibu wa maasum au kuwaombea viumbe haki, na hali anajua kuwa yeye ni mzushi na mwongo. Wote hawa ni makafiri waovu kwa Ijmai (kongamano), Kitab na Hadith.

Au azikadhibishaye ishara zake? Hakika madhalimu hawatafaulu.

Jumla iliyotangulia imeashiria yule anayeleta yasiyokuwepo; kama mwenye kumfanyia Mwenyezi Mungu washirika au mtoto. Na jumla hii inaashiria yule mwenye kukanusha vilivyopo, kama vile anayemkana

Mwenyezi Mungu kabisa. Hukumu ya wote wawili ni moja, kila mmoja wao ni dhalimu:

﴿مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ﴾

"Madhalimu hawana rafiki mpenzi wala muombezi anayetiiwa" (40:18) "Na siku tutakapowakusanya wote, kisha tutawaambia wale walioshirikisha: Wako wapi washirikishwa wenu mliokuwa mnadai" Wanaomwamini Mwenyezi Mungu wako aina mbili: Kuna wale wanaoamini uungu wake na kuwa ni mmoja tu. Hawa wanaitwa wanaompwekesha Mungu (watu wa Tawhid). Na kuna wale wanaoamini uungu wake na uungu mwingine. Hawa ndio wale walioharibu imani yao kwa mchanganyiko huu; na wakawa sawa na wale wanaomkana Mwenyezi Mungu. Kwa sababu kumjaalia Mwenyezi Mungu mfano maana yake hasa ni kumkana Mwenyezi Mungu kabisa. Kwani ilivyo nikuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) hana mshabaha wala mfano:

"Hakuna kama mfano wake kitu chochote." (42:11)

Mwenyezi Mungu atawakabili washirikina na swali hili (wako wapi washirikishwa mliokuwa mnadai na mkiwataka msaada, kama mnavyomtaka msaada Mwenyezi Mungu) kwa njia ya kutahayariza na kukaripia, na wala sio kwa njia ya kuhakikisha.

**Unaweza kuuliza**: kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema wako wapi washirikishwa wenu na wala hakusema wako wapi washirikishwa wangu, pamoja na kuwa makafiri ndiyo waliosema kuwa Mungu ana washirika na sio wao?

**Jibu**: Ni kwa kuwa wao ndiyo wako karibu zaidi na mnasaba huo; kwani wao ndio waliozusha ushirikina ambao hauna athari kabisa.

Kisha hautakuwa udhuru wao ila kusema Wallahi, Mola wetu! Hatukuwa washirikina.

Makusudio ya udhuru wao ni udhuru wao wa kushirikisha na kuabudu mizimu. Maana ni kuwa mwisho wa ushirikina waliozusha ni kiapo chao cha uovu kwamba wao hawakuwa washirikina.

**Unaweza kuuliza**: Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwasimulia watu hao: 'Wallahi Mola wetu! Hatukuwa washirikina' inapingana na kauli yake yake. "Wala hawatamficha Mwenyezi Mungu na mazungumzo (yao)" (4:42)

Zaidi ya hayo ni kuwa inajulikana kuwa mtu hawezi kusema uongo Siku ya Kiyama.

**Jibu**: Katika Kiyama kutakuwa na vituo kadhaa, baadhi yake mtu ataweza kukana na ambapo katika kituo hicho miguu yake na mikono yake haitamtolea ushahidi wa yale aliyokuwa akiyafanya. Kwenye kituo hicho ndipo huchukuliwa kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Wallahi Mola wetu! Hatukuwa washirikina' Na katika kituo kingine, atakiri ambapo hapatakuwa na nafasi ya kukana. Hapo ndipo huchukuliwa kauli yake Mwenyezi Mungu: "Wala hawataweza kumficha Mwenyei Mungu neno lolote" Ama kauli ya kuwa mtu atashindwa kabisa kusema uwongo siku ya Kiyama, inakanushwa na Aya isemayo:

﴿يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّـهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُ كَمَا يَحْلِفُونَ لَكُمْ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْكَاذِبُونَ﴾

"Siku atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote; wamuapie kama wanavyoapa kwenu, na watadhani kwamba wamepata kitu. Kwa hakika hao ndio waongo hasa" (58: 18)

**Swali la pili** linatokana na jibu la swali la kwanza nalo ni kuwa: ikiwa mtu ataweza kusema uwongo kesho, bali hata kuapa, kama ilivyo katika maisha haya ya duniani. Basi kuna wajihi gani kuita akhera nyumba ya ukweli na kuiita nyumba yetu hii (dunia) nyumba ya uwongo?

**Jibu**: Makusudio ya kutofautisha huku ni kwamba uwongo hapa duniani unaweza ukamletea mtu manufaa au kumkinga na madhara, Ama huko akhera hautafaa chochote. Kwa maneno mengine, kushindwa kusema uwongo, ni kitu kingine na kuweza kusema bila ya manufaa ni kitu kingine.

Angalia jinsi wanavyojisemea uwongo wenyewe.

Msemo unaelekezwa kwa Mtume **(s.a.w.w)** na makusudio yake ni kwa wote, nako ni kusataajabu kutokana na kukana kwao ushirikina na hali wamekufa juu ya ushirikina. Kila mwenye kukana jambo alilonalo au kudai asiyokuwa nayo kwa makusudi, basi amejidaganya mwenyewe, Mwenyezi Mungu na watu:

Na yamepotea waliyokuwa wakiyazua.

Hiyo inaungana na 'wanavyojisemea uwongo.' Maana yake ni angalia Ewe Muhammad vipi yamewapotea washirikina yale waliyokuwa wakiyatarajia kuwa yatawasaidia na kuwaombea.

﴿وَمِنْهُم مَّن يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ وَجَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَن يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا وَإِن يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا بِهَا حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوكَ يُجَادِلُونَكَ يَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَـٰذَا إِلَّا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ﴾

25. Na miongoni mwao wako wanaokusikiliza, na tumezitia pazia nyoyo zao wasije kuyafahamu na mna uziwi masikioni mwao, Na wakiona kila

Ishara hawaiamini. Hata wakikujia kujadaliana nawe wanasema waliokufuru: Hizi si chochote isipokuwa ni ngano za watu wa kale.

﴿وَهُمْ يَنْهَوْنَ عَنْهُ وَيَنْأَوْنَ عَنْهُ وَإِن يُهْلِكُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ﴾

26. Nao wanamkatazia na wenyewe wanajitenga naye. Na hawaangamizi ila nafsi zao na hawatambui.

## NYOYO ZAO ZINA PAZIA

**Aya 25 - 26**

### MAANA

Na miongoni mwao wako wanaokusikiliza, na tumezitia pazia nyoyo zao wasije kuyafahamu na mna uziwi masikioni mwao.

Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume wake katika Aya hii, baada ya kumwamrisha kuwambia hoja zinazowasimamia, Maana ni kuwa kundi katika hawa wapinzani wanamsikiliza Mtume, nao wanasoma Qur'an, lakini wao hawanufaiki nayo wala hawanufaiki na dalili na hoja nyingine- zo.

Kwa sababu wao tangu mwanzo waling'anga'ania inadi na kiburi, mpaka kung'angania huko kukapofua akili zao zisione haki na kukatia uziwi kwenye masikio yao.

**Unaweza kuuliza**: Dhahiri ya Aya inaonyesha kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyezipofua nyoyo zao akatia uziwi masikio yao. Kwa nini basi wastahiki shutuma na adhabu na hali ya kuwa wamelazimishwa hawana hiyari?

ibu: Kwa vile nyoyo za wapinzani hazikuitambua Qur'an na kunufaika nayo, na masikio yao hayakuisikiliza kwa usikizi wa kufahamu na kuzingatia, imesihi kusema, kimajazi, kwamba nyoyo zao zimefumba na katika masikio yao mna uziwi.

Na kwa vile Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye aliyeumba nyoyo na masikio, imesihi kunasibisha upofu na uziwi kwake yeye kimajazi vilevile.

Ama kulingana na hali halisi ilivyo ni kuwa washirikina ndio wenye jukumu. Kwa sababu wao waliipinga haki kwa kutaka wenyewe. Yamekwishatangulia maelezo ya hayo katika Juz. 1(2:7)

Ni vizuri kuashiria kuwa Aya hii inafahamisha kwa uwazi kwamba Uislam hauna mfano na chochote kwa ulivyo; bali kwa natija zake na athari zake. Kwa hiyo usikizi na uoni ni utekelezaji wa akili, na akili ndiyo inayopanga matendo. Ikiwa kitendo hakikufanyika, basi usikizi na uoni utakuwa hauna maana yoyote; kwa dhahiri au si kwa dhahiri.

Kwa maneno mengine katika Uislamu, mambo yote ya ndani na ya nje, na ya ardhini na ya angani ni nyenzo za manufaa ya watu katika kupangilia maisha yao na kutatua matatizo yao.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Anadai kwamba yeye anamtaraji Mwenyezi Mungu. Amesema uwongo kwa nini matarajio yake hayaonekani katika vitendo vyake, na kila mwenye kutarajia (Mwenyezi Mungu) hujulikana matarajio yake katika vitendo vyake."**

Na wakiona kila Ishara hawaiamini.

Muhammad **(s.a.w.w)** alifichua hakika ya waongo katika watu wapendao mali na jaha. Wakataharuki na kuhisi hatari ya masilahi yao wakakimbilia kukadhibisha na wakasema kuhusu Aya za Mwenyezi Mungu kuwa ni ngano za watu wa kale, na hali wao wana yakini kwamba Qur'an hii ni

mwongozo, lakini wakawa wanaitia njia za shaka shaka na makosa ili wawatumie watu kutokana na upotevu wao na ubatilifu; sawa na wanavyofanya leo watu wa serikali ovu na kanuni za dhuluma.

Na wanamkatazia na wenyewe wanajitenga naye.

Dhamiri ya neno nao inawarudia wale waliopinga haki kwa kupupia masilahi yao. Dhamiri ya wanamkatazia na kujiweka mbali naye, inamrudia Muhammad **(s.a.w.w)**.

Waongo walikataza watu wasimfuate Muhammad **(s.a.w.w)** na wakampinga, vilevile walijaribu kumtesa na wakakusanya majeshi kwa ajili ya kumpiga vita. Si kwa lolote ila ni kwamba yeye amefichua mabaya yao.

Na hawaangamizi ila nafsi zao na hawatambui.

Walitaka kuufanyia vitimbi Uislamu na Mtume wake, balaa ikawafikia wao, walipoangamia baadhi yao siku ya Badr wengine wakajisalimisha wakiwa madhalili na wanyonge siku ya kutekwa Makka. Huu ndio mwisho wa kila mwenye kuzama na kung'ang'ania dhuluma na inadi.

﴿وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وُقِفُوا عَلَى النَّارِ فَقَالُوا يَا لَيْتَنَا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبَ بِآيَاتِ رَبِّنَ ا وَنَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ﴾

27. Na ungeliona watakapoonyeshwa moto wakawa wanasema. Laiti tungerudishwa (duniani) wala hatutakadhibisha ishara za Mola wetu na tutakuwa katika wanaoamini.

﴿بَلْ بَدَا لَهُم مَّا كَانُوا يُخْفُونَ مِن قَبْلُ وَلَوْ رُدُّوا لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ﴾

28. Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangalirudishwa, bila shaka wangeyarudia yale waliyokatazwa na hakika wao ni waongo.

﴿وَقَالُوا إِنْ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ﴾

29. Na kusema: Hakuna kingine ila maisha yetu ya dunia, wala sisi hatutafufuliwa.

﴿وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وُقِفُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ قَالَ أَلَيْسَ هَـٰذَا بِالْحَقِّ قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا قَالَ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنتُمْ تَكْفُرُونَ﴾

30. Na ungeliona watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, Akasema: Je, si kweli haya? Watasema: Kwa nini? Tunaapa kwa Mola wetu. Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyakataa.

﴿قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِلِقَاءِ اللَّـهِ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَتْهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً قَالُوا يَا حَسْرَتَنَا عَلَىٰ مَا فَرَّطْنَا فِيهَا وَهُمْ يَحْمِلُونَ أَوْزَارَهُ مْ عَلَىٰ ظُهُورِهِمْ أَلَا سَاءَ مَا يَزِرُونَ﴾

31. Hakika wameshahasirika wale waliokadhibisha kukutana na Mwenyezi Mungu, na wamefuzu wale waliomwamini, mpaka itakapowajia ghafla saa (Kiyama) watasema: Oo! Majuto yetu juu ya yale tuliyoyapuuza! Nao watabeba mizigo yao migongoni mwao. Angalieni! Ni mabaya mno wanayoyabeba.

﴿وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَعِبٌ وَلَهْوٌ وَلَلدَّارُ الْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ يَتَّقُونَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ﴾

32. Na maisha ya dunia si kitu ila mchezo na upuzi. Na hakika nyumba ya akhera ni bora zaidi kwa wenye takua. Basi je hamtii akili?

## WATAKAPOSIMAMISHWA MOTONI

**Ay 27 - 32**

### MAANA

Na ungeliona watakapoonyeshwa moto.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amerudia kuelezea hali ya wakadhibishaji Siku ya Kiyama, na kwamba wao watakapoona adhabu waliyoandaliwa na thawabu walizoandaliwa waumini, watasema:

Laiti tungerudishwa duniani wala hatutakadhibisha ishara za Mola wetu na tutakuwa katika wanaoamini.

Yaani tutatubia na tufanye amali njema. Lakini masikitiko na mazingatio hayafai chochote ila ikiwa kumwogopa Mwenyezi Mungu na adhabu yake ni kabla ya kutokea adhabu. Ama baada ya kutokea, basi ni kulilia maiti na kusikitika yaliyofutu.

Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani.

Hataokoka kesho na adhabu ya Mwenyezi Mungu ila ambaye yuko wazi katika maisha haya, vitendo vyake vinaambatana na kauli yake; yote mawili yawe ni picha ya dhati yake na hali yake, mpaka viwe vyote ni kama kitu kimoja tu mbele ya Mwenyezi Mungu na watu.

Ama yule mwenye kuzibaziba, ambaye Muumba anayajua yale ayafanyayo na watu hawayajui, miongoni mwa ria na unafiki, huyu yatamdhihirikia malipo ya ria yake na unafiki wake; na nafsi yake itajutia uovu wake na kutamani kujisafisha kwa kurudishwa duniani, lakini wapi!

Na kama wangalirudishwa, bila shaka wangeyarudia yale waliyokatazwa na hakika wao ni waongo.

katika kusema kwao: Laiti tungerudishwa wala hatutakadhibisha ishara za Mola wetu na tutakuwa katika wanaoamini.

Tumesoma habari za wakosaji kadhaa ambao wanatubia wakiwa gerezani, lakini wanapotoka hurudia makosa yao. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَن تَدْعُونَ إِلَّا إِيَّاهُ فَلَمَّا نَجَّاكُمْ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ وَكَانَ الْإِنسَانُ كَفُورًا﴾

"Na inapowafikia dhara katika bahari hupotea wale mnawaomba isipokuwa Yeye tu, lakini anapowaokoa mkafika salama nchi kavu mnageuka; na mwanadamu ni mkanushaji mno" (17:67)

Na kusema: Hakuna kingine ila maisha yetu ya dunia, wala sisi hatutafufuliwa.

Yaani lau wangelirudishwa kwenye maisha yao ya mwanzo wangalisema waliyoyasema mwanzo: Hakuna ufufuo wala hisabu wala malipo.

**Unaweza kuuliza**: Vipi watakanusha na hali wao watakuwa wameshuhudia vituko vikubwa na wakaonyeshwa, mpaka wakataka kujitakasa nayo na kuahidi kuwa hawatarudia?

**Jibu**: Wao wanajua fika kwamba hisabu na adhabu itakuwa tu, hapana budi. Wakati huo huo wanajua kuwa lau wataitangaza haki na kuinyenyekea, chumo na faida zao watazikosa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

﴿وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا﴾

"Na wakazikanusha (ishara zetu) na hali yakuwa nafsi zao zina yakini nazo kwa dhulma na kujivuna" (27:14)

Na ungeliona watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, baada ya kukadhibisha kukutana naye. Atasema: Je, si kweli haya? Katika kufasiri Aya ya nne katika Sura hii tulisema kuwa Mwenyezi Mungu analingania kuamini haki pamoja na kusimamisha dalili yake. Mpingaji akiipinga, hoja inakuwa juu yake. Na Aya hii inatilia mkazo hilo na kutaja dalili na hoja walizozikanusha na kuzikadhibisha. Watasema: Kwanini? Tunaapa kwa Mola wetu. Hivi sasa yamepita yaliyopita na hakuna kilichobaki isipokuwa malipo yenye kulingana na adhabu kwa mwenye kukufuru na kukanusha.

Akasema: "Basi onjeni adhabu kwa sababu ya mliyokuwa mkikataa. Haya ni malipo ya kila mwenye kuiweka mbele dunia na kuiacha Akhera na akaificha haki kwa hawa ya nafsi yake.

**Utauliza**: Kauli yake Mwenyezi Mungu kwa Makafiri: 'Je, si kweli haya?' Na kauli yake: "Onjeni adhabu" mbona haziafikiani na kauli yake: "Wala hatawasemeza Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama"? (2:174)

**Jibu**: Makusudio ni kwamba Mwenyezi Mungu hatawasemesha yale yanayowafurahisha, bali atawasemeza yanayowaudhi, kama ilivyo katika Aya hii, na ilivyo katika Aya isemayo:

"Atasema: Tokomeeni humo wala msinisemeze." (23:108)

Hakika wamekwishahasirika wale waliokadhibisha kukutana na Mwenyezi Mungu na wamefuzu wale waliomwamini, mpaka itakapowajia ghafla saa (Kiyama) watasema: Oo! Majuto yetu juu ya yale tuliyoyapuza!

Imam Ali anasema: **"Matunda ya kupuuza ni majuto, na matunda ya uthabiti ni amani."**

Nao watabeba mizigo yao migongoni mwao. Angalieni! Ni mabaya mno wanayoyabeba.

Mizigo ni dhambi na kuibeba mgongoni ni fumbo, yaani kuwa nayo; kama vile isemwavyo: "Amepandwa na shetani." Yaani yuko naye hamwachi. Maana ni kuwa wanaoikadhibisha haki ndio watu wenye hali mbaya zadi huko akhera.

Mmoja wa wafasiri wapya anasema: "Bali mnyama ana hali nzuri zaidi kwa sababu hubeba mizigo mizito,; na mnyama huutua mzigo wake akaenda kupumzika, lakini hawa watakwenda na mizigo yao kwenye Jahannam wakisindikizwa na dhambi."

Na maisha ya dunia si kitu ila mchezo na upuzi." Umetangulia mfano wake katika Juz 4 (3:185)

﴿قَدْ نَعْلَمُ إِنَّهُ لَيَحْزُنُكَ الَّذِي يَقُولُونَ فَإِنَّهُمْ لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَٰكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ
يَجْحَدُونَ﴾

33. Hakika tunajua kwamba yanakuhuzunisha yale wanayoyasema, Basi hakika hao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu wanakataa ishara za Mwenyezi Mungu.

﴿وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا كُذِّبُوا وَأُوذُوا حَتَّىٰ أَتَاهُمْ نَصْرُنَا وَلَا مُبَدِّلَ
لِكَلِمَاتِ اللَّهِ وَلَقَدْ جَاءَكَ مِن نَّبَإِ الْمُرْسَلِينَ﴾

34. Na hakika walikadhibishwa Mitume kabla yako, wakavumilia juu ya kukadhibishwa na kuudhiwa, mpaka ikawafikia nusura yetu. Na hakuna wa kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu, Na bila shaka zimekujia baadhi ya habari za Mitume hao.

﴿وَإِن كَانَ كَبُرَ عَلَيْكَ إِعْرَاضُهُمْ فَإِنِ اسْتَطَعْتَ أَن تَبْتَغِيَ نَفَقًا فِي الْأَرْضِ أَوْ سُلَّمًا فِي السَّمَاءِ
فَتَأْتِيَهُم بِآيَةٍ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى الْهُدَىٰ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْجَاهِلِينَ﴾

35. Na ikiwa ni makubwa kwako huku kukataa kwao, basi kama unaweza kutafuta njia ya chini kwa chini katika ardhi au ngazi kwendea mbinguni na kuwaletea ishara. Na kama Mwenyezi Mungu angelitaka, bila shaka angeliwakusanya kwenye uongofu. Basi usiwe miongoni mwa wajinga

﴿إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ﴾

36. Hakika wanaokubali ni wale tu wanaosikia, Na wafu Mwenyezi Mungu atawafufua kisha watarejeshwa kwake.

﴿وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ قُلْ إِنَّ اللَّهَ قَادِرٌ عَلَىٰ أَن يُنَزِّلَ آيَةً وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا
يَعْلَمُونَ﴾

37. Na husema: Kwa nini hakuteremshiwa ishara kutoka kwa Mola wake? Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye uweza wa kuteremsha ishara yoyote, lakini wengi wao hawajui.

## TUNAJUA KUWA YANAKUHUZUNISHA

**Aya 33 - 37**

### MAANA

Hakika tunajua kwamba yanakuhuzunisha yale wanayoyasema.

Msemo unaelekezwa kwa Mtume **(s.a.w.w)**, Dhamir ya 'wanayoyasema' inawarudia wale waliomkadhibisha Mtume **(s.a.w.w)**. Ama yale wanayoyasema bali waliyasema hasa, ni yale yaliyoashiriwa na Mwenyezi Mungu (s.w.t):

﴿ثُمَّ تَوَلَّوْا عَنْهُ وَقَالُوا مُعَلَّمٌ مَّجْنُونٌ﴾

Kisha wakampa mgongo na wakasema: Amefunzwa (na) ni mwendawazimu." (44:14)

"Wakasema Makafiri: Hakika huyu ni mchawi dhahiri." (10:2) Na mengineyo.

Basi hakika hao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu wanakataa ishara za Mwenyezi Mungu.

Kila mwenye kumpiga vita mwenye haki, basi ameipiga vita haki yenyewe, na kila mwenye kumdharau Mtume kwa kuwa yeye anachukua risala ya aliyemtuma, basi atakuwa amemdharau yule aliyemtuma na sio Mtume mwenyewe.

Washirikina wa Makka walikuwa wakimwita Muhammad **(s.a.w.w)** mkweli mwaminifu, kabla ya Utume. Alipowaletea risala ya Mwenyezi Mungu na kuwasimamishia hoja, walimpiga vita na wakamwita mwendawazimu, mchawi nk.

Kwa hiyo kumkadhibisha kwao huku na hali hii, ni kukadhibisha risala ya Mwenyezi Mungu na hoja zake. Hakuna linalofahamisha hilo kwa dalili zaidi ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّـهَ يَدُ اللَّـهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ﴾

"Hakika wale wanaokubai, kwa hakika wanambai Mwenyezi Mungu; mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao" (48:10)

Na hakika walikadhibishwa Mitume kabla yako, wakavumilia juu ya kukadhibishwa na kuudhiwa, mpaka ikawafikia nusura yetu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anamwambia Mtume wake ikiwa watakukadhibisha, basi wamekadhibishwa Mitume kabla yako na wakaudhiwa katika kufikisha risala yake, wakavumilia juu ya maudhi mpaka ikawajia nusura. Kwa hiyo nawe vumilia kama walivyovumilia; na Mwenyezi Mungu atakunusuru kama alivyowanusuru.

Huu ndio mzunguko wa maisha - mvutano baina ya kheri na shari na haki na batili. Ni muhali kwa mpigania haki asipate maudhi kutoka katika maadui wa haki. Vilevile haki haiwezi kushinda ila wapatikane watakaoinusuru wavumilivu katika jihadi ya haki na wainunue kwa nafsi zao, watu wao na mali zao.

Ni desturi ya Mwenyezi Mungu, wala huwezi kupata mabadiliko katika desturi ya Mwenyezi Mungu, Hii ndio maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Na hakuna wa kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu.

Wala sijui wakati ambao wabatilifu wamekuwa na nguvu kuliko wakati huu tunaoishi. Wameweka vituo vya kijeshi kila mahali, vituo vya kuharibu, silaha kali za kumaliza watu na kubomoa. Wanatawala nyenzo za wananchi wadhaifu, mabenki, magazeti, uchapishaji na usambazaji, Mpaka yule mtu aliye mwaminifu mwenye ikhlasi anajikuta ametupwa hawezi kutoa makala huru au kutangaza haki kupitia kwenye Idhaa. Lakini mhaini, popote atakapoelekea atapata mapokezi na kutukuzwa[1].

Na bila shaka zimekujia baadhi ya habari za Mitume hao.

Yaani tumekusimulia kabla yale yaliyowapata Mitume kutokana na watu wao na jinsi walivyovumilia katika kukadhibishwa na maudhi, na kwamba mwisho ushindi ulikuwa wao.

---

1 7. Kumbuka wakati huo anaouzngumzia mwandishi ni 1967 Je, hivi sasa hali ikoje? Mtarjumu.

Na desturi hii itakupitia wewe, kama iliyowapita wao, wala hakuna mwenye kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu.

Na ikiwa ni makubwa kwako huku kukataa kwao, basi kama unaweza kutafuta njia ya chini kwa chini katika ardhi au ngazi kwendea mbinguni na kuwaletea ishara.

Aya hii ni mfano wa kauli yake Mwenyezi Mungu kumwambia Mtume wake Mtukufu:

﴿فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسَرَاتٍ إِنَّ اللَّـهَ عَلِيمٌ بِمَا يَصْنَعُونَ﴾

"Basi roho yako isitoke kwa majonzi juu yao; hakika Mwenyezi Mungu anayajua yote wanayoyafanya." (35:8)

Aya zote hizi mbili zinatoa picha jinsi Mtume **(s.a.w.w)** alivyokuwa akipata jakamoyo na uchungu kutokanana upinzani wa washirikina kwa mwito wake.

Yaliyompata Mtume kutoka kwa watu wake ni yale yanayoondoa upole wa mpole. Lakini yeye akavumilia na kuwa na matumaini; wala hakuwaapiza bali aliwaombea, akisema: **"Ewe Mola wangu! Wasamehe watu wangu, hakika wao hawajui"**

Pamoja na hayo yote alikuwa akihisi uchungu kwa kufuru zao. Ndipo Mwenyezi Mungu akamwambia kwa Aya hii, ili kumpoza na kumwondolea matumaini na aachane nao; kisha angoje kidogo, aone vile utakavyokuwa mwisho wa wakadhibishaji.

Na kama Mwenyezi Mungu angelitaka, bila shaka angeliwakusanya kwenye uongofu.

Razi anasema kuwa: "Hii inafahamisha kuwa yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu hataki makafiri waamini, bali anataka kuwabakisha kwenye ukafiri.

Lakini hii itakuwa ni dhuluma hasa, na Mwenyezi Mungu hawadhulumu waja. Usahihi wa maana ya jumla hii, ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) hataki kumlazimisha yeyote katika kumwamini, bali anamwachia hiyari yake baada ya kumsimamishia hoja kwa dalili na ubainifu. Lau angelitaka waja wake waamini kwa kusema 'kuwa ikawa', basi asingelikufuru yeyote katika wao. Lakini hekima yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ilitaka ajiingize katika mambo ya watu kama mwamrishaji na mwenye kutoa nasaha, si kama Muumba mwenye nguvu, Umetangulia ufafanuzi katika Juz. 1 (2:26)

Basi usiwe miongoni mwa wajinga.

Atakuwaje Mtume Mtukufu miongoni mwa wajinga na hulka zake ni hulka za Qur'an? Msemo huu umefaa kuelekezwa kwa mtukufu wa viumbe, kwa vile unatoka kwa Muumba wa viumbe na sio kwa kwa aliye kama yeye.

Wanaokubali ni wale tu wanaosikia, Na wafu Mwenyezi Mungu atawafufua kisha watarejeshwa kwake.

Aya hii ni mfano wa Aya isemayo:

﴿إِنَّكَ لَا تُسْمِعُ الْمَوْتَىٰ وَلَا تُسْمِعُ الصُّمَّ الدُّعَاءَ إِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِينَ﴾

"Hakika huwezi kuwasikilizisha wafu wala huwezi kuwasikilizisha viziwi mwito wanapogeuka kurudi nyuma" (27:80)

Maana ni kuwa: Ewe Muhammad! Wale unaopupia waonyeke hawakusikii kwa kufahamu na kuzingatia. Kwa sababu kupenda dunia kumewafanya kama wafu, na wafu haitakikani kuwaambia chochote; bali wanaachwa na mambo yao mpaka siku ya kiyama, watakapoiona adhabu ambayo hawataweza kuikimbia.

Na husema: Kwa nini hakuteremshiwa ishara kutoka kwa Mola wake?

**Utauliza**: vipi wanasema hivi na hali Mwenyezi Mungu amemteremshia Muhammad **(s.a.w.w)** ishara na hoja kadhaa na ubainifu.

**Jibu**: Makusudio ya ishara hapa ni muujiza ule walioutaka wao kuwa ni sharti la wao kumwamini Muhammad **(s.a.w.w)**; hawakusudii muujiza unaomkinaisha mwenye kuitafuta haki, Lau wangeliutaka huo wasingelisema hivyo.

Sema: Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye uweza wa kuteremsha ishara yoyote, ile wanayotaka, lakini yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu haiteremshi kwa kuitikia matakwa na hawaa zao; isipokuwa anateremsha miujiza kulingana na inavyopitisha hekima yake.

Lakini wengi wao hawajui, kuwa anateremsha miujiza kulingana na hekima Yake na sio hawa za watu.

﴿وَمَا مِن دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُم مَّا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِن شَيْءٍ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ﴾

38. Na hakuna mnyama katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake, ila ni umma kama nyinyi, Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha watakusanywa kwa Mola wao.

﴿وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا صُمٌّ وَبُكْمٌ فِي الظُّلُمَاتِ مَن يَشَإِ اللَّهُ يُضْلِلْهُ وَمَن يَشَأْ يَجْعَلْهُ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ﴾

39. Na wale waliokadhibisha ishara zetu ni viziwi na mabubu wako gizani. Amtakaye Mwenyezi Mungu humpoteza na amtakaye humweka katika njia iliyonyooka.

## WANYAMA NA NDEGE NI UMMA

**Aya 38-39**

### LUGHA

Mnyama, ni kila anayetembea katika ardhi wakiwa ni: Watu, wanyama na wadudu.

### MAANA

Na hakuna mnyama katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake, ila ni umma kama nyinyi.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anabainisha katika Aya hii kwamba baina yetu na wanyama kuna aina ya kufanana, lakini hakufafanua aina yenyewe. Je, tunafanana katika kuwa wao ni viumbe wa Mwenyezi Mungu; au katika kumwamini Mwenyezi Mungu na kumsifu kwa sifa zake njema? Au tunafanana katika kuwa wao ni aina zinazojulikana kwa majina; kama zinavyojulikana koo na kabila? Au ni katika kupanga maisha yao na kufanya mambo kulingana na masilahi?

Kwa hali yoyote iwayo ni kuwa wataalamu wengi wamechunguza tabia na kazi za wanyama, wadudu na ndege na wakafikia kwenye siri za ajabu zinazoshuhudia kuweko mpangaji mwenye hekima, Tutataja baadhi ya mifano.

Ndovu huweka mahakama kwa mhalifu na ndovu aliyekosea huhukumiwa kwa kutengwa na kundi la wengine ili aishi peke yake katika upweke.

Kunguru anapohisi hatari itakayowapata wenzake huwaonya kwa sauti maalum. Ama katika hali ya furaha hutoa sauti iliyo karibu na kicheko.

**Utauliza**: Kuna faida gani katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu kusema arukaye kwa mbawa zake ambapo kumtaja Ndege kunafahamisha moja kwa mja kuruka kwa mbawa?

**Jibu**: Hakuna faida, tuijuayo, isipokuwa ufasaha wa maneno.

Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote.

Imesemekana kuwa makusudio ya Kitab hapa ni lawhim-mahfudh (ubao maalum wenye kuhifadhiwa) wenye kukusanya yaliyokuwa na yatakayokuwa.

Kauli ya pili, inasema ni fumbo la ujuzi wa Mwenyezi Mungu kujua makusudio ya mtu, na kauli zake na vitendo vyake.

Kauli ya tatu, inasema ni Qur'an na kwamba Mwenyezi Mungu amebainisha ndani yake kila yapasayo kubainishiwa watu, miongoni mwa misingi ya dini na matawi yake na yanayofungamana nayo, Nasi tumeichagua kauli hii katika kufasiri Aya ya (2:2) Juz. 1, kifungu Qur'an na sayansi.

Kisha watakusanywa kwa Mola wao.

Dhahiri ya maneno inafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu atawakusanya wanyama na ndege siku ya Kiyama, kama atakavyowakusanya watu. Vilevile Aya isemayo: "Na wanyama mwitu watakapokusanywa." (82:5)

Maulama wengi wamesema hivyo kwa kutegemea Aya hizo mbili na Hadith isemayo**: "Hakika Mwenyezi Mungu atawachukulia kisasi watu kutokana na wenye pembe."**

Sisi tuko pamoja na Ibn Abbas aliyesema kuwa makusudio ya kukusanywa wanyama ni mauti yao; kama ilivyopokewa katika Hadith: "Anayepatwa na kifo ndiyo kiama chake." Kwa sababu hisabu na adhabu ni baada ya kukalifiwa na sharia na kuzihalifu. Wala hakuna kukalifiwa na sharia ila pamoja na akili; na wanyama na ndege hawana akili, kwa hiyo hawakalifiwi na sharia.

Kwa sababu hizo basi, hawatakusanya kwa ajili ya hisabu. Lau wanyama wangelichukuliwa hisabu basi ingefaa zaidi watoto wadogo wachukuliwe hisabu. Ama Hadith ya 'kuchukua kisasi', ni fumbo la uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kwamba yeye hataacha kidogo wala kikubwa ila atakidhibiti.

Ikiwa Mwenyezi Mungu atawaadhibu wenye pembe wakimpiga mtu, basi vizuri zaidi ni kutuharimishia sisi kuwachinja wanyama. Ama kauli ya anayesema kuwa Mwenyezi Mungu atayabadilisha maumivu ya mtu kwa mnyama, hiyo ni kumsemea Mwenyezi Mungu bila ya ujuzi wowote.

Na wale waliokadhibisha ishara zetu ni viziwi na mabubu wako gizani. Yaani wao ni kama viziwi, kwa sababu wao hawasikii mwito wa haki, na ni

kama mabubu kwa sababu wao hawaitamki haki waliyoijua na wako katika giza la kufuata na giza la ushirikina, ukafiri, ufasiki na dhambi.

Amtakaye Mwenyezi Mungu humpoteza na amtakaye humweka katika njia iliyonyooka.

Yametangulia maelezo kuhusu uongofu na upotevu katika Juz.1 (2:26) na Juz.2 (4:88).

﴿قُلْ أَرَأَيْتَكُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُ اللَّـهِ أَوْ أَتَتْكُمُ السَّاعَةُ أَغَيْرَ اللَّـهِ تَ دْعُونَ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ﴾

40. Sema: niambieni, kama ikiwafikia adhabu ya Mwenyezi Mungu au ikiwafikia ile saa, je, mtamuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni wakweli?

﴿بَلْ إِيَّاهُ تَدْعُونَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُونَ إِلَيْهِ إِن شَاءَ وَتَنسَوْنَ مَا تُشْرِكُونَ﴾

41. Bali yeye tu ndiye mtakayemuomba, Atawaondolea mnayomuomba akitaka, Na mtawasahau mnaowashirikisha.

﴿وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ فَأَخَذْنَاهُم بِالْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ لَعَلَّهُمْ يَتَضَرَّعُونَ﴾

42. Kwa hakika tulipeleka (Mitume) kwa umma zilizokuwa kabla yako; kisha tukawatia katika shida na madhara ili wapate kunyenyekea.

﴿فَلَوْلَا إِذْ جَاءَهُم بَأْسُنَا تَضَرَّعُوا وَلَـٰكِن قَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّ يْطَانُ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾

43. Basi mbona wasinyenyekee ilipowafikia adhabu yetu? Lakini nyoyo zao zilikuwa ngumu na shetani akawapambia waliyokuwa wakiyafanya.

﴿فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ أَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ حَتَّىٰ إِذَا فَرِحُوا بِمَا أُوتُوا أَخَذْنَاهُم بَغْتَةً فَإِذَا هُم مُّبْلِسُونَ﴾

44. Basi waliposahau yale waliyokumbushwa tuliwafungulia milango ya kila kitu, mpaka walipofurahia yale waliyopewa tuliwakamata kwa ghafla; na mara wakawa wenye kukata tamaa.

﴿فَقُطِعَ دَابِرُ الْقَوْمِ الَّذِينَ ظَلَمُوا وَالْحَمْدُ لِلَّـهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾

45. Ikakatwa mizizi ya watu waliodhulumu; na sifa njema ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote.

## SEMA NIAMBIENI

**Aya 40 - 45**

### MAANA

Sema: niambieni, kama ikiwafikia adhabu ya Mwenyezi Mungu au ikiwafikia ile Saa, je, mtamuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni wakweli?

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anamwamrisha Mtume wake awaambie washirikina: Niambieni kama ikiwafikia adhabu, kama ile iliyoteremshiwa wale waliokadhibisha Mitume yao; au yakiwafikia maumivu makubwa ya mauti na vitisho vya Kiyama, je katika hali hii, mtayaita masanamu na mizimu mliyokuwa mkiabudu na kudai kuwa itawaondolea fazaa na adhabu?

Makusudio ya Aya hii ni kuwa Makafiri kesho watajivua na yale waliyokuwa wakiyaabudu na kukimbilia kwa Mwenyezi Mungu baada ya kuwabainikia kuwa hakuna hila wala nguvu ila kwa msaada wake Yeye tu peke yake bila ya kuwa na mshirika.

## MWENYEZI MUNGU NA MAUMBILE

Bali yeye tu ndiye mtakayemuomba.

Baada ya kuwauliza kuwa mtamwomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu siku ya vituko vikubwa, amelithibithisha jibu kwa kusema kwake: (Bali yeye tu ndiye mtakayemuomba).

Hilo ndilo jibu linaloaminiwa na kujibiwa na umbile ambalo Mwenyezi Mungu amewaumbia watu, katika dunia na akhera, Na sio maana ya umbile la Mwenyezi Mungu kuwa mtu atamtambua Muumba hivi hivi tu bila ya dalili. Hapana! Kama ni hivo basi kusingelitokea mtu yeyote wa kumkanusha Mwenyezi Mungu.

Hakika maana ya umbile hili ni kuwa Mwenyezi Mungu amempa mtu maandalizi ya kufahamu dalili zinazofahamisha kuweko Mwenyezi Mungu, na dalili hizi haepukani nazo kwa hali yoyote. Anayekufuru anakufuru kwa kuzembea na kupuuza kwa kuepuka kuchunguza dalili na hoja. Kwa hiyo ndipo akastahiki adhabu kwa kupuuza huko.

Kwani hakuna tofauti kabisa katika mtazamo wa akili, baina ya mwenye kuacha kufanya amali, kwa makusudi, na huku anajua; na yule mwenye kuiacha haki akafuta batili kwa kutojua lakini ana uwezo wa kujua na kupambanua uongufu na upotevu, lakini akaacha kwa kupuuza na kudharau.

Inawezekana maandalizi hayo yakajificha nyuma ya pazia la kufuata maelezo na matamanio; sawa na linavyojificha jua nyuma ya mawingu, ikafikiriwa kwa yule asiyejua sitara hizo kuwa yeye amemkana Mwenyezi Mungu kwa kukosa dalili na dalili iko katika dhati yake na maumbile yale ambayo amemuumbia Mwenyezi Mungu. Na siku ya Kiyama sitara hii iliyozuka itaondoka na kudhihiri hakika iliyo wazi wala hakutasalia nafasi ya shaka na ukanusho.

Atawaondolea mnayomuomba akitaka.

Yaani nyinyi washirikina mtaacha siku ya Kiyama, kuomba masanamu mliyokuwa mkiyaabudu duniani na mtamwomba Mwenyezi Mungu peke yake, wakati hakika ya kila jambo itakapodhihiri.

Na mtawasahau mnaowashirikisha.

Yaani nyinyi washirikina siku ya Kiyama mtaacha kuyaomba masanamu mliyokuwa mkiyaabudu duniani na kumwomba Mwenyezi Mungu peke yake wakati itakapodhihiri hakika ya kila kitu.

Kwa hakika tulipeleka (Mitume) kwa umma zilizokuwa kabla yako; kisha tukawatia katika shida na madhara ili wapate kunyenyekea.

Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) hawaadhibu waja wake ila baada ya kuwapelekea mjumbe atakayewaongoza kwenye njia ya uongofu. Kama hawakuongoka anawapa fursa ili wajirudi wenyewe, na kuwatia katika mtihani kwa mabalaa ili wanyenyekee na watubie, lakini wao waling'ang'ania maasi; kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aya inayofuatia hii.

Basi mbona wasinyenyekee ilipowafikia adhabu yetu? Lakini nyoyo zao zilikuwa ngumu na shetani akawapambia waliyokuwa wakiyafanya.

Mwenyezi Mungu, ambaye zimetukuka sifa zake, anasema kuwa wao hawakunyenyekea ilipowafikia shida duniani wala hawakumdhalilikia Mwenyezi Mungu kwa kuacha inadi yao, bali waling'ang'ania ukafiri, na shetani akawa nyuma yao akiwapambia upotevu na ufisadi.

Aya hii inafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) anamkubali kila anayekimbilia kwake, hata kama kukimbia kwake ni kwa vikwazo vya shida na balaa. Hivi ndivyo alivyo aliye mkarimu na adhimu. Hamnyimi mwenye kuomba wala hamkatishi tamaa, kwa namna yoyote lengo na msukumo wake utakavyokuwa.

Basi waliposahau yale waliyokumbushwa tuliwafungulia milango ya kila kitu mpaka walipofurahia yale waliyopewa tuliwakamata kwa ghafla; na mara wakawa wenye kukata tamaa.

Aliwaonya kwanza kwa kauli kupitia kwa Mitume. Pili, kwa vitendo alipowapa mtihani kwa shida na madhara.

Waliponga'ang'ania ukafiri na inadi aliwafungulia milango ya riziki na raha, ili kuwasimamishia hoja na kuwavuta kidogo kidogo kwa neema baada ya mtihani wa nakama.

Walipofurahia raha na kuzidi kiburi na wala wasielekee kwenye uongofu, basi Mwenyezi Mungu aliwaadhibu kwa namna wasiyofikiria, wakajuta kwa kuzembea na wakakata tamaa ya kuokoka.

Kwa ufupi ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) mara nyingine aliwapa dhiki na mara nyingine furaha kwa kupenda waongoke; sawa na afanyavyo mzazi kumhurumia mwanawe akitaka atengenekewe.

Lakini wala hawakushukuru raha wala kuwaidhika na balaa. Wakang'olewa wote asibakie yeyote katika wao, ili wapate funzo watakaokuja baada yao.

Ikakatwa mizizi ya watu waliodhulumu; na sifa njema ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote.

Kwa sababu ya kuwaneemesha kwake waumin na kuwanusuru na watu wa kufuru na ufisadi.

9

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَخَذَ اللَّـهُ سَمْعَكُمْ وَأَبْصَارَكُمْ وَخَتَمَ عَلَىٰ قُلُوبِكُم مَّنْ إِلَـٰهٌ غَيْرُ اللَّـهِ يَأْتِيكُم بِهِ انظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ ثُمَّ هُمْ يَصْدِفُونَ﴾

46. Sema: Mwaonaje kama Mwenyezi Mungu akichukua kusikia kwenu na kuona kwenu na akaziziba nyoyo zenu, ni nani Mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu awezaye kuwaletea tena? Tazama jinsi tunavyozikariri ishara, kisha wao wanapuuza.

﴿قُلْ أَرَأَيْتَكُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُ اللَّـهِ بَغْتَةً أَوْ جَهْرَةً هَلْ يُهْلَكُ إِلَّا الْقَوْمُ الظَّالِمُونَ﴾

47. Sema: Mwaonaje ikiwafikia adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa ghafla au kwa dhahiri nani wataangamizwa isipokuwa watu waliodhulumu?

﴿وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ فَمَنْ آمَنَ وَأَصْلَحَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ﴾

48. Na hatutumi Mitume ila niwabashiri na waonyaji. Na wenye kuamini na wakafanya wema, basi haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika. 49. Na wale waliokadhibisha ishara zetu itawagusa adhabu kwa sababu ya walivyokuwa mafasiki.

## AKICHUKUA MWENYEZI MUNGU KUSIKIA NA KUONA

**Aya 46-49**

### MAANA

Sema: Mwaonaje kama Mwenyezi Mungu akichukuwa kusikia kwenu na kuona kwenu na akaziziba nyoyo zenu, ni nani Mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu awezaye kuwaletea tena?

Mtu ni usikizi, uoni na moyo. Lau haya yanamwondokea, basi hatakuwa ni chochote, mnyama atakuwa ni bora kuliko yeye. Hakuna mwenye shaka kwamba Mwenyezi Mungu anaweza kuvichukua hivyo, kwa sababu Yeye ndiye aliyeviumba.

Makusudio ya ishara hii ni kuwakumbusha Mwenyezi Mungu Makafiri kuwa wanaowafanya waungu asiyekuwa yeye hawatawakinga na madhara wala hawatawaletea manufaa:

﴿وَإِذَا أَرَادَ اللَّـهُ بِقَوْمٍ سُوءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُ﴾

"Na Mwenyezi Mungu anapowatakia watu adhabu hakuna cha kuzuia" (13:11)

Tazama jinsi tunavyozikariri ishara, kisha wao wanapuuza.

Yaani tumesimamisha hoja juu yao zinazofuatiwa na hoja kwa mifumo mbali mbali, ili wawaidhike na wazingatie. Tukawaondolea nyudhuru zote ili waamini. Lakini dalili hizo mkato hazikuwadishia ila kuendelea na ukafiri, dhuluma na inadi.

Sema: Mwaonaje ikiwafikia adhabu ya Mwenyezi Mungu kwa ghafla au kwa dhahiri nani wataangamizwa isipokuwa watu waliodhulumu?

Mara ya pili anawapa mawaidha na kuwatishia kuwaletea adhabu ambayo hawataweza kuikinga; ni sawa ingewajia ghafla kwa namna wasiyoijua au kwa wazi wazi kwa namna ya kuwa tayari nayo. Mara hii katika Aya hii anawaonya Mwenyezi Mungu na kuwapa onyo ili waiogope adhabu kabla ya kutukia kwake, na waelekee kwenye uongofu wao, lakini nyoyo zao zikasusuwaa na wala wasipondokee kwenye haki na uongofu.

Na hatutumi Mitume ila na waonyaji.

Hii ndiyo kazi ya Mtume, anawapa bishara watiifu na kuwaonya waasi. Kazi hii, pamoja na urahisi wa ufafanuzi wake na kueleweka kwake, lakini ndiyo kazi yenye mashaka makubwa na nzito. Kwa sababu inagusa maisha ya mataghuti moja kwa moja, na kuyaingilia masilahi yao na manufaa yao.

Mwishilio wa kazi ya Mtume ni kulipwa wema mwenye kuamini na kufanya matendo mema, na kuadhibiwa mwenye kukufuru na kuzikadhibisha ishara za Mwenyezi Mungu.

Na wenye kuamini na wakafanya wema, basi haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

Kwa sababu mwenye makosa ndiye anayehofia na kuhuzunika. Ama asiye na hatia huwa katika amani na utuvu.

Na wale waliokadhibisha ishara zetu itawagusa adhabu kwa sababu ya walivyokuwa mafasiki.

Ufasiki ni zaidi ya ukafiri. Kila kafiri ni fasiki, sio kila fasiki ni kafiri. Makusudio ya ufasiki hapa ni ukafiri, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: Waliokadhibisha ishara zetu.

﴿قُل لَّا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي خَزَائِنُ اللَّـهِ وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِنِّي مَلَكٌ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ أَفَلَا تَتَفَكَّرُونَ﴾

50. Sema: Siwaambii kuwa ninazo hazina za Mwenyezi Mungu, wala sijui ghaibu; wala siwambii mimi ni Malaika; sifuati ila ninayopewa Wahyi. Sema: Je, kipofu na mwenye kuona wako sawa? Je, hamfikiri?

﴿وَأَنذِرْ بِهِ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَن يُحْشَرُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ لَيْسَ لَهُم مِّن دُونِهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ لَّعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ﴾

51. Na waonye kwayo wale wanaoogopa kwamba watakusanywa kwa Mola wao. Hawana mlinzi wala mwombezi isipokuwa yeye ili wapate kuwa na takua.

﴿وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُم بِالْغَدَاةِ وَ الْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ مَا عَلَيْكَ مِنْ حِسَابِهِم مِّن شَيْءٍ وَمَا مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِم مِّن شَيْءٍ فَتَطْرُدَهُ مْ فَتَكُونَ مِنَ الظَّالِمِينَ﴾

52. Wala usiwafukuze wale wanaomwomba Mola wao asubuhi na jioni kwa kutaka radhi yake; si juu yako hisabu yao hata kidogo, wala hisabu yako si juu yao hata kidogo, kwamba uwafukuze na uwe miongoni mwa madhalimu.

﴿وَكَذَٰلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لِّيَقُولُوا أَهَـٰؤُلَاءِ مَنَّ ال لَّـهُ عَلَيْهِم مِّن بَيْنِنَا أَلَيْسَ اللَّـهُ بِأَعْلَمَ بِالشَّاكِرِينَ﴾

53. Na namna hii tumewajaribu wao kwa wao ili waseme: Je, hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewafadhili miongoni mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu hawajui wanaoshukuru?

﴿وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ أَنَّهُ مَنْ عَمِلَ مِنكُمْ سُوءًا بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابَ مِن بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

54. Na wanapokufikia wale wanaoamini ishara zetu waambie: Amani iwe juu yenu (Assalam alaykum), Mola wenu amejilazimisha rehema. Ya kwamba atakayefanya miongoni mwenu uovu kwa ujinga, kisha akatubu baada yake na akatengenea. Basi yeye ndiye mwingi wa maghufira mwenye kurehemu.

﴿وَكَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ وَلِتَسْتَبِينَ سَبِيلُ الْمُجْرِمِينَ﴾

55. Namna hii tunazieleza ishara na ili njia ya wakosefu ibainike.

## SIFUATI ILA NINAYOPEWAWAHYI

**Aya 50 -55**

### MAANA

Sema: Siwaambii kuwa ninazo hazina za Mwenyezi Mungu, wala sijui ghaibui, wala siwambii mimi ni Malaika; sifuati ila ninayopewa Wahyi.

Washirikina walimtaka Mtume **(s.a.w.w)** awaambie mambo ya siri, awatolee chemchem, awaletee Malaika, apande mbinguni na awaangushie hiyo mbingu na mengineyo ambayo hayana uhusiano wowote na Utume. Ndipo akateremsha Mwenyezi Mungu Aya hii na akamwamrisha Mtume kuwaambia, kuwa yeye si Mungu wala Malaika; isipokuwa yeye ni mtu anayepewa wahyi tu.

Kwa maneno mengine ni kuwa Mungu ana sifa zinazomhusu yeye tu; kama vile kuwa ni muweza wa kila kitu, mwenye kujua kila kitu. Vilevile Malaika ana sifa zinazomhusu; kama vile kupanda mbinguni na kuwa yeye hali wala hatembei sokoni. Ama Mtume ni mtu kama watu wengine; tofauti ni kuwa yeye analetewa wahyi tu kutoka kwa Mola wake, akimpa bishara ya malipo mazuri yule atakayemwitikia, na kumuonya kwa adhabu yule atakayempa kisogo.

Wala si mambo yanayohusu Utume, kutoa habari za siri na kuleta mambo yasiyokuwa ya kawaida. Kwa hiyo kuchanganya sifa za Malaika na Mitume yake ni ujinga na upofu.

Sema: Je, kipofu na mwenye kuona wako sawa?

Tofauti ilioje baina ya mjinga mpotevu ambaye hatofautishi baina ya sifa za Mwenyezi Mungu na sifa za Mtume, na yule anayefahamu kuwa Mtume ni mtu aliye na yale waliyo nayo watu wengine, isipokuwa yeye anapewa wahyi.

Je, hamfikiri? Kuwa Mtume siye Mungu wala Malaika na kwamba yeye ni mtoaji bishara na muonyaji, ili mzifanyie haki nafsi zenu na muamini Lailaha ila Ilah Muhammadur rasulullah? (Hakuna mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu)

Na waonye kwayo wale wanaoogopa kwamba watakusanywa kwa Mola wao.

Dhamir katika kwayo inarudia Qur'an, iliyotanguliwa kuashiriwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Sifuati ila ninayopewa Wahyi."

Wametofautiana wafasiri kuhusu wanaoogopa kukusanywa kwa Mola wao kuwa je ni waumini au makafiri, kwa kuangalia kuwa baadhi yao walikuwa wakiathirika kuhofishwa na Mtume na maonyo yake; kama ilivyoelezwa katika Tafsir ya Razi?

Tuonavyo ni kuwa baada ya Mtume **(s.a.w.w)** kuwaonya watu kwa hoja zinazowasimamia, Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha, katika Aya hii, kuendelea na kufuatishia kuwaonya waumini kwa Qur'an ili wazidi imani, na waijue dini na hukumu zake.

Vilevile kuwaonya wasiokuwa waumini katika wale ambao kuna matarajio ya kuongoka kwao kwa kufuatisha kuonya na kukaririka.

Hawana mlinzi wala mwombezi isipokuwa yeye ili wapate kuwa na takua.

Yaani wakati unapowaonya wanakusikiliza na kunufaika na unavyowaonya na kujua kuwa hawana mlinzi wa kuwanusuru isipokuwa Mwenyezi Mungu, wala mwombezi yeyote atakayeombea mbele yake ila kwa idhini yake.

Wala usiwafukuze wale wanaomwomba Mola wao asubuhi na jioni kwa kutaka radhi yake; si juu yako hisabu yao hata kidogo, wala hisTafsir abu yako si juu yao hata kidogo, kwamba uwafukuze na uwe miongoni mwa madhalimu.

Asubuhi na jioni ni fumbo la kuendelea kumtaja kwao Mwenyezi Mungu na kumwabudu; kama kusema "Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu asubuhi na jioni."

Dhamiri ya Hisabu yao na juu yao inawarudia waumini wanaomwomba Mola wao. Maana ya si juu yako hisabu yao ni kuwa hisabu yao na hisabu ya wengineo, haihusiani na Utume wala si katika mambo yake. Hisabu yao iko kwa Mwenyezi Mungu tu peke Yake; sawa na ilivyo hisabu yako ewe Muhammad.

Mwislamu, kwa hakika, anaamini moja kwa moja kwamba Muhammad **(s.a.w.w)** ni Mtukufu wa viumbe vyote na wakati huo anaamini kuwa utukufu wa Muhammad haumwezeshi kumhisabu yeyote au kumwadhibu au kumpa thawabu. Hakika hisabu na malipo ni ya Mwenyezi Mungu na yanatokana na Mwenyezi Mungu pekee bila ya kuwa na mshirika.

Kwa fadhila hii ndipo Uislamu ukatofautiana na dini zote kwa kukanusha uwezo wa mtu kwa mtu mwingine vyovyote atakavyokuwa. Na kwa hali hiyo tunajifaharisha na kujitukuza kuliko Wajamaa, Wakomunisti, Mabepari, Wademokrasia na watu wa dini zote na madhehebu yote.

Wafasiri wametaja sababu za kushuka Aya hii, kuwa mamwinyi wa Kikuraish walimpitia Mtume **(s.a.w.w)** akiwa na Ammar bin Yasir, Khabbab, Bilal na wengine katika Waislamu wa hali ya chini, wakasema: "Ewe Muhammad umewaridhia hawa? Unataka tuwe pamoja na hawa? Hebu waondoe tuwe sisi tu peke yetu na wewe; kisha tukimaliza warudishe ukae nao ukitaka" Imesemekana kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alitaka kuwakubalia, ndipo ikashuka Aya.

Dhahiri ya maneno hapa haiikatai hilo hasa kauli yake Mwenyezi Mungu: "Kwamba usiwafukuze na uwe miongoni mwa madhalimu." Kwa

kuwadhulumu hao, ambao ni bora hasa kukaa nao na wapate faida kutoka kwako.

Kwa maneno mengine ni kwamba Mtume alitaka kuwakaribisha matajiri, ili afaidike nao, ndipo Mwenyezi Mungu akamwambia mafukara ni bora kufaidika nao, Ukiacha ubora huu, basi umewadhulumu mafukara waumini katika kufaidika.

**Utauliza**: Je, kuacha lililo bora hakupingani na Isma?

**Jibu**: Kuacha lililo bora zaidi kunajuzu na wala si haramu, mpaka kupingane na Isma. Zaidi ya hayo ni kwamba Mtume hakujaribu kuwafukuza mafukara kwa kuwadharau kutokana na ufukara wao, bali ni kwa kupupia na kuwa na tamaa ya kusilimu viongozi. Ndipo Mwenyezi Mungu (s.w.t) akamfahamisha kuwa Uislamu hauna haja na hawa wenye kutakabari mataghuti; na kwamba iko siku watakuja silimu wakiwa madhalili walio chini; kama ilivyotokea baadaye.

Na namna hii tumewajaribu wao kwa wao ili waseme: Je, hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewafadhili miongoni mwetu?

Kujaribu Mwenyezi Mungu mja wake ni kumdhihirisha kwa watu hakika yake kwa njia ya vitendo vyake na kauli zake; kama tulivyofafanua katika kufasiri Juz hii (5:94)

Maana ni kuwa tumewajaribu matajiri kwa mafakiri, ili wamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwaneemesha, lakini hilo likawapeleka kuwa na kiburi na kujitukuza. Imam Ali (a.s) anasema: **"Msizingatie mapenzi na chuki kwa mali na watoto tu, mkasahau fitina na mtihani katika utajiri"** Amekwisha sema Mwenyezi Mungu (s.w.t):

﴿أَيَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِ مِن مَّالٍ وَبَنِينَ ﴿٥٥﴾ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ بَل لَّا يَشْعُرُونَ﴾

"Je, wanafikiri kuwa yale tunayowapa mali na watoto ndio tunawaharakishia katika heri? Bali hawatambui" (23: 55)

Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) anawajaribu waja wake wenye kutakabari katika nafsi zao kwa mawalii wake wanyonge machoni mwao. Musa bin Imran na nduguye Harun waliingia kwa Firaun wakiwa na majuba ya sufi na mikononi wameshikila fimbo.

Wakampa sharti la kusilimu ikiwa anataka ufalme wake na cheo chake kibakie. Akasema: Hamwoni ajabu eti hawa wananipa masharti yakubakia ufalme na cheo na wao wenyewe mnawaona walivyo na hali ya ufukara na udhalili?"

### ASSALAMU ALAYKUM WA RAHMATULLAH

Na wanapokufikia wale wanaoamini ishara zetu waambie: Amani iwe juu yenu (Assalam alaykum), Mola wenu amejilazimisha rehema. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "Mola wangu amenifundisha adabu, akaifanya nzuri adabu yangu." Ni adabu gani iliyo kama adabu ya Muumbaji wa mbingu na ardhi. Ni nafsi gani inayokuwa na kuleta matunda ya mafundisho ya Mwenyezi Mungu kuliko nafsi ya Muhammad?

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameifundisha nafsi hii njema na takatifu, ili kuiandaa na risala yake, risala ya rehema kwa viumbe ambayo kwayo na kwa mwenye nayo, zimetimia tabia njema.

Mwenyezi Mungu amemfundisha adabu Muhammad katika Aya kadhaa; ikiwemo Aya hii tuliyo nayo, ambayo inafundisha Mtume wa Mwenyezi

Mungu na bora ya viumbe vya Mwenyezi Mungu, namna ya kufuatana na kuamiliana na wanyonge masikini.

Alikuwa akiwakabili kwa bashasha na makaribisho na kuwambia: Assalamu alykum (Amani iwe juu yenu), Mola wenu amejilazimisha rehema, Na alikuwa akiifunga nafsi yake kukaa nao maadamu wako mpaka waondoke wao.

Ikiwa Mtume ndiye aliyekusudiwa na Mwenyezi Mungu kwa mafunzo haya, basi sisi ndio tuliokusudiwa kufuata nyayo zake. Usimtukuze yeyote kwa mali au jaha au jinsi na rangi. Isipokuwa tumheshimu na kumtukuza kwa dini na tabia nzuri.

Baadhi ya wafasiri wapya wanasema: "Maisha ya watu kabla ya Muhammad **(s.a.w.w)** yalikuwa chini yenye kuwayawaya na Muhammad akayapandisha juu hadi kileleni; na hivi sasa yameondoka kwenye kilele kirefu na kuanguka huko New York, Washington na Chicago kwenye ubaguzi wa rangi."

Ndio! katika Usilam hakuna jinsia, rangi, jaha wala utajiri. Hakuna ubora katika Uislamu ila kwa takua. Kwa misingi hii ndipo inapopatikana siri ya kunyenyekea kwa wanavyuoni wa Kiislamu wanaofuatwa katika fatwa zao (marjaa). Mdogo na mkubwa anaweza kumfikia kwa njia ya usawa tu, bila ya kuweko bawabu au kizuizi na wanazungumza naye vile wanavyotaka na bila ya taklifu.

Ama baba mtakatifu (Papa) na wengineo katika viongozi wa dini, hakuna anayeota kukaa naye na kuzungumza naye ila waziri na wakubwa, tena amwekee wakati maalum na muda atakaozungumza naye.

Turudie kwenye kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Na wanapokufikia wale wanaoamini ishara zetu waambie: Assalamu alaykum (Amani iwe juu yenu), Mola wenu amejilazimisha rehema.'

Assalamu alaykum warahmatullah, (Amani na rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu).

Haya ndiyo maamkuzi ya Kiislam, kumwombea unayemwamkua kuokoka na kila maovu na aishi kwa amani na utulivu na kwa rehema ya Mwenyezi Mungu na radhi zake, Kwani hakuna amani wala kuokoka ikiwa kuna ghadhabu yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ama ukiongozea Wa barakatuh (na baraka zake), utakuwa umemwombea mwenzako riziki pana.

Wapi na wapi maamkuzi ya marahaba, sabalkher na 'good night' na maamkuzi haya ya Mungu ya Kiislamu? Imetangulia kauli yake Mwenyezi Mungu; amejilazimisha rehema katika Aya 12 ya Sura hii. Na tukaeleza katika Tafsir yake kuwa rehema yake Mwenyezi Mungu Mtukufu haiepukani na dhati yake tukufu, sawa na uweza Wake na elimu Yake.

Ya kwamba atakayefanya miongoni mwenu uovu kwa ujinga, kisha akatubu baada yake na akatengenea.

Kuhusu toba, tumeweka mlango mahsusi kwa anuani ya toba na maumbile, katika kufasiri Juz.4 (4:18).

Basi yeye ndiye mwingi wa maghufira mwenye kurehemu.

Huyu ndiye Mola tunayemwabudu, husamehe mwenye kutubia na hurehemu waja. Kila mwenye kuwahurumia watu na akafanya kazi kwa ajili ya utengenevu wao, basi atakuwa amemwabudu Mwenyezi Mungu katika matendo yake; hata kama atapinga kwa ulimi wake. Na kila mwenye

kuwaingilia watu katika haki zao, basi atakuwa amemkufuru Mwenyezi Mungu kivitendo, hata kama ataleta takbira na tahlili.

Namna hii tunazieleza ishara na ili njia ya wakosefu ibainike.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja katika Kitab chake sifa za watu wema, Vilevile ametaja sifa za wenye makosa ili lidhihirike kila kundi na alama yake. Zaidi ya hayo ni kwamba kujua moja ya vikundi viwili husababisha kujua kundi jingine; sawa na uongofu na upotevu.

﴿قُلْ إِنِّي نُهِيتُ أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ ۚ قُل لَّا أَتَّبِعُ أَهْوَاءَكُمْ ۙ قَدْ ضَلَلْتُ إِذًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُهْتَدِينَ﴾

56. Sema: Nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu. Sema: Sifuati hawaa zenu, maana hapo nitapotea na sitakuwa miongoni mwa walioongoka. Sema: Nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameashiria njia ya wenye makosa, Katika Aya hii anaibainisha njia hiyo; kumwabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

﴿قُلْ إِنِّي عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي وَكَذَّبْتُم بِهِ ۚ مَا عِندِي مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ ۚ إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّـهِ ۖ يَقُصُّ الْحَقَّ ۖ وَهُوَ خَيْرُ الْفَاصِلِينَ﴾

57. Sema: Hakika mimi ninayo dalili wazi itokayo kwa Mola wangu, nanyi mmeikadhibisha. Mimi sina haraka kwa mnayoyataka. Hapana hukmu ila ya Mwenyezi Mungu. Anasimulia yaliyo kweli; naye ni mbora wa wanaohukumu.

﴿قُل لَّوْ أَنَّ عِندِي مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ لَقُضِيَ الْأَمْرُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ وَاللَّـهُ أَعْلَمُ بِالظَّالِمِينَ﴾

58. Sema: Lau ningelikuwa nayo mnayotaka haraka, basi shauri lingekwisha baina yangu. na baina yenu Na Mwenyezi Mungu anawajua zaidi madhalimu.

## SIFUATI HAWAA ZENU

**Aya 56-58**

### MAANA

Sema: Nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu.

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameashiria njia ya wenye makosa. Katika Aya hii anaibainisha njia hiyo; kumwabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu.

Sema: Sifuati hawaa zenu, maana hapo nitapotea na sitakuwa miongoni mwa walioongoka.

Kwa sababu kuomba kwao hakuna asili yoyote ila hawaa na upotevu, sasa vipi atafuata Mtume Mtukufu?

Sema: Hakika mimi ninayo dalili wazi itokayo kwa Mola wangu, nanyi mmeikadhibisha.

Yaani ninamwabudu Mwenyezi Mungu kwa ujuzi na nyinyi mnamkanusha; na mnaabudu masanamu kwa ujinga, Kwa mantiki gani mjuzi amfuate mjinga? Na mwenye batili amwongoze mwenye haki?

Sina haraka kwa mnayoyataka.

Mtume alipowatolea mwito wa kuamini walisema: "Tuletee mvua ya mawe kutoka mbinguni au tuletee adhabu kali."

Ndipo Mwenyezi Mungu akamwamrisha aseme: Sina haraka. Bali yako kwa Mwenyezi Mungu anaiteremsha wakati anaotaka wala mimi sina uwezo wa kuitanguliza au kuichelewesha.

Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu katika kuteremsha adhabu na kuitanguliza au kuiahirisha.

Anasimulia yaliyo kweli.

Yaani anasema kweli: Naye ni mbora wa wanaohukumu, hadhulumu yeyote katika hukumu yake.

Sema: Lau ningelikuwa nayo mnayotaka haraka katika adhabu, basi shauri lingekwisha baina yangu na baina yenu kwa kuangamizwa mwenye kudhulumu katika nyinyi

Na Mwenyezi Mungu anawajua zaidi madhalimu.

Huharakisha au kuchelewesha adhabu kulingana na vile inavyopitisha hekima yake.

10

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿وَعِندَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَمَا تَسْقُطُ مِن وَرَقَةٍ إِلَّا
يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴾

59. Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye; anajua kilichomo nchi kavu na kilichomo baharini; na halianguki jani ila analijua wala punje katika giza la ardhi; wala kibichi au kikavu, ila kimo katika Kitab kinachobainisha.

﴿وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّاكُم بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُم بِالنَّهَارِ ثُمَّ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لِيُقْضَىٰ أَجَلٌ مُّسَمًّى
ثُمَّ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ ثُمَّ يُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴾

60. Naye ndiye anayewafisha usiku. Na anakijua mlichokifanya mchana kisha huwafufua humo ili muda umalizike, Kisha kwake yeye ndiyo marejeo kwenu; kisha awaambiye mliyokuwa mkiyafanya.

﴿وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ حَفَظَةً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ رُسُلُنَا
وَهُمْ لَا يُفَرِّطُونَ﴾

61. Naye ndiye mwenye nguvu za kushinda juu ya waja wake, Na huwapelekea waangalizi, Hata mmoja wenu yakimjia mauti wajumbe wetu humfisha nao hawazembei.

﴿ثُمَّ رُدُّوا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ أَلَا لَهُ الْحُكْمُ وَهُوَ أَسْرَعُ الْحَاسِبِينَ﴾

62. Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa haki. Hakika hukumu ni yake, naye ni mwepesi kuliko wote wanaohisabu.

## HAZINA YA SIRI IKO KWAKE

**Aya 59-62**

### MAANA

Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna aijuaye ila Yeye; anajua kilicho nchi kavu na kilicho baharini; na halianguki jani ila analijua wala punje katika giza la ardhi; wala kibichi au kikavu, ila kimo katika Kitab kidhihirishacho.

Yaani Mwenyezi Mungu anajua ulimwengu, yaliyotokea na yatakayotokea yote, ya kimada au ya kimaana. Ujuzi wake haufungiki na wakati, mahali au kuwa katika hali fulani kinyume na hali nyingine. Kwa sababu ujuzi wake ni wa kidhati si wa kuchuma; na dhati yake si ya wakati na mahali; wala haibadiliki kwa kubadilika matukio na hali.

Katika Hadith imeelezwa: **"Hakika hazina za siri ni tano"** Na Qura'n inasema:

﴿إِنَّ اللَّهَ عِندَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَيُنَزِّلُ الْغَيْثَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّاذَا
تَكْسِبُ غَدًا وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تَمُوتُ ﴾

"Hakika ujuzi wa Saa (Kiyama) uko kwa Mwenyezi Mungu. Naye huteremsha mvua, na anayajua yaliyo katika matumbo ya uzazi; na nafsi

yoyote haijui itachuma nini kesho na nafsi yoyote haijui itafia nchi gani. (31:34)

Mwanafalsafa, Mulla Sadra anasema: "Vitu vyote vizima (kamili) au mafungu vinatiririka kutokana naye, naye ni msingi wa kila kilichopo, kiakili au kihisia na kwa kuwaza au kwa kuona. Na mtiririko wake kutokana naye hauepukani kuwa wazi mbele yake."

Allama Hilli anasema: "Kila kilichopo kisichokuwa Mwenyezi Mungu ni chenye kuwezekana, chenye kutegemezwa kwake. Atakuwa ni mwenye kukijua, ni sawa kiwe chote au baadhi; na ni sawa kiwe ni chenye kusimama hicho chenyewe au kwa kutegemea kingine, na ni sawa kiwe kiko machoni au mawazoni.

Kwa sababu kupatikana picha katika mawazo ni katika mambo yenye kuwa vilevile; kwa hiyo yanamtegemea Yeye. Na ni sawa picha hiyo ya mawazo iwe ni jambo lilioko au lisilokuwapo, linalowezekana au lisilowezekana. Ujuzi wake hauepukani na kitu chochote kiwezekanacho na kisichowezekana."

Naye ndiye anayewafisha usiku.

Kufa na mauti ni maneno mawili yenye maana moja katika kawaida ya ufahamu, nako ni kukosa uhai. Matamko yote mawili hutumiwa katika usingizi kimajazi. Kwa vile viungo hupumzika kufanya kazi kwa sababu ya usingizi. Na katika maana hayo ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿اللَّـهُ يَتَوَفَّى الْأَنفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ تَمُتْ فِي مَنَامِهَا  فَيُمْسِكُ الَّتِي قَضَىٰ عَلَيْهَا الْمَوْتَ وَيُرْسِلُ الْأُخْرَىٰ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى﴾

"Mwenyezi Mungu huziua roho wakati wa mauti yake na zile ambazo hazijafikiwa na mauti katika usingizi. Basi huzizuia zile alizozipitishia mauti, na huzirudisha zile nyingine mpaka wakati uliowekwa" (39:42)

Yaani Mwenyezi Mungu anakata mawasiliano ya roho na mwili, kwa dhahiri na kwa hali halisi, wakati wa kufa na kuzizuia kwake. Uhusiano huu anaukata kwa dhahir, sio kwa hali halisi, wakati wa kulala; na wakati wa kuamka uhusiano huu unarudia kama ulivyokuwa na kubaki hadi wakati uliowekewa kufa kikweli. Kwa hiyo mwenye kulala ni maiti hai.

Makusudio ya kufa katika Aya hii ni mauti ya kimajazi. Imam Ali (a.s) anasema: **"Roho ya mtu hutoka wakati wa kulala na kubaki miale yake mwilini, Kwa miale anaota ndoto. Akizinduka roho hurudi mara moja"**

Na anayajua mlichokifanya mchana kisha huwafufua humo.

Humo ni mchana; na maana ya kuwafufua ni kuwaamsha usingizini. Wafasiri wamesema kuwa maneno haya ni dalili ya ufufuo na Kiyama. Kwa sababu usingizi unafanana na mauti, na kuamka kunafanana na kufufuka baada ya mauti.

Kisha kwake yeye ndiyo marejeo yenu; kisha awaambiye mliyokuwa mkiyafanya ya kheri na ya shari, katika usiku na mchana.

Kwa ufupi ni kwamba kila mtu anakufa kwa kwisha siku zake zilizoandikwa, kisha Mwenyezi Mungu atamfufua baada ya mauti, sawa na anavyomwamsha usingizini; kisha ailipe kila nafsi ilichokichuma na wao hawatadhulumiwa.

Ikiwa mtu atasema: Kwa nini Aya imehusisha kulala usiku na kufanya kazi mchana ambapo mtu mara nyingine hulala mchana na akafanya kazi usiku?

Tutamwambia Aya imekuja katika hali iliyo aghlab.

Naye ndiye mwenye nguvu za kushinda juu ya waja wake.

Inatosha kuwa amewazidi nguvu kwa vile wanadamu wanakuja katika maisha haya kwa nguvu na wanayaacha kwa nguvu. Imam Ali (a.s) anasema: **"Hakuna chochote isipokuwa mmoja mwenye kushinda nguvu ambae kwake ni marejeo ya mambo yote yaliyoanza umbile lake bila ya kujiweza na yatakayokwisha bila ya kujizuia."**

Na huwapelekea waangalizi.

Watunzaji hao ni Malaika. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

﴿وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَافِظِينَ ﴿١٠﴾ كِرَامًا كَاتِبِينَ ﴿١١﴾ يَعْلَمُونَ مَا تَفْعَلُونَ﴾

"Na hakika mna waangalizi, Watukufu wenye kuandika, Wanajua mnayoyatenda" (82:10-12)

Nasi tunaamini hayo, kwani Wahyi umeyaelezea na akili haiyakatai. Katika maneno ya Mwenyezi Mungu au ya Mtume haukuja ubainifu wa sifa za hao waandishi na maandishi; na akili hailazimishwi kufanya utafiti na kuuliza. Kwa hiyo tunayaacha katika ujuzi wake Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ama kufananisha waandishi na polisi wa siri; kama ilivyo katika Tafsir Almanar na Maraghi, ni kama kufananisha ghaibu na yanayoonekana na kufananisha mbingu na ardhi ambazo zina tofauti kubwa.

Hata mmoja wenu yakimjia na mauti, wajumbe wetu humfisha nao hawazembei.

Utapata Tafsir yake katika Sura (32:11) Inshallah, Hayo vilevile ni katika mambo ya ghaibu yanayowezekana kiakili na yaliyothibiti Ki-Wahyi; sawa na watunzaji wanaoandika.

Kisha watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa haki ili wahukumiwe kwa hukumu Yake.

Hakika hukumu ni yake, naye ni mwepesi wa wanaohisabu.

Anahisabu, anahukumu na anatekeleza katika muda mchache sana. Kwa sababu haki iko wazi, hukumu itapitishwa na malipo yameandaliwa na kila kitu kitatimia kwa kutaka tu.

﴿قُلْ مَن يُنَجِّيكُم مِّن ظُلُمَاتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ تَدْعُونَهُ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً لَّئِنْ أَنجَانَا مِنْ هَـٰذِهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ﴾

63. Sema: Ni nani anyewaokoa katika viza vya nchi kavu na baharini? Mnamwomba kwa unyenyekevu na kwa sauti ndogo: Kama akituokoa na haya, hakika tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru.

﴿قُلِ اللَّـهُ يُنَجِّيكُم مِّنْهَا وَمِن كُلِّ كَرْبٍ ثُمَّ أَنتُمْ تُشْرِكُونَ﴾

64. Sema: Mwenyezi Mungu huwaokoa katika hayo na katika kila mashaka, Kisha nyinyi mnamshirikisha.

﴿قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَن يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِّن فَوْقِكُمْ أَوْ مِن تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ أَوْ يَلْبِسَكُمْ شِيَعًا وَيُذِيقَ بَعْضَكُم بَأْسَ بَعْضٍ انظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُونَ﴾

65. Sema: Yeye ndiye awezaye kuwaletea adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu; au awavuruge (muwe) makundi, na awaonjeshe baadhi yenu jeuri ya wenzao. Tazama jinsi tunavyozieleza ishara kwa njia mbali mbali ili wapate kufahamu.

﴿وَكَذَّبَ بِهِ قَوْمُكَ وَهُوَ الْحَقُّ قُل لَّسْتُ عَلَيْكُم بِوَكِيلٍ﴾

66. Na watu wako wameikadhibisha nayo ni haki. Sema: Mimi si kuwakilishwa juu yenu.

﴿لِّكُلِّ نَبَإٍ مُّسْتَقَرٌّ وَسَوْفَ تَعْلَمُونَ﴾

67. Kila habari ina wakati maalum, Na punde mtajua.

## WAOKOA

**Aya 63 - 67**

### MAANA

Sema: Ni nani anyewaokoa katika viza vya nchi kavu na baharini? Mnamwomba kwa unyenyekevu na kwa sauti ndogo.

Viza vya nchi kavu na baharini ni fumbo la shida na machungu anayoyapata mwanadamu katika mambo yote anayoyafanya bara na baharini; nasi tunaongezea (katika ufafanuzi wetu)'angani' baada ya kuwa katika zama za anga, ambako ni hatari zaidi kuliko nchi kavu na baharini.

Maana ni kuwa Ewe Mtume! Waulize Washirikina na Walahidi, ni nani wanayemkimbilia kumwomba katika saa ya dhiki na kumnyenyekea katika siri na dhahiri. Je,wanamkimbilia Mwenyezi Mungu au wanawakimbilia wanaowaabudu asiyekuwa Mungu?

Tumesema katika kufasiri Aya ya 41 katika Sura hii kwamba umbile la mtu linamtambua Muumbaji wake, lakini pazia ya kufuata na hawaa inauzuia mwanga wake machoni. Wakati wa shida inaondoka pazia hii na hutamka mtu kwa umbile lake safi. Hakuna yeyote anayeokoka na shida hii vyovyote alivyo, hata mwenye afya huogopa maafa na kuhofia mwisho mbaya, akiwa ana akili.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Mwenye shida sana hahitaji dua zaidi kuliko yule asiye na shida ambaye hasalimiki na balaa."**

Kama akituokoa na haya, hakika tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru.

Yaani wanamfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu peke yake wakati wa shida na hofu na wanatoa ahadi wao wenyewe kuwa watampwekesha Mwenyezi Mungu na kumshukuru, kama akiwaokoa na viza vya nchi kavu na baharini. Mara tu wanaposalimika na kuwa katika starehe wanamshirikisha na kufanya ufisadi. Elimu imethibitisha kuwa udhaifu wa utu na matakwa yake unakwenda na hali; sawa na yalivyo maji hufuata rangi ya chombo yalimowekwa.

Sema: Mwenyezi Mungu huwaokoa katika hayo na katika kila mashaka.

Kwa hiyo ilikuwa ni juu yenu kuzitukuza neema za Mwenyezi Mungu na kuzishukuru.

Kisha nyinyi mnamshirikisha.

Lakini baada ya kuwaneemesha kwa kuokoka mmebadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa ukafiri na shirki.

Sema: Yeye ndiye awezaye kuwaletea adhabu kutoka juu yenu. Au kutoka chini ya miguu yenu, kama mitetemeko na kudidimizwa ardhini,

Au awavuruge (muwe) makundi.

Yaani awachanganye-changanye na kuwafanya vikundi vinavyopondana visivyokuwa na msimamo; au amfanye mmoja wenu awe katika vita na ugomvi pamoja na nafsi yake, aridhie jioni yale yaliyomkasirisha asubuhi na kinyume, hali yake igongane wala asiwe na msimamo.

Na awaonjeshe baadhi yenu jeuri ya wenzao.

Yaani mpigane wenyewe kwa wenyewe.

Tazama jinsi tunavyozieleza ishara kwa njia mbali mbali ili wapate kufahamu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasimamisha hoja na dalili zilizo wazi juu ya haki, kwa hisia akili na maono, na anapiga mifano ya kila aina kwa mbinu mbali mbali ili waijue haki waifuate, na batili wajiepushe nayo; na atakayehalifu basi hoja imemsimamia na atastahiki adhabu.

Na watu wako wameikadhibisha nayo ni haki.

Msemo unaelekezwa kwa Mtume, dhamiri ya wameikadhibisha inarudia kwa Qur'an inayotamka dalili na hoja na adhabu ya mwenye kuikadhibisha.

Sema: Mimi si kuwakilishwa juu yenu.

Bali ni mtoa bishara na mwonyaji anayefikisha aliyotumwa na kumwachia Mwenyezi Mungu mambo ya hisabu na adhabu.

Kila habari ina wakati maalum.

Inawezekana Tafsir ya 'mahali maalum' Maana ni kuwa kila habari anayoitekeleza Mwenyezi Mungu ina wakati au mahali maalum bila ya kuhalifu.

Na punde mtajua wakati wa kutokea kwake. Hili ni kemeo na kiaga kwa kukadhibisha haki.

﴿وَإِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَخُو ضُونَ فِي آيَاتِنَا فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ حَتَّىٰ يَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ وَإِمَّا يُنسِيَنَّكَ الشَّيْطَانُ فَلَا تَقْعُدْ بَعْدَ الذِّكْرَىٰ مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ﴾

68. Na unapowaona wanaoziingilia Aya zetu basi jitenge nao mpaka waingie katika mazugumzo mengine. Na kama shetani akikusahaulisha, basi usikae baada ya kukumbuka pamoja na watu madhalimu.

﴿وَمَا عَلَى الَّذِينَ يَتَّقُونَ مِنْ حِسَابِهِم مِّن شَيْءٍ وَلَـٰكِن ذِكْرَىٰ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ﴾

69. Wala si juu ya wale wenye takua hesabu yao hata kidogo, lakini ni mawaidha ili wapate kuwa na takua.

﴿وَذَرِ الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لَعِبًا وَلَهْوًا وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَذَكِّرْ بِهِ أَن تُبْسَلَ نَفْسٌ بِمَا كَسَبَتْ لَيْسَ لَهَا مِن دُونِ اللَّـهِ وَلِيٌّ وَلَا شَفِيعٌ وَإِن تَعْدِلْ كُلَّ عَدْلٍ لَّا يُؤْخَذْ مِنْهَا أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ أُبْسِلُوا بِمَا كَسَبُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ﴾

70. Na waache wale walioifanya dini yao ni mchezo na upuuzi na yamewadanganya maisha ya dunia. Na wakumbushe kwayo, isije nafsi yoyote ikafungwa kwa sababu ya yale iliyoyachuma, Haina mlinzi wala mwombezi isipokuwa Mwenyezi Mungu, Na hata ikatoa kila fidia haitapokelewa. Hao ndio waliofungwa kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Watapata kinywaji cha maji ya moto sana na adhabu chungu kwa sababu ya waliyokuwa wakiyakanusha.

## MPAKAWAINGIE KATIKA MAZUNGUMZO MENGINE

**Aya 68 - 70**

### MAANA

Na unapowaona wanaoziingilia Aya zetu basi jitenge nao mpaka waingie katika mazugumzo mengine.

Yamepita maelezo yake katika kufasiri Juz.5 (4:139)

Na kama shetani akikusahaulisha, basi usikae, baada ya kukumbuka, pamoja na watu madhalimu.

Msemo unaelekezwa kwa Mtume kwa dhahiri, lakini makusudio ni kwa mwingine kwa hali halisi. Kwa sababu Mtume ni mwenye kuhifadhiwa na madhambi na makosa na kusahau (maasum). Vinginevyo basi kauli yake na vitendo vyake na uthibitisho wake usingekuwa ni hoja na dalili mkato isiyokubali mjadala wala ubishi.

Wala si juu ya wale wenye takua hesabu yao hata kidogo, lakini ni mawaidha ili wapate kuwa na takua.

Yaani si juu ya waumini wanaomcha Mwenyezi Mungu chochote katika kufuatilia makafiri ambao wanaingilia Aya za Mwenyezi Mungu, lakini wawakumbushe na wawakataze ili wajiepushe kuingilia Aya za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ama Aya zifuatazo zina mambo yafuatayo:

Na waache wale walioifanya dini yao ni mchezo na upuuzi na yamewadanganya maisha ya dunia.

Kwa dhahiri amri inamwelekea Mtume na kwa hali ilivyo inamwelekea yeye na anayemfuata katika waumini. Anawaamrisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) waache kutangamana na wale ambao wameifanya dini yao ni mchezo na upuuzi na wala hakuwaamrisha kuwapuuza na kuacha kuwaonya. Kwa sababu kauli yake Mwenyezi Mungu:

Na wakumbushe kwayo ni amri ya kuwaonya.

Kila mwenye kuwa katika dini yoyote miongoni mwa dini na asiheshimu na kuitukuza misingi yake yote na hukumu zake zote, basi atakuwa ameifanya dini yake ni mchezo na upuzi. Mwenye kuifanyia dini chumo au akaita moja ya hukumu zake kwa namna ambayo inapelekea dharau, basi yeye atakuwa ndiye anayekusudiwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Walioifanya dini yao ni mchezo na upuzi.

Hakuna mwenye kutia shaka kuwa ambaye hana dini ni bora kuliko yule anayedharau misingi yake na hukumu zake. Kwa sababu huyu alivyo hasa ni kuwa ameifanyia dini mchezo na upuzi na hiyo ndiyo dini yake.

Na wakumbushe kwayo, isije nafsi yoyote ikafungwa kwa sababu ya yale iliyoyachuma. Haina mlinzi wala mwombezi isipokuwa Mwenyezi Mungu.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kumwamrisha Mtume na waumini kutotangamana na wale walioifanyia mchezo dini yao, aliwaamrisha kuwakumbusha Qur'an wale ambao wanaingilia Aya za Mwenyezi Mungu na kucheza na dini ili wasiadhibiwe kwa yale makosa na madhambi yaliyo chumwa na mikono yao, katika siku ambayo hawatapata msaidizi wa kuwasaidia asiyekuwa Mwenyezi Mungu wala mwombezi atakayewaombea mbele ya Mwenyezi Mungu.

Na hata ikatoa kila fidia haitapokelewa.

Yaani kama ambavyo kafiri hatapata mlinzi wala mwombezi siku ya Kiyama, vilevile haitakubaliwa fidia yake kwa namna yoyote itakavyokuwa. Amesema Razi: "Mtu akifikiri namna ya adhabu kwa njia hii atakurubia kugwaya anapothubutu kumwasi Mwenyezi Mungu."

Hao ndio waliofungwa kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Watapata kinywaji cha maji ya moto sana na adhabu chungu kwa sababu ya waliyokuwa wakiyakanusha.

Hao ni ishara ya wale walioifanyia mchezo dini. Na kufungika kwa waliyoyachuma; yaani wamewekwa rahani na matendo yao. Ama kupata kinywaji cha maji ya moto sana, ni kubainisha adhabu ya ukafiri wao na uasi wao.

11

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿قُلْ أَنَدْعُو مِن دُونِ اللَّـهِ مَا لَا يَنفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا وَنُرَدُّ عَلَىٰ أَعْقَابِنَا بَعْدَ إِذْ هَدَانَا اللَّـهُ كَالَّذِي اسْتَهْوَتْهُ الشَّيَاطِينُ فِي الْأَرْضِ حَيْرَانَ لَهُ أَصْحَابٌ يَدْعُونَهُ إِلَى الْهُدَى ائْتِنَا قُلْ إِنَّ هُدَى اللَّـهِ هُوَ الْهُدَىٰ وَأُمِرْنَا لِنُسْلِمَ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ﴾

71. Sema: Je, tuwaabudu wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawatunufaishi wala kutudhuru? Na turudishwe nyuma baada ya Mwenyezi Mungu kutuongoza? Kama yule ambaye mashetani wamempoteza; akiwayawaya katika ardhi, Anao marafiki wanaomwita kwenye uongofu: Njoo kwetu. Sema: Mwongozo hasa ni mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Na tumeamrishwa tusilimu kwa Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote.

﴿وَأَنْ أَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَاتَّقُوهُ وَهُوَ الَّذِي إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ﴾

72. Na simamisheni Swala na mcheni yeye; naye ndiye ambaye kwake mtakusanywa.

﴿وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ وَيَوْمَ يَقُولُ كُن فَيَكُونُ قَوْلُهُ الْحَقُّ وَلَهُ الْمُلْكُ يَوْمَ يُنفَخُ فِي الصُّورِ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ﴾

73. Naye ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi kwa haki, Na siku anayosema 'kuwa' basi huwa. Kauli yake ni haki. Na ufalme ni wake siku itakapopulizwa parapanda.

## SEMA: JE: TUWAABUDU WASIOKUWA MWENYEZI MUNGU?

**Aya 71-73**

### MAANA

Sema: Je, tuwaabudu wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawatunufaishi wala kutudhuru?

Mtume **(s.a.w.w)** aliwalingania washirikina katika kumwabudu Mwenyezi Mungu; nao wakamtaka aabudu masanamu yao. Inasemekana kwamba walitoa rai ya kuwa waabudu nao waungu wao na wao waabudu naye Mola wake.

Kwa vyovyote itakavyokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha, katika Aya hii, kuwaambia kwa kukanusha, vipi tuache kumwabudu Mwenyezi Mungu anayenufaisha na kudhuru na tuabudu wale wasiojiweza wao wenyewe kujinufaisha au kujikinga na madhara?

Na turudishwe nyuma baada ya Mwenyezi Mungu kutuongoza.

Kurudi nyuma ni neno linalotumiwa kwa mtu aliyeiacha haki akafuata batili.

Kama yule ambaye mashetani wamempoteza; akiwayawaya katika ardhi. Anao marafiki wanaomwita kwenye uongofu: Njoo kwetu.

Huu ni mfano anaoutoa Mwenyezi Mungu kwa aliyekataa Tawhid na kwenda kwenye ushirikina au ulahidi. Kwa ufupi nikuwa mfano wa mtu

huyu ni kama mfano wa mtu aliyekuwa katika msafara unakwenda kwa amani na salama.

Akauacha na akafuata njia yake jangwani bila ya mwelekeo wowote; kama ambaye amezungwa na mashetani. Basi wenzake wakamhurumia na kumwita: 'Njoo kwetu, hii ndiyo njia ya uongofu', lakini asiwajibu kwa kubabaika kwake. Ikawa mwisho wake ni balaa na maangamivu.

Mjuzi wa ghaibu na yanayoonekana, Naye ndiye mwenye hekima mwenye habari.

Sema: Mwongozo hasa ni mwongozo wa Mwenyezi Mungu.

Muundo huu wa kiubainifu unafahamisha kuwa mwongozo wa Mwenyezi Mungu haungiliwi na shaka yoyote; kama ambavyo unafahamisha kuwa mwongozo ni wa Mwenyezi Mungu peke yake katika kila kitu - katika itikadi sharia maadili na hali. Itikadi yoyote au fikra yoyote au kazi yoyote isiyokutana na mwongozo wa Mwenyezi Mungu basi ni ujinga na upotevu.

Na tumeamrishwa tusilimu kwa Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote.

Hii ni katika kutaja mahsusi baada ya ujumla. Kwa sababu mwongozo wa Mwenyezi Mungu unaingia katika kila aliloamrisha Mwenyezi Mungu na kulikataza. Makusudio ya kuuhusisha Uislamu ni kukumbusha utukufu wake.

Na simamisheni swala.

Kwani hakuna mwongozo wala Uislam ila kwayo; ndiyo nguzo ya dini, ikikubaliwa hukubaliwa mengine na ikikataliwa hukataliwa mengine.

Na mcheni yeye Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu. Ameamrisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) takua baada ya kuamrisha swala, Kwa sababu hakuna swala wala imani sahihi bila ya takua, Kumwabudu Mwenyezi Mungu kweli ni kwenda kwenye njia yake na kumtii katika hukumu zote, sio baadhi tu.

Naye ndiye ambaye kwake mtakusanywa.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na itakuja kila nafsi pamoja na mwendeshaji na shahidi" (50:21).

Mwendeshaji atakayeiendesha hadi mahshar (watakapokusanya watu) na shahidi atakayeishuhudilia kwa yale yaliyoandaliwa kwa siku hii.

Naye ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi kwa haki.

Haki hapa ni ishara ya kuwa ulimwengu una kanuni zinazouhukumu na desturi inayokwenda nao kwa mpangilio bila ya mkorogano wowote. Hii ni dalili fasaha ya kuweko mpangaji wa mambo na atakayeilipa kila nafsi ililochuma.

Na siku anayosema 'kuwa' basi huwa, Kauli yake ni haki.

Katika maneno haya kuna kukadiriwa, kutangulizwa, na kuwekwa nyuma. Asili yake ni hivi: Kauli yake ni haki siku anapokiambia kitu kuwa, huwa. Maana yake ni kuwa kauli ya Mwenyezi Mungu inakuwa tu; na hudhihirika wazi hilo siku anapokiambia kitu kuwa, kikawa, Ni sawa aliyasema haya siku alipoanza kuumba viumbe au siku atakapowarudisha.

Kwa maneno mengine ni kuwa kauli ya Mwenyezi Mungu ndiyo kitendo chake katika kupatikana kitu bila ya kitu, na katika kukirudisha jinsi kilivyokuwa baada ya kuharibika na kuchangukana.

Na ufalme ni wake siku itakapopulizwa parapanda.

Kupulizwa parapanda ni fumbo la kufufuliwa walio makaburini. Na maana ya ufalme wa ufufuo huu ni kwamba yeye ndiye anayerudisha wafu kwenye uhai.

### MASUFI

Mjuzi wa ghaibu na yanayoonekana.

Ghaibu ni mambo ya siri yaliyojificha, kama vile Malaika, ufufuo na mambo anayoyaficha mtu nafsini mwake. Na dhahiri ni yale yanayoonekana kidhahiri, kama vile ardhi, mbingu na anayoyafanya mtu wazi wazi.

Haya kwa binadamu ni sawa; ama kwa Mwenyezi Mungu hakuna ghaibu si katika mbingu wala ardhi, Hata hivyo masufi wanadai kuwa nafsi zao zinafichua ghaibu.

Ibn Al-Arabi, katika Futuhatil- makkiya mlango wa 302, anasema: "Hakika watu wa Mwenyezi Mungu wana macho wanayoonea na masikio wanayosikizia na nyoyo wanazofahamia na ndimi wanazosemea; si macho haya wala masikio au nyoyo na ndimi hizi. Kwa macho hayo wanaona na kwa masikio hayo wanasikia na kwa nyoyo hizo wanafahamu na kwa ndimi hizo wanasema na maneno yao yanapatia"

Naye ndiye mwenye hekima mwenye habari.

Yeye tu peke yake hana mshirika katika kupangilia mamabo ya viumbe vyake kulingana na heima yake na katika kujua siri zote. Basi hebu naamuogope Mwenyezi Mungu yule anayedai kuwa ana nyoyo mbili, ndimi mbili, macho mane na masikio mane.

﴿وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ آزَرَ أَتَتَّخِذُ أَصْنَامًا آلِهَةً إِنِّي أَرَاكَ وَقَوْمَكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ﴾

74. Na Ibrahim alipomwambia baba yake Azar: Unawafanya masanamu kuwa waungu? Hakika ninakuona wewe na watu wako mko katika upotofu ulio wazi.

﴿وَكَذَٰلِكَ نُرِي إِبْرَاهِيمَ مَلَكُوتَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلِيَكُونَ مِنَ الْمُوقِنِينَ﴾

75. Na namna hii tukamwonyesha Ibrahim ufalme wa mbingu na ardhi ili awe katika wenye yakini.

﴿فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ اللَّيْلُ رَأَىٰ كَوْكَبًا قَالَ هَـٰذَا رَبِّي فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَا أُحِبُّ الْآفِلِينَ﴾

76. Na usiku ulipomwingilia, akaona nyota, alinena: Hii ni Mola wangu. Ilipotua akasema: Sipendi wanaotua.

﴿فَلَمَّا رَأَى الْقَمَرَ بَا زِغًا قَالَ هَـٰذَا رَبِّي فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَئِن لَّ مْ يَهْدِنِي رَبِّي لَأَكُونَ نَّ مِنَ الْقَوْمِ الضَّالِّينَ﴾

77. Na alipouona mwezi unachomoza alisema: Huu ni Mola wangu. Ulipotua alisema: Asiponiongoza Mola wangu, hakika nitakuwa katika watu waliopotea.

﴿فَلَمَّا رَأَى الشَّمْسَ بَازِغَةً قَالَ هَـٰذَا رَبِّي هَـٰذَا أَكْبَرُ فَلَمَّا أَفَلَتْ قَالَ يَا قَوْمِ إِنِّي بَرِيءٌ مِّمَّ ا تُشْرِكُونَ﴾

78. Na alipoliona jua linachomoza alisema: Hili ndilo Mola wangu. Hili ni kubwa kabisa. Lilipotua alisema: Enyi watu! Mimi simo katika hayo mnayoyashirikisha.

﴿إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ﴾

79. Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi. Hali ya kuwa nimeacha dini za upotevu, tena mimi si katika washirikina.

## IBRAHIM NA BABA YAKE NAWATU WAKE

**Aya 74-79**

### MAANA

Na Ibrahim alipomwambia baba yake Azar: Unawafanya masanamu kuwa waungu? Hakika ninakuona wewe na watu wako mko katika upotofu ulio wazi.

Dhahiri ya Aya inafahamisha waziwazi kuwa Azar ni baba hasa wa Ibrahim Khalil (a.s); na kwamba alikuwa mshirikina muabudu masanamu; na kwamba Ibrahim alimkataza ushirikina na akamlingania kwenye Tawhid. Huu ndio ufahamisho wa Aya unaofahamika mara moja kwenye fahamu ya mjuzi na mjinga, bila ya kuweko ufafanuzi au tafsir.

Pamoja na hayo wafasiri wamerefusha maneno na wakatofautiana kuwa je, Azar ni baba hasa wa Ibrahim au ni baba yake kimajazi.

Tofauti hii inazalisha tofauti nyingine kuwa je mababa na mababu wote wa Muhammad **(s.a.w.w)** waliamini Mungu mmoja na wala haifai kuweko mshirikina hata mmoja, au inawezekana kuweko washirikina na wapwekeshaji? Baadhi ya maulama wametunga vitabu maalum vya hilo tu.

Shia wanasema baba na mababu zake wote Muhammad ni wapwekeshaji Mungu kutokana na Hadith isemayo: **"Niliendelea kugura kutoka migongo ya watakatifu mpaka kwenye mifuko ya uzazi ya watakatifu hadi akanitoa Mwenyezi Mungu kwenye ulimwengu wenu huu."**

Wakasema kuwa baba hasa wa Ibrahim anaitwa Tarik na kwamba Azar ni ndugu wa baba yake au babu yake wa upande wa mama yake, amepewa jina la baba kimajazi tu[1].

Al-Alusi anasema, "Kundi kubwa la Sunni pia wanasema hivyo" Lakini mwenye Tafsir Al-manar na Razi wanasema: "Sunni hawaafikiani na Shia kwenye rai yao hii na wanasema inawezekana kuweko washirikina au walahidi katika mababu wa Mtume."

Dhahiri ya Qur'an iko pamoja nao, hasa kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿وَاذْكُرْ فِي الْكِتَابِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّهُ كَانَ صِدِّيقًا نَّبِيًّا ﴿٤١﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنكَ شَيْئًا﴾

"Na mtaje Ibrahim katika Kitab, Hakika yeye alikuwa mkweli sana, Nabii, Alipomwambia baba yake: Ee baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyosikia na visivyoona na visivyokufaa chochote" (19: 41-42)

Kwa vyovyote iwavyo hakuna faida ya mzozo huu, kwa sababu hauna uhusiano wowote na itikadi ya Kiislamu. Kwa sababu linalotakikana kwa Mwislamu ni kuamini Utume wa Muhammad **(s.a.w.w)** na Isma yake na

---

1 Zimekuja Hadith Mutawatir kwamba Abdul Mutwalib, babu wa Mtume (s.a.w.w) aliapa kuwa akiruzukiwa watoto kumi atamchinja mmoja wao na kwamba kura ilimwangukia Abdullah, baba wa Muhammad (s.a.w.w). Haya yanapingana na kuwa mababu zake Mtume wote walikuwa kwenye dini ya Ibrahim.

kwamba yeye ni bwana wa Mitume na ni wa mwisho wao. Ama kuamini kuwa baba na mababu zake wote ni wapwekeshaji Mwenyezi Mungu, na kwamba Azar ni ami wa Ibrahim na sio baba yake, Yote haya si chochote katika itikadi ya Kiislamu.

Na namna hii tukamwonyesha Ibrahim ufalme wa mbingu na ardhi.

Makusudio ya 'namna hii' ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) kama ambavyo alimfichulia Ibarahim upotevu wa watu wake wa kuabudu kwao masanamu, pia alimfunulia maajabu ya mbingu na ardhi ili atoe dalili, kwa ustadi wa nidhamu yake na ufundi wa utengenezwaji wake, juu ya kuweko Mwenyezi Mungu, umoja wake na utukufu wake na awe miongoni mwa wenye yakini.

Aya hii inafahamisha mambo mawili:

**Kwanza**: itikadi ya Uislamu inaismamia uhuru wa rai na akili. Kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakuwajibisha mtu kumwamini ila baada ya kumwekea hoja na akataka afanye uchunguzi.

**Pili**: kuwa dalili aliyoiweka juu ya kuweko kwake ni nyepesi na sahali kufahamiwa na watu wote bila ya kuhitaji juhudi wala sayansi au falsafa. Yatosha mtu kuangalia maajabu ya ulimwengu na utaratibu wake ili aweze kuongoka kwa Muumbaji wake na mtegenezaji wake.

Na usiku ulipomwingilia, akaona nyota, alinena: Hii ni Mola wangu.

Watu wa Ibrahim walikuwa wakiabudu nyota badala ya Mwenyezi Mungu. Akataka kuwavuta kidogo kidogo kwenye haki na kuwaelekeza kwenye mantiki ya kiakili na kimaumbile kwa upole na ulaini. Akangoja mpaka usiku ulipoingia na kufunga giza, akaona nyota wanazoziabudu. Akasema kwa kuigiza madai yao: 'Huyu ni Mola wangu'. Wakamwamini, lakini ilipotua na kupotea pambizoni, akili zao zilizinduka na mtazamo wao ukaona kuwa Mwenyezi Mungu habadiliki wala kugeuka na wala hifichwi na chochote.

Na alipouona mwezi unachomoza alisema kwa kutaka kuwavuta: Huu ni Mola wangu, kwa sababu ni mkubwa na una mwangaza zaidi kuliko ule wa kwanza.

Ulipotua alisema: Asiponiongoza Mola wangu, hakika nitakuwa katika watu waliopotea.

Anaashiria kuwa yeye bado hajatulizwa nafsi yake na nyota hizii; na kwamba yeye bado hajaongoka kwenye njia na akamtaka Mwenyezi Mungu amwokoe.

Na alipoliona jua linachomoza alisema: Hili ndilo Mola wangu. Hili ni kubwa kabisa. Lilipotua alisema: Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayoyashirikisha.

Jaribio la kwanza, la pili na la tatu yamepita na shaka ikabakia kama ilivyokuwa. Kwa hiyo hapana budi kujiepusha na kuabudu nyota, Kwani hazistahiki kuabuduiwa wala kutukuzwa. Baada ya kutangaza kujitoa katika waungu wao aliuelekeza moyo wake kwa Muumba wa ulimwengu na akasema:

Hakika mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi, hali ya kuwa nimeacha dini za upotevu, tena mimi si katika washirikina.

Hii ndiyo natija ya utafiti na kufikiria katika kitu chochote miongoni mwa vitu vya ulimwengu huu. Mtazamo mmoja tu, wa kuangalia sura yoyote katika sura za ulimwengu huu, lazima utapelekea kwenye yakini ya mkato kuwa Mwenyezi Mungu pekee yake ndiye Muumba wa mbingu na ardhi.

﴿وَحَاجَّهُ قَوْمُهُ قَالَ أَتُحَاجُّونِّي فِي اللَّـهِ وَقَدْ هَدَانِ وَلَا أَخَافُ مَا تُشْرِكُونَ بِهِ إِلَّا أَن يَشَاءَ رَبِّي شَيْئًا وَسِعَ رَبِّي كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ﴾

80. Na watu wake wakamhoji. Akasema: Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu na hali yeye ameniongoza? Wala siogopi wale mnaowashirikisha naye; isipokuwa Mola wangu akitaka kitu, Mola wangu ana wasaa wa kujua kila kitu. Je, hamkumbuki.

﴿وَكَيْفَ أَخَافُ مَا أَشْرَكْتُمْ وَلَا تَخَافُونَ أَنَّكُمْ أَشْرَكْتُم بِاللَّـهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا فَأَيُّ الْفَرِيقَيْنِ أَحَقُّ بِالْأَمْنِ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ﴾

81. Nitaogopaje hao mnaowashirikisha, na hali nyinyi hamwogopi kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kile ambacho hakukiteremshia dalili kwenu? Basi kundi gani katika mawili haya linastahiki kupata amani kama nyinyi mnajua?

﴿الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُم بِظُلْمٍ أُولَـٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُم مُّهْتَدُونَ﴾

82. Wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na upotevu, hao ndio watakaopata amani na ndio walioongoka. 83. Na hiyo ndiyo hoja yetu tuliyompa Ibrahim juu ya watu wake. Tunamuinua kwa vyeo yule tumtakaye, Hakika Mola wako ndiye mwenye hekima, Mjuzi.

## JE, MNANIHOJI JUU YA MWENYEZI MUNGU

**Aya 80 – 83**

### LUGHA

Neno 'hoja' linatumika kwa maana ya dalili zenye kuthibitisha haki; na hutumiwa kwa maana yale anayoyatolea hoja mdai kuthibitisha madai yake.

### MAANA

Na watu wake wakamhoji.

Baada ya Ibrahim kuwapatia watu wake hoja inayoingia akilini kutokana na mantiki ya kiakili na kimaumbile, na kuthibitisha uharibifu na ibada yao ya mizimu na nyota, baada ya yote hayo nao walileta hoja zao dhaifu. Wakasema miongoni mwa waliyoyasema:

﴿قَالُوا وَجَدْنَا آبَاءَنَا لَهَا عَابِدِينَ﴾

"Tumewakuta baba zetu wakiyaabudu" (21:53)

Ndipo Ibrahim akawajibu kwa kusema:

Je, mnanihoji juu ya Mwenyezi Mungu na hali yeye ameniongoza?

Yaani ni hoja gani hizi kuhusu Mwenyezi Mungu na hali yeye ameniongoza kumjua kutokana na nafsi yangu na ulimwengu. Imetangulia katika sura hii Aya ya 71:

﴿قُلْ إِنَّ هُدَى اللَّـهِ هُوَ الْهُدَىٰ﴾

"Sema: Mwongozo hasa ni mwongozo wa Mwenyezi Mungu" (6:71) Ambao hauna shaka yoyote, vinginevyo ni ujinga na upotevu. Ama

kuhofisha waungu wao alikujibu kwa kusema: Wala siogopi wale mnaowashirikisha naye wasiokuwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hawadhuru wala hawanufaishi, hawoni wala hawasikii, Isipokuwa Mola wangu akitaka chochote kwa kuniangushia sanamu kichwani kwangu linivunje fuvu, au kimondo cha nyota kitakachoniunguza.

Mola wangu ana wasaa wa kujua kila kitu.

Kwa hiyo siogopi kuwa nitapatwa na jambo lolote baya bila ya kujua yeye au kutaka.

Je, hamkumbuki kuwa miungu yenu si chochote na kwamba Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye kudhuru na kunufaisha. Kwa sababu yeye ni Muumbaji wa kila kitu.

Nitaogopaje hao mnaowashirikisha, na hali nyinyi hamwogopi kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kile ambacho hakukiteremshia dalili kwenu?

Makusudio ya mliowashirikisha ni masanamu na nyota mnaoziabudu. Maana nikuwa mnataka niwaogope waungu wenu walioumbwa wanaoshindwa na nyinyi hamwogopi madai yenu ya kumfanyia Mungu washirika, madai ambayo ni uzushi usiokuwa na hoja wala dalili!

Kwa maneno mengine, Ibrahim aliwaambia je, mnanihofisha kwa wale wasiokuwa na uwezo, na nyinyi mmejiamini na kumfanyia uzushi yule mwenye nguvu na uwezo kwa wote?

Basi kundi gani katika mawili haya linastahiki kupata amani kama nyinyi mnajua?

Kundi linalomwamini Mwenyezi Mungu mwenye nguvu, mwenye kushinda, au linaloamini udhaifu ulio dhalili?

Wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na upotevu, hao ndio watakaopata amani na ndio walioongoka.

Huu ni ubainifu wa kundi lililookoka katika makundi mawili na kwamba wao ndio waliomfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu katika imani yao na hawakuchanganya na imani hii kushirikisha katika itikadi wala katika kutii hawaa za kiumbe yeyote awaye. Hawa peke yao ndio waliosalimika, wenye kuongoka.

Na hiyo ndiyo hoja yetu tuliyompa Ibrahim juu ya watu wake.

Yaani hizo ndizo hoja ambazo tumemtia ilham Ibrahim , zinazoingia bongoni ambazo aliwahshinda nazo Ibrahim watu wake. Aya hii ni dalili wazi kwamba Mitume na wale wanaoongozwa na mwongozo wao katika maulama, ni maneno ya Mwenyezi Mungu na ubainifu wake; na kwamba kuwapinga ni kumpinga Mwenyezi Mungu hasa; kama ilivyoelezwa katika Hadith.

Tunamuinua kwa vyeo yule tumtakaye.

Utaipata Tafsir yake katika Juz 28 (58:11.) inshaallah Sababu ya kuinuliwa mtu kwa Mwenyezi Mungu ni imani na elimu, na kila moja katika hayo ina daraja ya juu na ya juu zaidi. Ibrahim alifikia ile ya juu zaidi mpaka akawa rafiki wa Mwenyezi Mungu (Khalilullah).

Hakika Mola wako ndiye mwenye hekima, Mjuzi.

Mwenye hekima aliyetakata na mchezo na matamanio, anajua anayostahiki kila mtu katika daraja na vyeo.

﴿وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۚ كُلًّا هَدَيْنَا ۚ وَنُوحًا هَدَيْنَا مِن قَبْلُ ۖ وَمِن ذُرِّيَّتِهِ دَاوُودَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَىٰ وَهَارُونَ ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ﴾

84. Na tukampa Is-haq na Yaqub Kila mmoja tulimuongoza, Na Nuh tulimwongoza zamani. Na katika kizazi chake Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na kama hivyo tunawalipa wafanyao mema.

﴿وَزَكَرِيَّا وَيَحْيَىٰ وَعِيسَىٰ وَإِلْيَاسَ ۖ كُلٌّ مِّنَ الصَّالِحِينَ﴾

85. Na Zakariya na Yahya na Isa na Ilyas; wote ni katika wema.

﴿وَإِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطًا ۚ وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَى الْعَالَمِينَ﴾

86. Na Ismail na Al-yasaa na Yunus na Lut; na kila mmoja tulimfadhilisha juu ya walimwengu wote.

﴿وَمِنْ آبَائِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَإِخْوَانِهِمْ ۖ وَاجْتَبَيْنَاهُمْ وَهَدَيْنَاهُمْ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ﴾

87. Na katika baba zao na vizazi vyao na ndugu zao na tukawachagua na kuwaongoza katika njia iliyonyooka.

﴿ذَٰلِكَ هُدَى اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۚ وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾

88. Huo ni uongozi wa Mwenyezi Mungu, Kwa huo humwongoza amtakaye katika waja wake. Na kama wangelishirikisha bila shaka yangeliporomoka yale waliyokuwa wakiyatenda.

﴿أُولَٰئِكَ الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ ۚ فَإِن يَكْفُرْ بِهَا هَٰؤُلَاءِ فَقَدْ وَكَّلْنَا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوا بِهَا بِكَافِرِينَ﴾

89. Hao ndio tuliowapa Kitab na hukumu na utume. Kama hawa wakiyakataa, basi tumekwisha yawakilisha kwa watu wasioyakataa.

﴿أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۖ فَبِهُدَاهُمُ اقْتَدِهْ ۗ قُل لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرَىٰ لِلْعَالَمِينَ﴾

90. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza, basi fuata mwongozo wao. Sema: Siwaombi ujira juu ya haya. Haikuwa hiyo ila ni mawaidha kwa waimwengu wote.

## NA TUKAMPA IS-HAQ NA YAQ'UB

**Aya 84 - 90**

### MAANA

Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Aya hizi ametaja Mitume 18 akiwemo Ibrahim, Baadhi akawaashiria kwa baba zao, vizazi vyao na ndugu zao. Na amewasifu wote kwa hisani, wema na uongofu, na kwamba yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaneemesha Mitume waliotajwa kwa hekima na Unabii na baadhi yao akawaneemesha kwa kuteremshiwa Kitab.

Makusudio katika hayo ni kutoa hoja Muhammad **(s.a.w.w)** kwa Waarabu kwamba babu yao ni Ibrahim na wanawe wengi walikuwa wenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu.

Vilevile Mtume afuate nyayo za Mitume waliotangulia katika kulingania kwa Mwenyezi Mungu na kuvumilia adha. Huu ndio muhtasari wa madhumuni ya Aya hizi saba.

Uko wazi usiohitaji ubainifu wa kurefusha na ufafanuzi, lakini baadhi ya wafasiri wamekataa ila kurefusha, wakatoka nje ya maudhui ya Tafsir kufikia ambako hakuna uhusiano wowote na maisha.

Ni vizuri ifahamike kuwa majina ya Mitume yaliyotajwa katika Aya hayakuja kwa mpangilio wa wakati au ubora; kama ambavyo wametajwa kwa njia ya mifano tu.

Na tukampa Is-haq na Yaqub.

Dhamir ya 'tukampa' inamrudia Ibrahim. Is-haq ni mwanawe wa kumzaa na mama yake ni Sara. Yaqub ni mwana wa Is-haq, na mwana wa mwana ni mwana. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿فَبَشَّرْنَاهَا بِإِسْحَاقَ وَمِن وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ﴾

"Basi tukambashiria Is-haq na baada ya Is-haq ni Yaqub." (11:71)

Kila mmoja Is-haq na Yaqub tulimuongoza.

Na Nuh tulimwongoza zamani kwani yeye ni wa zamani kuliko Ibrahim.

Na katika kizazi chake.

Dhamir inamrudia Nuh, yaani na kizazi cha Nuh, kwa sababu ndiye wa karibu kutajwa, Imesemekana kuwa inamrudia Ibrahim.

Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun.

Yaani wote hawa tumewaongoa kama tulivyomwongoza Nuh, Is-haq na Yaqub.

Na kama hivyo tunawalipa wafanyao mema.

Kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) anamlipa mwema kwa wema, awe Mtume au sio Mtume; kama anavyomlipa mwovu kwa amali yake awe mweupe au mweusi. Na Zakariya na Yahya na Isa na Ilyas. Hawa vilevile ni katika aliowaongoza Mwenyezi Mungu.

Wote ni katika watu wema.

Na kila mwenye kutumia kipawa chake kwa kheri yake na kheri ya watu basi yeye ni mwema na mtengenevu.

### HASAN NA HUSEIN NI WANAWA MTUME

Anasema Razi katika Tafsir yake kuhusu Aya hii: "Hakika Aya hii inafahamisha kuwa Hasan na Hussein ni katika kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**.

Kwa sababu Mwenyezi Mungu amemjaalia Isa ni katika kizazi cha Ibrahim, ingawaje yeye amenasibiana na Ibrahim kwa upande wa mama tu. Vilevile Hasan na Hussein ni katika kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu ingawaje wananasibika na Mtume kwa mama. Inasemekana kuwa Abu Jafar Al-Baqir, aliitolea dalili Aya hii mbele za Hajjaj bin Yusuf."

Mwenye Tafsir Al-Manar anasema: "Ninasema katika mlango wa Hadith Abu Bukra kwa Bukhari, iliyo Marfu'. (Hakika mwanangu, huyu ni Sayyid) yaani Hassan. Na neno mwanangu, kwa Waarabu, halitajwi kwa watoto wa binti. Na Hadith ya Umar katika Kitab Ma'rifatu Sahaba cha Abu Naim, iliyo marfu'; (kuwa kila mtoto wa Adam ukoo wao unatokana na baba yao, isipokuwa watoto wa Fatima, mimi ndiye baba yao na ni ukoo wao). Watu wakazoea haya, wakawa wanasema kuhusu watoto wa Fatima kuwa ni

watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na ni kizazi chake na Ahlu bait (watu wa nyumbani) wake."

Maana ya maneno haya ni kuwa watoto wa Fatima (a.s) si watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kilugha, lakini ni watoto wake kisharia, kutokana na kauli ya Mtume 'mimi ni baba yao na ukoo wao.' Vilevile ni watoto wake kimazoweya, kwa sababu watu walizoweya kuwaita kuwa ni watoto wa mtume.

Wamekongamana kwa kauli moja maulama wa Sunni na Shia kwamba sharia inatangulia ufahamisho wa matamko kimazowea na kilugha; na kwamba mazoea yanaitangulia lugha. Kwa sababu, mwenye hekima huzungumza na watu kwa lile wanalolifahamu haraka sio kwa lile lililoandikwa katika kamusi za lugha.

Likija neno katika Aya au Hadith, na tukakuta Tafsir maalum ya maana yake katika Qur'an au Hadith, basi tamko hilo litachukuliwa katika maana haya maalum; na huitwa maana ya kisharia na kupuuzwa ile ya kilugha na kimazoea. Ikiwa hatukupata maana maalum, basi tutalichukulia kwa maana wanayoifahamu watu; na huitwa maana ya mazoea. Wakitolifahamu watu kwa maana hayo, basi itachukuliwa maana yake kutoka kwenye kamusi za lugha.

Kwa hiyo basi maana ya sharia yanakuwa katika ngazi ya kwanza, ya mazoea katika ngazi ya pili na ya kilugha katika ngazi ya tatu. Na imethibiti kisharia na kimazoea kuwa Hassan na Hussein ni watoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Hivyo ikapuuzwa maana ya kilugha. Kwa sababu lugha inahukumiwa na sharia na mazoea.

Ama siri ya kuwa Hasan na Husein ni wana wa Mtume ingawaje si wanawe kilugha, ataipata mpekuzi katika sifa za hao wawili na hulka zao. Inamtosha mwenye kufanya utafiti wa sera ya Hasan kuwa Muawiya bin Abu Sufian hakupata wasaa wa Ufalme aliokuwa nao na huku Hassan bado yu hai. Na inamtosha mwenye kutafiti sera ya Hussein kwamba Yazid bin Muawiya dunia ilimzonga kwa kuweko Husein, kama ilivyomzonga baba yake, Muawiya kwa kuweko Hasan.

Na Ismail na Al-yasaa na Yunus na Lut, Vilevile tuliwaongoa.

Na kila mmoja tulimfadhilisha juu ya walimwengu wote katika zama zake.

Na katika baba zao na vizazi vyao na ndugu zao.

'Katika' hapa ni ya kubaadhisha; yaani baadhi yao Kwa sababu katika vizazi vyao na ndugu zao walikuwako makafiri; bali Isa na Yahya hawakuwa na kizazi.

Na tukawachagua na kuwaongoza katika njia iliyonyooka.

Sifa hizi ni utanguluzi wa kauli yake Mwenyezi Mungu:

Huo ni uongozi wa Mwenyezi Mungu, Kwa huo humwongoza amtakaye katika waja wake.

Yaani uongozi ambao ni wajibu kufuata ni ule waliokuja nao Mitume, wala hafuati mwongozo huu ila aliyepewa tawfiki na Mwenyezi Mungu.

Na kama wangeshirikisha, bila shaka yangeliporomoka yale waliyokuwa wakiyatenda.

Yaani hawa Mitume pamoja na ubora wao na utukufu wao wa vyeo, lau ingelitokea kufanya chembe ya kitu inayofahamisha shirk, basi bila shaka yangelibatilika yale waliyokuwa wakiyatenda na kuwa ni bure tu.

Lengo la ishara hii ni kuzindua kuwa Mwenyezi Mungu atawafanyia watu kulingana na amali zao si kulingana na vyeo vyao, na kwa watakavyoishilia wanapokufa, si kwa walivyoanzia uhai wao.

Hao ndio tuliowapa Kitab na hukumu na utume.

Hao, ni wale Mitume waliotangulia kutajwa. Na Kitab, ni jinsi ya Kitab inayochanganya vitabu vyote vya Mwenyezi Mungu vilivyoitangulia Qur'an, kama vile Mbao za Ibrahim, Tawrat, Zabur na Injil. Makusudio ya 'Hukumu' ni kujua kuhukumu na kila lile aliloliwekea sharia Mwenyezi Mungu katika halali na haramu.

Kama hawa wakiyakataa, basi tumekwisha yawakilisha kwa watu wasioyakataa.

Hawa, ni washirikina wa Kiquraish ambao wameukana Utume wa Muhammad **(s.a.w.w)** na kumfanyia uadui. Wanayoyakataa ni Utume. Makusudio ya watu ambao hawayakanushi ni Muhajirina na Ansari[1] ambao walimwamini Muhammad na wakamsaidia.

Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza, basi fuata mwongozo wao.

Hao wanaotajwa hapa ni Mitume waliotangulia kutajwa. Mwenyezi Mungu amemwamrisha Mtume wake mtukufu kufuata nyao zao katika kuilingania haki na kuvumilia adha katika njia yake.

Sema: Siwaombi ujira juu ya haya.

Kwa sababu dini haikuwekwa kuwa ni chumo na biashara.

Haikuwa hiyo ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.

Dhamir ya hiyo ni Qur'an. Maneno haya ni dalili wazi kuwa Muhammad ametumwa kwa watu, wakati wote na mahali pote.

﴿وَمَا قَدَرُوا اللَّـهَ حَقَّ قَدْرِهِ إِذْ قَالُوا مَا أَنزَلَ اللَّـهُ عَلَىٰ بَشَرٍ مِّن شَيْءٍ ۗ قُلْ مَنْ أَنزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَىٰ نُورًا وَهُدًى لِّلنَّاسِ ۖ تَجْعَلُونَهُ قَرَاطِيسَ تُبْدُونَهَا وَتُخْفُونَ كَثِيرًا ۖ وَعُلِّمْتُم مَّا لَمْ تَعْلَمُوا أَنتُمْ وَلَا آبَاؤُكُمْ ۖ قُلِ اللَّـهُ ۖ ثُمَّ ذَرْهُمْ فِي خَوْضِهِمْ يَلْعَبُونَ﴾

91. Na hawakumkadiria Mwenyezi Mungu kwa haki ya kadri yake, waliposema: Mwenyezi Mungu hakuteremshia chochote juu ya binadamu yoyote. Sema: nani aliyekileta Kitab alichokuja nacho Musa chenye nuru na mwongozo kwa watu? Mlichokifanya nyaraka- nyaraka, mkizidhihirisha na mkificha mengi, Na mkafundishwa msiyoyajua nyinyi wala baba zenu. Sema: Ni Mwenyezi Mungu, Kisha waache wacheze katika porojo zao.

﴿وَهَـٰذَا كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ مُّصَدِّقُ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَلِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا ۚ وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۖ وَهُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ﴾

92. Na hiki ni kitab tulichokiteremsha, kilichobarikiwa, chenye kusadikisha yale yaliyokitangulia. Na ili uwaonye (watu wa) Ummul qura

1 Muhajirina ni wale waliohama pamoja na Mtume kutoka Makka hadi Madina na Ansar ni wale waliowakaribisha Muhajirina.

na walio pambizoni mwake. Na wale wanaoamini akhera, wanakiamini, Nao huzihifadhi Swala zao.

## HAWAMHESHIMU MWENYEZI MUNGU KAMA INAVYOTAKIWA

**Aya 91 - 92**

### MAANA

Na hawakumkadiria Mwenyezi Mungu kwa haki ya kadiri yake, waliposema: Mwenyezi Mungu hakuteremshia binadamu chochote.

Aya hii inafahamisha kuwa katika wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kulikuwa na watu wanaokanusha wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa mtu yoyote, na wakisema kuwa Mwenyezi Mungu hakumtuma mtu yeyote kuwa mjumbe.

Lakini Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakubainisha ni akina nani waliokanusha na kusema hivyo, Kwa ajili hii waliotofautiana wafasiri, kuhusu waliokusudiwa katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Je, ni washirikina wa Kiarabu au Mayahudi wa Hijaz?

Kuna kundi la wafasiri waliosema kuwa ni washirikina wa Kiarabu. Kauli hii inapingwa, kwanza kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha Mtume wake kuwakabili na swali hili:

Sema: Ni nani aliyekileta Kitab alichokuja nacho Musa chenye nuru na mwongozo kwa watu?

Kimsingi ni kuwa swali hili linaelekezwa kwa yule anayekubali Utume wa Musa na Tawrat; na yajulikana kuwa washirikina wa Kiarabu hawakubali Utume wa Musa na Tawrat yake; vinginevyo wangelikuwa ni katika watu wa Kitab.

Pili, ni kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewatahayariza wakanushaji kwa kauli yake:

Mlichokifanya nyaraka-nyaraka, mkizidhihirisha na mkificha mengi.

Yaani kuwa nyinyi mmeibadilisha Tawrat, mkadhihirisha yale yanayoafikiana na hawaa zenu na mkaficha yale yasiyoafikiana nayo. Inajulikana kuwa walioibadilisha Tawrat ni Mayahudi, sio washirikina wa Kiarabu.

Kundi jingine la wafasiri limesema kwamba waliosema kuwa Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote kwa mtu, ni Mayahudi. Wakatoa dalili kwa mambo mawili: Kuwa Mwenyezi Mungu alimwamrisha Mtume wake Muhammad amjibu anayesema hivi kwa Utume wa Musa na Tawrat, nalo ni jibu sahihi, kisha akatilia mkazo jibu hili kwa kuipotosha kwao Tawrat akasema: "Mlichokifanya nyaraka-nyaraka."

Kauli hii iko karibu na dhahiri ya Aya kuliko ile ya kwanza.

Na mkafundishwa msiyoyajua nyinyi wala baba zenu.

Msemo huu unaelekezwa kwa Mayahudi vilevile; na maana yake ni, vipi mnasema - Enyi Mayahudi - kuwa Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote kwa mtu yeyote na hali nyinyi mnaitakidi kwamba Musa ni mwanadamu na kwamba Tawrat imeteremshwa kwake? Na mmejua kutokana nayo yale mliyokuwa hamyajui nyinyi na baba zenu.

Miongoni mwayo ni kuwa nyinyi mlikuwa mkisoma katika Tawrat sifa za Muhammad kabla ya kutumwa kwake, wala hamkuwa mkimjua kwa

ufafanuzi aliyekusudiwa. Mwenyezi Mungu alipomtuma na mkamjua aliyekusudiwa hasa, kwa kiburi na inadi yenu mkageuza na kuondosha yale yanayomwelezea.

Sema: Ni Mwenyezi Mungu.

Hili ni jawabu la swali lililotangulia (Sema: Ni nani aliyeteremsha Kitab alichokuja nacho Musa?

**Jibu**: hili ndilo lenyewe hasa na halikimbiliki. Kwa sababu Mayahudi wanakiri kuwa Tawrat inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Na kwa ajili ya kukiri kwao huku ndio inawasimamia hoja na kuwajibu kauli yao ya kuwa Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote kwa mtu.

Kisha waache wacheze katika porojo zao.

Yaani sema haki Ewe Muhammad, na waache Mayahudi katika batili zao wala usijishughulishe na inadi zao na ria zao.

Huku ni kuwapa onyo na kuwapa kiaga, kama ambavyo pia ni kuwadharau na kuwapuuza.

**Utauliza**: Mayahudi wanaukubali Utume wa Musa (a.s) na kuteremshwa Tawrat, kama yalivyotangulia maelezo. Kwa hiyo imekuwaje Mwenyezi Mungu akawanasibishia kukanusha wahyi na Utume?

**Jibu**: Wao wanakanusha wahyi na Utume kwa dhahiri, kwa inadi na kiburi kwa Muhammad **(s.a.w.w)** na si kwa undani hasa.

﴿وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا﴾

"Na wakazikakataa kwa dhuluma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo" (27:14)

## MITUME WA MWENYEZI MUNGU NA WANASAYANSI

Wanasayansi wengi wakati huu wanaamini kuweko Mwenyezi Mungu, Kwa sababu wameona kuwa ulimwengu huu unakwenda kulingana na kanuni thabiti, na iliyowazi inayohukumu, haiepukani nao kwa hali yoyote ile.

Kwa ajili hii imewezekana kuichunguza, kuikisia na kufaidika nayo. Huku ni kuthibitika kuweko nguvu ya hali ya juu nyuma ya ulimwengu inayofanya uhandisi na kujenga; na nguvu hiyo ndio Mwenyezi Mungu.

Kwa maneno mengine, si lazima mtu akitaka kujua kuweko kila kitu afanye majaribio katika vyombo na kukiona kwa macho, bali inatosha kwa kujua kwa elimu isiyo na shaka na dhana, ni sawa elimu hiyo iwe imetokana na majaribio na macho au imetokana na natija ya akili ya kiasili. Mwenye fikira na uchunguzi akitaamali ulimwnengu huu kwa taamuli ya kielimu isiyo na shaka shaka, lazima atakomea kwenye kumjua Mwenyezi Mungu.

Lakini Wanasayansi waliojua kuweko Mwenyezi Mungu kwa Kisayansi, wamekanusha kuwa ana wajumbe katika watu anaowapa wahyi na wakasema: Nguvu-asili (nature) peke yake ndio Kitab cha Mwenyezi Mungu na wala sio Tawrat, Injil na Qur'an.

Sina shaka kwamba wataalam hawa, lau wangelipa somo la Qur'an wakati mdogo tu katika muda ule ule walioutoa kwa kusoma sayansi wangelikinai kuwa Mwenyezi Mungu ana vitabu viwili: Ulimwengu na wahyi, Na kwamba mtu anavihitajia vyote viwili.

Kutokana na Kitab cha ulimwengu atajua Ufalme wa Mwenyezi Mungu na kumwamini. Na kutokana na Kitab cha wahyi atajua sharia ya Mwenyezi

Mungu ambayo itamwangazia njia ya maisha, kusonga mbele na kujiepusha na maangamizo na matatizo ambayo yatachelewesha safari yake ya kwenda mbele.

Mtu ameumbwa ili afanye kazi katika maisha haya, kwa hivyo basi, hapana budi kwa kila anayefanya amali kuwa na njia anayoifuata katika kufanya kazi, Kwa sababu kujifanyia mambo ovyo ovyo hakupelekei kheri yoyote. Na Mwenyezi Mungu ndiye aliyememuumba mtu, anajua siri yake na dhahiri yake, nguvu yake na udhaifu wake na yale yanayomnufaisha na kumdhuru.

Kwa hiyo basi ni lazima kuwa yeye ndiye marejeo ya kwanza ya njia ambayo inapasa mtu kuifuata katika kazi yake; sawa na ilivyo kwa mgunduzi wa ndege na gari na mengineyo; ambapo inakuwa lazima kumrejea yeye katika kutaka kuitumia na kufaidika nayo. Kwa sababu yeye ndiye Ayajuae zaidi masilahi ya ndege na madhara yake.

Hakuna mwenye shaka kwamba kuifikisha njia ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake na kuwafahamisha kunafungika na Mitume na Manabii, kwa sababu wao ndio lugha ya Mwenyezi Mungu na ubainifu wake. Huu ndio wahyi hasa.

Anayetaka ufafanuzi na arejee kitab chetu Al-Islam wal-aql (Uislamu na akili) sehemu ya Utume na akili.

Na hiki ni kitab tulichokiteremsha, kilichobarikiwa, chenye kusadikisha yale yaliyokitangulia.

Hii, ni Qur'an Tukufu; na maana ni kuwa kama tulivyoteremsha Tawrat kwa Musa, Vilevile tumeiteremsha hii Qur'an Kwa Muhammad **(s.a.w.w)** nayo ina manufaa na faida nyingi kwa anayejua hukumu zake na siri zake na akazitumia.

Nayo Vilevile inasadikisha vitabu vya Mwenyezi Mungu ambavyo vimeteremshiwa Mitume wa Mwenyezi Mungu tangu zamani. Imam Ali anasema: "Jifundisheni Qur'an kwani hiyo ni mazungumuzo mazuri, na ifahamuni kwani hiyo ni utuvu wa nyoyo, na ifanyeni dawa kwa nuru yake kwani hiyo ni ponyo la nyoyo, na isomeni vizuri kwani hiyo ina visa vizuri."

Na ili uwaonye (watu wa) Ummul qura na walio pambizoni mwake.

Ummul-qura (Mama wa miji) ni Makka. Imeitwa hivyo kwa sababu mna nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Wastashriki (Wataalamu wa kimagharibi juu ya mambo ya uislamu) na kabla yao Mayahudi walidai kuwa Muhammad **(s.a.w.w)** ametumwa kwa Waarabu tu, kwa kutolea hoja Aya hii, na kusahau Aya nyingine; kama vile:

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ﴾

"Na hatukukutuma ila uwe ni rehema kwa walimwengu wote" (21:107)

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ﴾

"Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri na muonyaji; lakini watu wengi hawajui" (34:28)

Wamejitia purukushani na Aya hizo na hali chimbuko la Qur'an ni moja. maneno yake yanajifasiri hayo yenyewe na Aya mbili hizi ni ubainifu wa kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Na ili uwaonye (watu wa) Ummul qura na walio pembezoni mwake.'

Na Vilevile makusudio yake ni kuanza mwito wa Uislam, mwanzo kabisa, katika mji wa mwenye mwito huo; yaani Makka.

Mpaka utakapopata wafuasi ndipo uwape bishara walio kando kando yake; kama vile mwito wowote unavyoanza, ambapo unazaliwa kisha unatembea mabara yote.

Zaidi ya hayo imethibiti riwya kwa njia ya Mutawatir kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliwaandikia Wafalme na viongozi wote akiwalingania kwenye Uislamu, miongoni mwao ni Mfalme Kisra wa Fursi (Iran) na Kaizari wa Roma. Wastashriki wanajua hayo, lakini baadhi yao wanaficha wanayoyajua.

Na wale wanaoamini akhera, wanakiamini.

Dhamiri ya wanakiamini inarudia Kitabu ambacho ni Qur'an. Yeyote atakayeisoma Qur'an kwa uchunguzi na kuzingatia maana hutoka na kitu. Akiwa anamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, basi huzidi imani, na akiwa anamwamini Mwenyezi Mungu tu, basi ataamini wahyi na ufufuo; akiwa anamwamini Mwenyezi Mungu na ufufuo bila wahyi, basi ataamini Mitume na vitabu vya Mwenyezi Mungu, na hasa Utume wa Muhammad na Qur'an.

Akiwa anamkanusha Mwenyezi Mungu atamwamini; Kwa sababu Qur'an itamwonyesha dalili za hilo na kumhimiza kuichunguza. Nayo kwa asili yake humpeleka mtafiti, anayechunga haki, kwenye elimu.

Nao huzihifadhi Swala zao.

Ili daima wawe na mawasiliano ya kutegemewa na Mwenyezi Mungu. Ameihusisha kutaja Swala kinyume cha ibada nyinginezo kwa sababu ndiyo nguzo kubwa ya dini na inayodumisha imani. Miongoni mwa kazi za swala ni kumkataza mwenye kuswali uovu na mambo mabaya.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA

﴿وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّـهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ شَيْءٌ وَمَن قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنزَلَ اللَّـهُ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنفُسَكُمُ الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّـهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ﴾

93. Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule amzuliaye uwongo Mwenyezi Mungu. Au mwenye kusema: Nimeletewa Wahyi; na hali hakuletewa wahyi wowote Na yule asemaye: Nitateremsha kama alivyoteremsha Mwenyezi Mungu. Na lau ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti na Malaika wamewanyooshea mikono. Zitoeni roho zenu; leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyokuwa haki, na mlikuwa mkizifanyia kiburi ishara Zake.

﴿وَلَقَدْ جِئْتُمُونَا فُرَادَىٰ كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَتَرَكْتُم مَّا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ وَمَا نَرَىٰ مَعَكُمْ شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَاءُ لَقَد تَّقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ عَنكُم مَّا كُنتُمْ تَزْعُمُونَ﴾

94. Na hakika mtatujia wapweke kama tulivyowaumba kwanza. Na mmeacha nyuma yenu yale tuliyowapa. Na hatuwaoni waombezi wenu pamoja nanyi ambao mlidai ni washirika.

## KUMZULIA UWONGO MWENYEZI MUNGU

**Aya 93-94**

### MAANA

Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule amzuliaye uwongo Mwenyezi Mungu.

Kumzulia Mwenyezi Mungu uwongo ni kumtengenezea mambo ambayo hayana chimbuko katika Qur'an wala Hadith au katika misingi ya akili. Na hayo yanakuwa kwa mambo yafuatayo:

• Kuhalalisha aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu au kuharamisha aliyoyahalalisha.

• Kumsingizia Mwenyezi Mungu, kwa makusudi, yale asiyokuwa nayo au kumfanyia washirika au kuwa ana watoto na mabinti.

• Kudai Utume kwa asiyekuwa Mtume. Hilo ameliashiria Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kauli yake: Au mwenye kusema: Nimeletewa Wahyi; na hali hakuletewa Wahyi wowote. Jumla hii inaungana na ile ya 'Amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo.' Ni katika mlango wa kuunganisha mahsusi kwenye ujumla.

• Na yule asemaye: Nitateremsha kama alivyoteremsha Mwenyezi Mungu.Yaani mlaanifu huyu anadai kuwa ana uwezo wa kutunga Kitab kitakachofanana na Qur'an katika utukufu wake. Imesekana kuwa mtu huyo

ni Abdullah bin Sa’d bin Abu Sarh. Wengine wamesema ni Nadhr bin Harith.

Kwa ufupi ni kwamba kila mwenye kumnasibishia Mwenyezi Mungu kitu chochote bila ya kutegemea kauli ya Mwenyezi Mungu na ya Mtume au misingi ya akili basi huyo ni mzushi, mwongo mkubwa na anayestahiki shutuma na adhabu.

Na lau ungewaona madhalimu wanavyokuwa katika mahangaiko ya mauti na Malaika wamewanyooshea mikono.

Mahangaiko ya mauti ni maumivu ya kukata roho, Wafasiri wametofautiana katika makusudio ya kunyoosha mikono ya Malaika. Je, makusudio ni kunyoosha kiuhakika wakati mtu anapokata roho, au ni fumbo tu la kufananisha vituko vya mauti?

Sisi hatuoni haja yoyote ya mzozo huu, Kwa sababu akili haikatai kuweko Malaika wala kuwa na mikono wanaoinyoosha au ndimi za kuzungumzia. Kwani Wahyi umelieleza hilo, kwa hiyo ni wajibu kuamini. Msingi huu wanautegemea Maulama wote Waislamu katika kuthibitisha itikadi na sharia.

Zitoeni roho zenu; leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkisema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyokuwa ya haki, na mlikuwa mkizifanyia kiburi ishara zake.

Haya yote ni maneno ya Malaika wakiwaambia wazushi wakati wa kufa. Nayo ni lawama na shutuma kwa uzushi wao na kukana kwao haki. Kuna Hadith isemayo: "Anayekufa kiyama chake kimesimama." Kwa sababu hii wamesema baadhi ya wajuzi kwamba mtu ana viyama viwili, kidogo ambacho ni mauti na kikubwa, ufufuo.

Shutuma za Malaika kwa anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, katika Kiyama kidogo, ni onyo la vituko vya Kiyama kikubwa atakavyokumbana navyo. Imam Ali anasema: "Kifo kwa Mumin ni kama kuvua nguo chafu na kufungua minyororo na kuvaa kanzu ya kifahari na kushukia kwenye maliwazo. Ama kwa kafiri, ni kama kuvua kanzu ya kifahari na kuvaa gwanda chafu, na kutoka kwenye maliwazo kwenda kwenye vitisho na adhabu kubwa."

Na hakika mtatujia wapweke kama tulivyowaumba kwanza.

Yaani mwanadamu atakutana na Mola wake kesho, kama alivyotoka tumboni mwa mamake hana chochote.

Afadhali angeliingia ardhini kama alivyotoka - haulizi wala haulizwi, lakini atarudi akiwa ni mwenye kuulizwa. Alhamdulilah, mwenye kuuliza ni mwadilifu hamdhulumu yeyote na atamfanyia mtu vile alivyowafanyia watu alipokuwa katika uhai wake wa kwanza. Ikiwa ni kheri basi itakuwa kheri na ikiwa ni shari basi ni shari.

Wametofautiana wanavyuoni kuhusu kufufuliwa kuwa je, ni kwa roho tu, au ni kwa roho na kiwiliwili pamoja. Dhahiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu: kama tulivyowaumba kwanza, inafahamisha kufufuliwa kwa roho na kiwiliwili kwa sababu vyote viwili vimeumbwa pamoja.

﴿كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُعِيدُهُ وَعْدًا عَلَيْنَا إِنَّا كُنَّا فَاعِلِينَ﴾

"Kama tulivyoanza umbo la awali tutalirudisha tena, Ni ahadi iliyo juu yetu, hakika sisi ni watendaji" (21:104)

Na mmeacha nyuma yenu yale tuliyowapa.

Mtu atarudi ardhini akiwa ameacha watu wake, marafiki mali na ufalme.

Na hatuwaoni waombezi wenu pamoja nanyi ambao mlidai ni washirika (wa Mwenyezi Mungu) kwenu.

Kama vile masanamu, nyota na mengineyo mliyokuwa mkiyaabudu na kuwatawalisha wafisadi na wapotevu.

Kwa hakika yamekatika (mahusiano) baina yenu.

Yaani hamna mawasiliano yoyote ya duniani.

Na yamewapotea mliyokuwa mkidai katika madai ya uwongo kwa wale mliowafikiria kuwa ni washirika au waombezi mbele yake, na yamepotea matumaini yenu baada ya kufichuka uhakika; na mwema ni yule atakayefuzu kupata radhi za Mwenyezi Mungu na maghufira yake.

﴿إِنَّ اللَّهَ فَالِقُ الْحَبِّ وَالنَّوَىٰ يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَمُخْرِجُ الْمَيِّتِ مِنَ الْحَيِّ ذَٰلِكُمُ اللَّهُ
فَأَنَّىٰ تُؤْفَكُونَ﴾

95. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye mpasuaji mbegu na kokwa. Humtoa aliye hai katika maiti na ni mtoaji wa maiti katika aliye hai. huyo ndiye Mwenyezi Mungu basi mnageuzwa wapi?

﴿فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ﴾

96. Ndiye mpambazuaji wa asubuhi; ameufanya usiku kuwa mapumziko na utulivu, na jua na mwezi (kwenda) kwa hesabu, Hayo ndiyo makadirio ya Mweye nguvu, Mjuzi.

﴿وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ النُّجُومَ لِتَهْتَدُوا بِهَا فِي ظُلُمَاتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ
يَعْلَمُونَ﴾

97. Na yeye ndiye aliyewafanyia nyota ili muongoke kwazo katika viza vya bara na baharini. Hakika tumezifafanua ishara kwa watu wanaojua.

﴿وَهُوَ الَّذِي أَنشَأَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ فَمُسْتَقَرٌّ وَمُسْتَوْدَعٌ قَدْ فَصَّلْنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَفْقَهُونَ﴾

98. Na Yeye ndiye aliyewaanzisha nyinyi kutokana na nafsi moja. Pako mahali pa kutulia na pa kupita njia. Hakika tumezifafanua ishara kwa watu wanaofahamu.

﴿وَهُوَ الَّذِي أَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ نَبَاتَ كُلِّ شَيْءٍ فَأَخْرَجْنَا مِنْهُ خَضِرًا نُّخْرِجُ مِنْهُ
حَبًّا مُّتَرَاكِبًا وَمِنَ النَّخْلِ مِن طَلْعِهَا قِنْوَانٌ دَانِيَةٌ وَجَنَّاتٍ مِّنْ أَعْنَابٍ وَالزَّيْتُونَ وَالرُّمَّانَ مُشْتَبِهًا
وَغَيْرَ مُتَشَابِهٍ انظُرُوا إِلَىٰ ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَيَنْعِهِ إِنَّ فِي ذَٰلِكُمْ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ﴾

99. Naye ndiye aliyeteremsha maji kutoka mbinguni na kwayo tunatoa mimimea ya kila kitu, Kisha tukatoa kutokana nayo kijani, Tukatoa ndani yake punje zilizopandana, Na katika mitende yakatoka kwenye makole yake mashada yaliyo karibu. Na bustani za miza bibu na mizaituni na mikomamanga. Yanayofanana na yasiyofanana. Angalieni matunda yake yanapozaa na kuiva kwake. Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaoamini.

## HUTOA ALIYE HAI KATIKA MAITI

**Aya 95-99**

## MAANA

Katika Aya hizi kuna mifano ya ajabu katika viumbe ambavyo anayemiliki utengenezaji wake ni Mwenyezi Mungu peke yake. Vilevile kufahamisha kuwepo Mwenyezi Mungu na utukufu wake. Mifano imetajwa kwa mpango ufuatao:

Hakika Mwenyezi Mungu ndiye mpasuaji mbegu na kokwa.

Ukiweka mbegu ya ngano au kokwa ya tende katika ardhi itapasuka chini na juu. Upande wa chini itatoka mizizi na kushuka ardhini, na upande wa juu utatoka mti utakaorefuka hewani. Kisha ile mbegu au kokwa itapotea na mchanganyiko wote kuwa kitu kimoja, sehemu moja itakuwa ardhini na nyingine itakuwa kwenye hewa.

Hakuna mwenye shaka kwamba kazi yote hii inategemea sababu zake za kimaumbile; kama vile mchanga, maji, jua na hewa, lakini vyote hivyo vinaishia kwa Mwenyezi Mungu peke yake, kwa sababu yeye ndiye aliyeumba maumbile, msababishaji wa sababu na mpatishaji wa mada ya kwanza kwa neno 'Kuwa' na ikawa.

## UHAI UMETOKA WAPI?

Humtoa aliye hai katika maiti na ni mtoaji wa maiti katika aliye hai.

Si ajabu kuzalika kitu hai kutoka kwa kilicho hai mfano wake; na kisicho na uhai kutoa kisicho na uhai. Vilevile chenye uhai kuzaa kisicho na uhai, au kinyume chake. Msemaji mmoja alisema: "Uhai unazalikana kutokana na nguvu ya asili ya maumbile." Tumwulize msemaji huyu:

Ni nani aliyeifanya ipatikane asili hiyo, nguvu zake na utendaji kazi wake? Ikiwa msukumano tu unatosha kuleta uhai bila ya kuweko msaada wa Mwenyezi Mungu, basi kwa nini wanasayansi wameshindwa kutengeneza uhai kama vile watengenezavyo vyombo vya jikoni na mengineyo; pamoja na kuwa wamejaribu wakaleta msukumano; lakni baada ya kukata tamaa walisema kwamba kutengeneza uhai ni kuzito kuliko kumrudisha mzee utotoni.

Hebu tuchukulie kuwa wao wanajiona watafaulu katika kutengeza chembehai, je, wamefaulu kutengeza mdudu mdogo tu?.

Tuache binadamu na ubongo wake na wanyama na maumbile yao ya ajabu na tupige mfano wa hawa wadudu tunaowaogopa na kupiga madawa kuwauwa. Baadhi ya wataalamu wa wadudu wanasema hivi: "Baadhi ya wadudu wanaishi katika nyuzi joto 50 chini ya sifuri; wengine wanaishi nyuzi joto hizi hizi juu ya sifuri, wengine katika hewa ya sumu na wengine katika visima vya mafuta, na wana utaratibu mzuri sana katika maisha yao na kazi zao."

Ikiwa mwanaadamu anaweza kugundua satalaiti, maroketi na akili za Elktroni, lakini hawezi kabisa kutengeza bawa la mbu au chembe moja ya mbawa zake. Akili ya binadamu ni kubwa lakini ukubwa wake ni wenye kuhemewa mbele ya uweza wa ajabu ulioumba mbu na chungu na nyuki!

Yote hayo yako wazi, Lakini msiba mkubwa ni kuwa tumejisahau, hatujiangalii sisi wenyewe na uwazi wa uweza wa Mwenyezi Mungu mwenye hekima. Kama tukiangalia tutazidi imani kwa kiwango kikubwa kwa muumba aliye mkubwa. Tunachohitajia ni imani na imani yetu inahitajia akili kwa sababu imani bila ya akili ni kama uso bila macho.

Ndiyo, tunahitaji kuamini uweza wa Mwenyezi Mungu ili tufasiri yale yaliyoshinda akili za mabingwa, ambazo zimeshindwa kufasiri maumbile ya uhai. Na wengi wenye akili hizo wanakimbilia kwenye kitu kilicho nyuma ya maumbile, Uwezo wenye hekima na ujuzi, wanaufasiri kwa kusema kuwa ni asili ya uhai, huyo ndiye Mwenyezi Mungu basi mmegeuzwa wapi?

Anaema Enstein: "Hakika uoni wetu wa kidini ndio unaloelekeza uoni wetu wa kielimu". Ustadh Tawfiq Al-Ahkim aliongeza katika kitabu chake Fannul-adab: 'Huku bila shaka ni kukiri dini. Hakuna mtaalamu yeyote katika waliopiata aliyesema kuhusu dini kama alivyosema huyu."

Nasi twaongeza juu ya kauli ya Al-Hakim, kwamba siri pekee ya kukubali wataalamu wa karne ya ishirini ni kuwa uoni wa dini ndio chimbuko la uoni wa kielimu, ni kuendelea kwa elimu katika karne hii na kuwa ilikuwa nyuma katika zama zilizopita. Kila inapopiga hatua elimu ndipo dini inapozidi kupata watetezi; kama Einstein anayekubali ukuu wa dini na kuamini kuwa ni haki ambayo haiingiliwi na batili mbele yake wala nyuma yake.

Ndiye mpambazuaji wa asubuhi; ameufanya usiku kuwa mapumziko na utulivu, na jua na mwezi (kwenda) kwa hesabu.

Mwenyezi Mngu (s.w.t) ametaja katika Aya zlizotangulia mifano ya utukufu wake kwa kupatikana uhai kwenye ardhi; na katika Aya hii ametaja mifano mitatu ya mbinguni:

**Kwanza**: kuwa ameitoa asubuhi kwenye usiku, hilo ni fumbo la kupatikana mchana ambao watu wanahangaikia riziki na kupanga mambo yao.

**Pili**: kwamba yeye Mwenyezi Mungu ameuleta usiku kwa ajli ya kutulia na kupumzika kutokana na machovu za kazi ya mchana kutwa.

**Tatu**: kwamba ameweka Jua na Mwezi kwa kiasi mahsusi cha haraka na polepole kwa namna ambayo ardhi inakuwa na harakati mbili: Harakati za masaa 24, hisabu ya siku moja, na harakati za mwaka, ambazo ndani yake mna misimu mine ambayo ni hisabu ya mwaka mmoja. Mwenyezi Mngu (s.w.t) amesema:

﴿هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَّرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ﴾

"Yeye ndiye aliyelijaalia Jua kuwa mwanga na mwezi kuwa nuru na akaupimia vituo ili mjue idadi ya miaka na hisabu' (10:5)

**Utauliza**: kwa hiyo basi kupatikana usiku na mchana ni natija ya mzunguko wa ardhi , basi kuna wajihi gani wa kutegemeza kwa Mwenyezi Mungu?

**Jibu**: kwa sababu yeye ndiye Muumba mbingu na ardhi na kwake yeye ndio mwisho wa sababu zote , kwa hali yoyote ni kuwa makusudio ya kwanza ya kila yaliyokuja katika Aya hizi ni kuwa hakuna kitu katika vitu vya ulimwengu vilivyopatikana kwa sadfa na kibahati, isipokuwa kumetokana na aliye Mjuzi, Mwenye hekima aliyekipa kila kitu umbile lake na kukikadiria.

Hayo ndiyo makadirio ya weye nguvu, Mjuzi, Na Yeye ndiye aliyewafanyia nyota ili muongoke kwazo katika viza vya bara na baharini. Hakika tumezifafanua ishara kwa watu wanaojua.

Nyota hapa ni kutoa Jua na Mwezi kama inavyofahamika kutokana na mpangilio wa maneno. Katika kitabu Qur-an walilmul-hadith anasema

bingwa wa falaki James Jentis: "Tunapotaka kujua nyumba fulani katika mji iko wapi tunauliza jina la mtaa kisha namba yake, basi ni hivyohivyo katika nyota, kwani katika hizo kuna zilizo maarufu kwa majina yake mahsusi nazo ni alama muhimu wanazozifuata mabaharia katika majahazi yao na waendeshao vyombo na wapanda wanyama. Ni misafara mingapi inyokwenda kwa ramani ya mbinguni na nyota wakati dira inapoacha kufanya kazi?"

Na Yeye ndiye aliyewaanzisha nyinyi kutokana na nafsi moja. Pako mahali pa kutulia na pa kupita njia. Hakika tumezifafanua ishara kwa watu wanaofahamu.

Nafsi iliyoumbwa kila moja kutokana nayo ni mtu wa kwanza ambaye watu wote wametokana naye ambaye ni Adam.

Tumezungumzia kwa ufafanuzi tulipofasiri Juz.4 (4:1) Razi ametaja kauli sita katika kufasiri mahali pa kutulia na pa kupita njia.

Wafasiri wengi wamesema 'kutulia' ni kutulia manii katika migongo ya wanaume na 'pa kupita njia' kuwa katika matumbo ya uzazi ya wanawake. Katika Aya hakuna linalofahamisha hilo, wala lolote katika maana sita alizozinukuu Razi.

Imepokewa kutoka kwa Imam Sadiq (a.s) kwamba: yeye amegawanya waumini katika mafungu mawili; mwenye kuamini imani ya kweli inayotulia mpaka kufa, ambaye maneno yake yanaafikiana na vitendo vyake, na mumini ambaye imani yake inalegalega iko kwa muda tu, inamwondoka kabla ya kufa; maneno yake yanatofautiana na vitendo vyake.

Hakika tumezifafanua ishara kwa watu wanaofahamu.

Na asiyefahamu dalili hizi za ulimwengu juu ya ukuu wa muumbaji, mwanzilishi, basi huyo ni katika wale waliokusudiwa na kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿صُمٌّ بُكْمٌ عُمْيٌ فَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ﴾

"Ni viziwi ni mabubu ni vipofu kwa hivyo hawafahamu" (2:171)

Naye ndiye aliyeteremsha maji kutoka mbinguni na kwayo tunatoa mimea ya kila kitu.

Mvua ndio chimbuko la maji tamu, lau si hiyo ardhi ingelikuwa kame isiyo na uhai. Mwenyezi Mungu ametegemeza kushuka maji kwake yeye, kwa sababu yeye ndiye msababishaji wa sababu, kwake huanza kila kitu hata kama mzunguko utakuwa mrefu kiasi gani.

Kisha tukatoa kutokana nayo kijani.

Dhamiri ya 'nayo' inarudia kwenye mimea. Makusudio ya kijani ni ubichi, yaani kutokana na mmea huchipua matawi mabichi. Inasemekana kuwa maana ya kijani hapa ni ubichi zaidi.

Tukatoa ndani yake punje zilizopandana.

Dhamiri ya 'ndani yake' ni ndani ya hiyo kijani, yaani tunatoa mashuke katika matawi kama vile ya ngano nk, na kama mfano wa, tunda la komamanga ambalo tembe zake zinapandana.

Na katika mitende yakatoka kwenye makole yake mashada yaliyo karibu.

Yaani ni rahisi kuyachuma au kuwa kukurubiana kwa wingi wake.

Na bustani za miabibu na mizaituni na mikomamanga.

Yaani tunatoa katika mimea aina hizi tatu. Mwenyezi Mungu amezitaja kwa njia ya kupigia mfano ambayo kutokana nazo itajulikana mingine.

Yanayofanana na yasiyofanana.

Katika mimea kuna inayofanana katika umbile na ladha na mingine haifananai.

Angalieni matunda yake yanapozaa na kuiva kwake.

Yaani zingatieni vipi linatoka tunda mwanzo, linakuwa dogo lisilo na manufaa kisha linabadilika badilika mpaka kuiva na kuwa na ladha tamu.

Hakika katika hayo kuna ishara kwa watu wanaoamini.

Makusudio ya wanaoamini siyo wale wanaoamini tu, bali ni wale wanaotikia mwito wa imani na kunufaika na dalili na hoja. Ama wenye nyoyo zilizofungwa wanazipita kama wanyama.

Kwa ufupi makusudio ya kwanza ya mifano hii ya ardhini na mbinguni ni kuleta uzindushi kuwa vitu vya ulimwengu huu na vilivyomo ndani yake vinatokana na uanzilishi na upangiliaji.

Ni muhali kuwa vimekuja kisadfa katika mtazamo wa kiakili na kimaumbile.

Hizo mbili zinahukumu kwa mkato kwamba kila liliopo limepatikana kwa matakwa na makusudio na kwa hekima ya hali ya juu anayoijua mjuzi na mjinga, wala hakuna kitu kinachobatilisha sadfa kama vile kukaririka tukio moja kila zinapokaririka sababu zake.

﴿وَجَعَلُوا لِلَّـهِ شُرَكَاءَ الْجِنَّ وَخَلَقَهُمْ ۖ وَخَرَقُوا لَهُ بَنِينَ وَبَنَاتٍ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۚ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يَصِفُونَ﴾

100. Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika majini, Hali yeye amewaumba. Na wamemsingizia kuwa na wana wa kike na wa kiume bila ujuzi. Ametakasika na ametukuka juu ya hayo wanayombandikiza nayo.

﴿بَدِيعُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ أَنَّىٰ يَكُونُ لَهُ وَلَدٌ وَلَمْ تَكُن لَّهُ صَاحِبَةٌ ۖ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ﴾

101. Mbunifu wa mbingu na ardhi. Inawezekanaje awe na mwana hali hana mke, Na ameumba kila kitu. Naye ni Mjuzi wa kila kitu.

﴿ذَٰلِكُمُ اللَّـهُ رَبُّكُمْ ۖ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ فَاعْبُدُوهُ ۚ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ﴾

102. Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu hakuna Mola (mwingine) isipokuwa Yeye; Muumba wa kila kitu, Kwa hivyo mwabuduni yeye. Na yeye ni mtegemewa wa kila kitu.

﴿لَّا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ ۖ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ﴾

103. Hayamfikii macho, Bali yeye huyafikia macho. Naye ni Mpole Mwenye habari.

﴿قَدْ جَاءَكُم بَصَائِرُ مِن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَنْ أَبْصَرَ فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ عَمِيَ فَعَلَيْهَا ۚ وَمَا أَنَا عَلَيْكُم بِحَفِيظٍ﴾

104. Hakika zimewajia busara kutoka kwa Mola wenu. Basi atakayefungua macho ni faida yake mwenyewe; na atakayeyapofua ni hasara yake mwenyewe, Nami si mtunzaji wenu.

﴿وَكَذَٰلِكَ نُصَرِّفُ الْآيَاتِ وَلِيَقُولُوا دَرَسْتَ وَلِنُبَيِّنَهُ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ﴾

105. Na namna hii tunazifafanua ishara na waseme umesoma. Na ili tuyabainishe kwa watu wanaojua.

﴿اتَّبِعْ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ ۖ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ﴾

106. Fuata uliyopewa wahyi kutoka kwa Mola wako. Hakuna Mola (mwingine) isipokuwa Yeye; na jitenge na washirikina.

﴿وَلَوْ شَاءَ اللَّـهُ مَا أَشْرَكُوا ۗ وَمَا جَعَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ۖ وَمَا أَنتَ عَلَيْهِم بِوَكِيلٍ﴾

107. Na kama Mwenyezi Mungu angetaka wasingeshirikisha. Na hatukukufanya uwe mtunzaji wao wala wewe si mlinzi juu yao.

## WAMEMFANYIA MWENYEZI MUNGU WASHIRIKA

**Aya 100-107**

### MAANA

Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika majini.

Washirikina wako aina nyingi, kuna waliofanya masanamu ni miungu, kuna walioabudu nyota, walioabudu Iblisi na waliofanya giza kuwa ni Mungu. Kundi jingine wamefanya majini kuwa ni washirika wa Mwenyezi

Mungu. Mwenyezi Mungu ameeleza kuwapo Malaika na kwamba amewaumba kutokana na moto.

Katika Aya tuliyo nayo Mwenyezi mungu ameeleza tu kikundi ambacho kimewafanya majini ni washirika wa Mwenyezi Mungu, lakini hakubainisha aina ya majini hawa walioabudiwa na washirikina, je ni majini wa kuwazia tu au ni wengineo?

Kwa ajili hii ndipo wafasiri wakatofautiana, Kuna waliosema ni Ibilisi wengine wakasema ni giza na mengineyo ambayo hayana msingi wowote wa kielimu kabisa.

Kwa maana yoyote itakavyokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu amewajibu washirikina hawa kwa kifupitu Hali yeye amewaumba, na dhamir ya Amewaumba inawarudia majini. kwani wao ndio walio karibu na hiyo dhamir.

Inawezekana kuwa inawarudia wshirikina au wote, kwa sababu Mwenyezi Mungu ameumba majini na watu; kwa maana yakuwa ni vipi Mwenyezi Mungu awe na washirika naye ni Muumba wa kila kitu?

Na wamemsingizia kuwa na wana wa kike na wa kiume bila ujuzi.

Washirikina wa kiarabu walisema kuwa malaika ni mabinti wa Mungu, Mayahudi wakasema Uzair ni mwana wa Mungu na wakristo wakasema Masih ni mwana wa Mungu Maneno yote hayo ni dhana na madai bila ya ujuzi.

Ametakasika na ametukuka juu ya wanayombandikiza nayo.

Ametakata Mwenyezi Mungu na upungufu na yuko juu kuliko wanavyomsifu nayo, Mbunifu wa mbingu na ardhi. Yaani ameziumba bila ya mfano uliotangulia.

Inawezekanaje awe na mwana hali hana mke wa jinsia yake wala wa jinsia nyingine, kwa sababu hana mfano na kitu kingine naye ni mwenye kujitosha na kila kitu. Umetangulia ufafanuzi katika kufasiri Juz.5 (4:50)

Na ameumba kila kitu.

Na muumbwa hawezi kuwa mshirika na Muumba.

Naye ni Mjuzi wa kila kitu.

Pamoja na hayo ati hajui kama ana mtoto; lau angekuwa naye angelimjua. Kwa hivyo kuacha kujua jambo hakumaanishi kutokuwepo kulingana na asiyekiuwa Mwenyezi Mungu. Ama kulingana na Mwenyezi Mungu ni kuwa ujuzi wake hauepukani na kupatikana yanayojulikana.

Huyo ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu hakuna Mola (mwingine) isipokuwa Yeye; Muumba wa kila kitu, Kwa hivyo mwabuduni yeye.

Msemo unaelekezwa kwa washirikina maana ni kuwa Mwenyezi Mungu amekusanya sifa zote za upweke, akaumba ulimwengu na vilivyomo na kupanga mambo yote basi yeye ndiye mwenye haki ya kumpwekesha kwa ibada wala msimshirikishe na yeyote pia msimnasibishie mke na mwana.

Hayamfikii macho.

Tumezungumzia kwa ufafanuzi kuhusu kumwona Mungu katika kufasiri Juz.1 (2:55)

Bali yeye huyafikia macho na mengineyo kwa sababu Yeye amekizunguka kila kitu.

Naye ni Mpole, Mwenye habari.

Mpole kwa waja wake, mwenye habari ya matendo yao na makusudio yao.

Hakika zimewajia busara kutoka kwa Mola wenu.

Makusudio ya busara hapa ni dalili na hoja za kuwepo Mwenyezi Mungu na kuwa Yeye ni mmoja, zikiwamo zile zilizotangulia kupasua mbegu na kokwa (konde), kuumba usiku na mchana, kuumba watu kutokana na nafsi moja na kuteremsha maji ambayo ni uhai wa kila kitu. Kutumia busara kuwa ni dalili ni katika hali ya kutumia kisababishi kuwa ni sababu. Kwani busara ni kujua kunakotokana na na moyo; na kujua huku kunatokana na dalili na hoja.

Basi atakayefungua macho ni faida yake mwenyewe; na atakayeyapofua ni hasara yake mwenyewe.

Baada ya kutoa dalili za mkato juu ya haki, hapa Mwenyezi Mungu anasema kuwa atakayefuata basi ameifanyia nafsi yake na atakayehalifu basi ameifanyia ubaya nafsi yake mwenyewe.

﴿إِنْ أَحْسَنتُمْ أَحْسَنتُمْ لِأَنفُسِكُمْ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا﴾

"Mkifanya wema mnajifanyia wema nafsi zenu, mkifanya ubaya mnajifanyia nafsi zenu" (17:7)

Na namna hii tunazifafanua ishara na waseme umesoma. Na ili tuyabainishe kwa watu wanaojua.

Wakati wa Ujahiliyya Waarabu walikuwa hawajui kusoma, hawana elimu yoyote. Waliposikia Qur'an na wakaona fani za fasihi, aina kwa aina za hoja zinazowazima wao na yale wanayoyatukuza, Lakini bado waliendelea kukataa. Hali yao ilipokuwa hivyo walitafuta vijisababu wakasema: "Ewe Muhammad, Qur'an hii uliyokuja nayo umejifundisha tu wala sio Wahyi kutoka kwa Mungu".

Kwa maelekezo haya inatubainikia kuwa kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Na namna hii tunazifafanua ishara,' maana yake ni, tumetermsha katika Qur'an aina na dalili na ubainifu kwa makusudio ya kuongoka kwazo washirikina na waache kumwambia Mtume kuwa wewe umesoma.

Ama kauli yake: 'Ili tuyabainishe kwa watu wanaojua' maana yake ni tunazifanua Aya za Qur'an ili wanufaike nazo wale wanaojua maana yake uwaongoze kwenye imani na haki. Ama wajinga na wapotevu hakuna matarajio ya kuongoka kwao. mwisho wa mambo ni kuwa Aya hizi zinakata nyudhuru zao na kuwa ni hoja juu yao.

Fuata uliyopewa wahyi kutoka kwa Mola wako. Hakuna Mola (mwingine) isipokuwa Yeye; na jitenge na washirikina.

Hii ni amri ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake ya kuonya na kutoa bishara kwa Qur'an na kudumu juu ya hilo wala asijali ukanushaji wa washirikina na kukadhibisha na istihzai zao.

La kushangaza ni kauli ya asemaye kuwa Aya hii ni mansukh (imefutwa hukumu yake) na Aya ya kupigana. Mwenyezi Mungu hakumwamrisha Mtume kuacha kupigana na washirikina katika Aya hii mpaka isemwe kuwa ni mansukh ila amemwamrisha kufuatilila kuilingania haki na kutojali ukadhibishaji wa washirikina.

Kimsingi ni kuwa kulingania haki bila ya kujali ni jambo jingine na kupigana ni jambo jingine. Sharti ya kwanza ya naskh na mansukh (yenye kufuta na yenye kufutwa hukmu) ni kuwa maudhui yawe mamoja.

Na kama Mwenyezi Mungu angetaka wasingeshirikisha.

Yaani Yeye Mwenyezi Mungu mtukufu hakutaka kuwasukuma kwenye imani au kuwalazimisha kuacha ushirikina kwa neno 'kuwa ikawa' ambalo ameliumbia ulimwengu. Lau angelitaka waamini kwa matakwa haya basi wasingeshirikisha. Angalia tafsiri ya Juz.1 (2:26).

Na hatukukufanya uwe mtunzaji wao wala wewe si mlinzi juu yao.

Jumla ya kwanza na ya pili zina maana moja au maana yanayokurubiana wala hatufahamu lengo lolote la hilo isipokuwa kutilia mkazo; bali mkazo huu vilevile ni mkazo wa kauli yake: 'Na jitenge na washirikina.' Kwa sababu lau angelikuwa ni mtunzaji na mlinzi wao, basi isingelijuza kujitenga nao.

﴿إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم﴾

"Hakika ni kwetu sisi marejeo yao, kisha ni juu yetu sisi hesabu yao" (88:25-26)

﴿وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ فَيَسُبُّوا اللَّـهَ عَدْوًا بِغَيْرِ عِلْمٍ كَذَٰلِكَ زَيَّنَّا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلَهُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِم مَّرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾

108. Wala msiwatukane wale wanaoomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua, Kama hivyo tumewapambia kila umma vitendo vyao. Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao, naye atawaambia yale waliyokuwa wakiyatenda.

﴿وَأَقْسَمُوا بِاللَّـهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَتْهُمْ آيَةٌ لَّيُؤْمِنُنَّ بِهَا قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِندَ اللَّـهِ وَمَا يُشْعِرُكُمْ أَنَّهَا إِذَا جَاءَتْ لَا يُؤْمِنُونَ﴾

109. Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukomo wa viapo vyao, kuwa ikiwafikia ishara bila shaka wataiamini. Hakika ishara ziko kwa Mwenyezi Mungu tu. Na ni kitu gani kitakachowatambulisha ya kuwa zitakapowafikia hawataamini?

﴿وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَذَرُهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ﴾

110. Na tutazigeuza nyoyo zao na macho yao kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza, Na tutawaacha katika upotevu wao wakimangamanga.

## MSIWATUKANE

**Aya 108-109**

### MAANA

Wala msiwatukane wale wanaoomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua.

Wamesema kuwa Waislamu walikuwa wakiwatusi makafiri na wao huwajibu kwa kumtukana Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kauli hii haiko mbali sana na maana. Mara nyingi hutokea hivyo kwa wanaotofautiana kidini.

Tamko la Aya pia halilikatai hilo, bali imepokewa kutoka kwa Imam Jafar Aswadiq (a.s) kwamba aliulizwa kuhusu kauli ya Mtume: **"Hakika shirki inajificha zaidi kuliko mtambao wa chungu kwenye jiwe jeusi katika usiku wa giza"**

Akajibu: **"Waumini walikuwa wakiwatukana wanaoabudiwa na washirikina na wakawa wanamtukana anayebudiwa na waumini. Waumini wakakatazwa kuwatukana waungu wao ili makafiri wasimtukane Mungu wa waumini.**

Kama kwamba waumni wamemshirikisha Mwenyezi Mungu bila ya kujua, Kauli yake Mwenyezi Mungu 'bila ya kujua', Ni ishara ya ujinga wa washirikina. Katika Aya kuna ufahamisho wazi kuwa; ambalo lina madhara zaidi ya manufaa ni haramu na kwamba Mwenyezi Mungu hatiiwi anapoasiwa.

Kama hivyo tumewapambia kila umma vitendo vyao.

Maana ya dhahiri ya jumla hii ni kuwa Mwenyezi Mungu kama alivyowapambia vitendo vyao, vilevile amewapambia wengine vitendo vyao hata washirikina. Lakini hakuna mwenye shaka kwamba maana haya sio makusudio, kwa sababu Shetani ndiye anayewapambia washirikina uasi kwa nukuu ya Aya 43 ya Sura hii.

Zaidi ya hayo ni kuwa Mwenyezi Mungu hamwamrishi mja wake ukafiri na ampambie kisha amwadhibu, bali ni kinyume na hayo. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَلَٰكِنَّ اللَّهَ حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ﴾

"Lakini Mwenyezi Mungu ameipendezesha kwenu imani na akaipamba nyoyoni mwenu na amewaafanya muuchukie ukafiri na ufasiki na uasi" (49:7)

Kwa ajili hii tunatilia nguvu kuichukulia Aya kuwa Mwenyezi Mungu amewaumba watu katika hali inayoona vizuri vitendo anavyovifanya mtu na inayokwenda na desturi na akampa akili ya kupambanua baya na zuri. Lau angeliwaumba katika hali ambayo inaona ubaya wa vitendo vyake vyote, asingelifanya chochote. Haya ndiyo maana ya kauli yake hiyo Mwenyezi Mungu: 'Tumewapambia kila umma vitendo vyao' sawa na kauli yake:

﴿كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ﴾

"Kila kundi linafurahia kwa waliyo nayo" (23:53)

Nasi tunasema: "Kila mtu huridhia amali yake".

Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao, naye atawaambia yale waliyokuwa wakiyatenda.

Kwa hiyo waumini waache kutukana waungu wa washirikina, maadamu Mwenyezi Mungu atawaadhibu.

**Unaweza kuuliza**: kuwa anayemtukana Mwenyezi Mungu au Mtume wake ni wajibu kumuua, lakini mbona Aya hii inafahamisha kuwa ataachiwa hisabu yake na adhabu yake siku ya Kiyama?

**Jibu**: Aya hii ilishuka Makka, siku waislamu walipokuwa dhaifu, wakiwa bado hawajapewa ruhusa ya kupigana. Kwa sababu kupigana wakati huo kulikuwa ni kama kujiua. Ama ulipokuwa na nguvu Uislamu, ikawa ni wajibu kutekeleza hukumu ya kuuawa kwa mwenye kutukana; wala haijuzu kuchelewesha.

Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukomo wa viapo vyao, kuwa ikiwafikia ishara bila shaka wataiamini.

Mwenyezi Mungu (swt) alimpa nguvu Mtume wake Muhammad **(s.a.w.w)** kwa dalili za kutosha juu ya Utume wake, lakini washirikina wa Kikuraishi wakamtaka Muhammad **(s.a.w.w)** muujiza maalum na kufanya ndio sharti la kuamini kwao. Wakaapa kwa kiapo cha nguvu kuwa kama Muhammad atawakubalia maoni yao watamwamini. Ndipo Mwenyezi Mungu akamwamrisha Mtume wake kuwaambia:

Hakika ishara ziko kwa Mwenyezi Mungu huziteremsha kwa hoja inayowasimamia wote. Zaidi ya hapo huteremsha au huacha kuteremsha kwa hekima yake na kupitisha kwake.

Waumini wakatamani Mwenyezi Mungu aitikie maombi ya makafiri kwa kuwataka wasilimu na waamini. Mwenyezi Mungu akawaambia kwa kauli yake:

Na ni kitu gani kitakachowatambulisha ya kuwa zitakapowafikia hawataamini?

Yaani kutoka wapi mmejua kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) akiteremsha muujiza waliotaka makafiri wataacha kufuru yao na inadi yao? Yametangulia maelezo kwa ufafanuzi katika kufasiri Sura hii, Aya 34 - 37 na katika kufasiri Juz.1 (2:118)

Na tutazigeuza nyoyo zao na macho yao kama kama walivyokuwa hawakuamini mara ya kwanza.

Tutazigeuza nyoyo zao na macho yao ni fumbo la kujua Mwenyezi Mungu hakika yao, Dhamir ya kumwamini inamrudia Muhammad au Qur'an. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu anajua kuwa washirikina hawataamini baada ya kushuka muujiza waliotaka, bali wao wataendelea kung'ang'ania upotevu wao wa kwanza waliokuwa nao kabla ya kushuka muujiza wanaoutaka. Wao ni watafutaji wa batili na upotevu, na wala sio watafutaji wa haki na uongofu.

Na tutawaacha katika upotevu wao wakimangamanga.

Yaani baada ya kung'anga'ania upotevu, pamoja na kusimamishiwa hoja, tutawaacha na upotevu wao mpaka ifike siku watakayopata malipo ya amali yao, Yamekaririka maana haya katika Aya kadhaa.

## MWISHO WA JUZUU YA SABA

15

## SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

## YALIYOMO


**1** ............. **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
KIMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD
1 ........................................................ MUGHNIYYA
1 .............. KIMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA
1 ...... KIMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED
1 . KUPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU
1 ................................. UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI
1 ................................. UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI
2 ............................................... MAKOSA YA CHAPA
**3** ............. **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
3 ........... UADUI WA MAYAHUDI NA URAFIKI WAWAKRISTO
3 .............................................................. MAANA
4 .........NI NANI WALIO KARIBU NAWAISLAMU KIMAPENZI
6 ..............................................MSIHARAMISHE VIZURI
6 .............................................................. MAANA
7 ...................................................VIAPO VYA UPUUZI
7 .............................................................. MAANA
**9** ............. **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
9 ....................................................POMBE NA KAMARI
9 .............................................................. MAANA
10 ..................................... WENYE TAKUA NA KUAMINI
10 ............................................................ MAANA
HAKUNA KUWINDA KATIKA HARAM WALA PAMOJA NA
11 ................................................................. IHRAM
11 ............................................................ MAANA
12 .......... MAANAYA KUJARIBU KWA MWENYEZI MUNGU
**15** .......... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
15 ................................................ NYUMBA TAKATIFU
15 ............................................................ MAANA
16 ................................................. WINGI WA MWOVU
16 ............................................................ MAANA
17 ........................JE RIZIKI NI BAHATI AU MAJAALIWA?
19 ...........................................MSIULIZEULIZE MAMBO
19 ............................................................ MAANA
20 ...................................HAKUNA BAHIRAWALA SAIBA

21 ............................................................ MAANA
**23** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
23 ............................................... KUTHIBITISHAWASIA
23 ............................................................ MAANA
26 ............................MITUME NA SIKU YA KUKUSANYWA
26 ............................................................ MAANA
27 ...................................... ISA NA UTUME WA UTOTO
29 ....................................CHAKULA KUTOKA MBINGUNI
29 ............................................................ MAANA
30 WANAFUNZI WA MUHAMMAD (S.A.W.W) NAWA ISA (AS)
**32** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
32 ........................................................ ISSA NA WATU
32 ............................................................. LUGHA
32 ............................................................ MAANA
34 ............................................... UKWELI WAWAKWELI
34 ............................................................ MAANA
34 ................. MWISHO WA SURA YA TANO: AL - MAIDAH
35 ......................................KUUMBA MBINGU NAARDHI
35 ............................................................ MAANA
37 ..........................KUKANA HOJA ZA MWENYEZI MUNGU
37 ............................................................. LUGHA
37 ............ HAKUNA UDIKTETAARDHINI WALA MBINGUNI
**39** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
39 ........................LAU TUNGELIKUTEREMSHIA KARATASI
39 ............................................................ MAANA
42 .......................................AMEJILAZIMISHIA REHEMA
42 ............................................................ MAANA
44 HAKUNA MWONDOAJI MADHARA ILA MWENYEZI MUNGU
44 ............................................................ MAANA
**47** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
WANAMFAHAMU KAMAWANAVYO WAFAHAMU WANAWAO 47
47 ............................................................ MAANA
50 ...........................................NYOYO ZAO ZINA PAZIA
50 ............................................................ MAANA
52 ............................. WATAKAPOSIMAMISHWA MOTONI

52 ............................................................ MAANA
**54** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
54 .........................TUNAJUA KUWA YANAKUHUZUNISHA
54 ............................................................ MAANA
57 ............................... WANYAMA NA NDEGE NI UMMA
57 ............................................................ LUGHA
57 ............................................................ MAANA
59 ...................................................SEMA NIAMBIENI
59 ............................................................ MAANA
60 .......................... MWENYEZI MUNGU NA MAUMBILE
**62** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
62 ...... AKICHUKUA MWENYEZI MUNGU KUSIKIA NA KUONA
62 ............................................................ MAANA
64 ...............................SIFUATI ILA NINAYOPEWAWAHYI
64 ............................................................ MAANA
66 .................ASSALAMU ALAYKUM WA RAHMATULLAH
68 ............................................. SIFUATI HAWAA ZENU
68 ............................................................ MAANA
**70** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
70 ..................................... HAZINA YA SIRI IKO KWAKE
70 ............................................................ MAANA
73 ............................................................ WAOKOA
73 ............................................................ MAANA
75 ......... MPAKAWAINGIE KATIKA MAZUNGUMZO MENGINE
75 ............................................................ MAANA
**77** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
77 SEMA: JE: TUWAABUDU WASIOKUWA MWENYEZI MUNGU?
77 ............................................................ MAANA
79 ............................................................ MASUFI
80 ..................... IBRAHIM NA BABA YAKE NAWATU WAKE
80 ............................................................ MAANA
82 ....................JE, MNANIHOJI JUU YA MWENYEZI MUNGU
82 ............................................................ LUGHA
82 ............................................................ MAANA
**84** ........... **TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
84 .............................. NA TUKAMPA IS-HAQ NA YAQ'UB

84 ............................................................ MAANA
85 ................... HASAN NA HUSEIN NI WANAWA MTUME
HAWAMHESHIMU MWENYEZI MUNGU KAMA
88 .....................................................INAVYOTAKIWA
88 ............................................................ MAANA
89 ..... MITUME WA MWENYEZI MUNGU NAWANASAYANSI
**92 .......... TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
92 ......................KUMZULIA UWONGO MWENYEZI MUNGU
92 ............................................................ MAANA
94 ................................HUTOAALIYE HAI KATIKA MAITI
95 ............................................................ MAANA
95 ..........................................UHAI UMETOKAWAPI?
**99 .......... TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SABA**
99 ...........WAMEMFANYIA MWENYEZI MUNGU WASHIRIKA
99 ............................................................ MAANA
102 ......................................................MSIWATUKANE
102 ........................................................ MAANA
104 ............................... MWISHO WA JUZUU YA SABA
104 .........................................SHARTI YA KUCHAPA
105 ........................................................YALIYOMO